ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe.Balozi Seif Ali Iddi - MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6. Mhe. Haji Omar Kheri - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed - MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo - MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali - MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume - MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma - MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed - MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico - MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib - MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib - MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said - MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim - Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe

21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman - Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete

24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani

25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi

26. Mhe. Chum Kombo Khamis - Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake

27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla - Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake

29. Mhe.Juma Makungu Juma - Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini

30. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Jimbo la Mwanakwerekwe

31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Jimbo la Jang'ombe

32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil - Uteuzi wa Rais

33. Mhe. Ali Khamis Bakar - Jimbo la Tumbe

34. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani

35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele

36. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi

37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake

38. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani

40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake

41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi

42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake

43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo

44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo

45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy - Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake

75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga

76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu

77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais

78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani

79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake

81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni

82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni

85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake

86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 12 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2017/2018. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, pia naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2017/2018. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Bahati Khamis Kombo: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti naomba kuweka mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu majumuisho ya mijadala ya bajeti ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2017/2018. Mhe Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2017 NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/18. Sambamba na hotuba hii, naomba kuwasilisha vitabu viwili. Kitabu cha Kwanza cha Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo kwa Julai 2016 hadi Machi 2017 na cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2017 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/18. Taarifa zote hizo zimezingatia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar wa Awamu ya Tatu (MKUZA III) kwa kipindi cha mwaka 2016-2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2015- 2030 pamoja na Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoitoa kwenye uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba nitangulize hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba wa vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, ikiwa ni pamoja na sisi waja wake. Namshukuru kwa kutupa uhai, afya na uwezo na kukutana tena leo katika shughuli hii muhimu katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu nchi yetu na wananchi wake. Kwani baadhi ya wapendwa wetu tuliokuwa nao kipindi kilichopita leo hii hatunao tena duniani. Namuomba

Mwenyezi Mungu atuzidishie sote hekima na busara katika mijadala ya kikao hiki, atujaalie kheri, baraka na maelewano kati yetu. Atupe pia utulivu, upendo na mshikamano miongoni mwetu. Bila ya yeye, hatuna nguvu wala uwezo wa kufanya lolote.

Mhe. Spika, kwa moyo wa dhati naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi yake kubwa anayoifanya ya kuibadilisha Tanzania kuwa nchi ya utendaji zaidi kuliko maneno. Ni wazi kuwa kauli mbiu ya HAPA KAZI TU!!!! imeanza kuleta mabadiliko na mafanikio chanya yameanza kujitokeza katika ukuzaji uchumi hasa wa viwanda, kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato na hatimae kupungua kwa tatizo la ajira nchini na wananchi kufurahia matunda ya uhuru wao.

Mhe. Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naomba pia kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa jitihada zake kubwa za kuimarisha uchumi na kuinua huduma za jamii zikiwemo afya, maji na elimu. Ni wajibu wa mashirika yaliyopo nchini na nje ya nchi na wananchi kuunga mkono juhudi za Rais wetu mpendwa katika jitihada zake za kuiinua Zanzibar, ili ifikie uchumi wa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2020 kama Dira yetu ya Maendeleo inavyoelekeza. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango ya Zanzibar kwa uongozi makini katika maamuzi makubwa ya kuiendeleza nchi yetu katika masuala ya uwekezaji na maandalizi ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Hekima, busara na jitihada zake zimeendelea kuiweka Zanzibar katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Miongozo na hekima zake katika ukusanyaji wa mapato imeifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje katika kuendesha bajeti yake.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Msaidizi Mkuu wa Mhe. Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais kwa usimamizi wa shughuli za serikali, ushauri na kufanya kazi kwa karibu zaidi na Mhe. Rais. Tunaamini kuwa kwa umakini wa Kiongozi wetu huyu nchi yetu itaendelea kujengeka katika misingi ya utawala bora na kufuata sheria ili maendeleo yetu yawe endelevu. Kwa nafasi hii naomba pia kuwashukuru wajumbe wote wa Tume ya Mipango kwa miongozo na maelekezo wanayotupatia katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango mikuu ya kitaifa na ukuzaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba sasa nikushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Zuberi Ali Maulid kwa kuendesha na kusimamia vyema vikao vya Baraza letu. Hii inaonesha wazi ujasiri na umahiri ulionao katika kuviendesha vikao pamoja na shughuli nyengine za Baraza. Tumuombe Mwenyezi Mungu akuzidishie fikra, wepesi na moyo wa dhati katika utendaji wa kazi zako za kila siku. Ni matumaini yetu kuwa ushirikiano madhubuti, hekima na busara zitaendelezwa kama zilivyooneshwa na wasaidizi wako wote akiwemo Mhe. Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na Waheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Shehe Hamad Mattar Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, aidha kwa nafasi ya kipekee naishukuru Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi iliyo chini ya Uongozi wa Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa), Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, lakni vile vile nampongeza na kumshukuru sana Mhe. Bahati Khamis Kombo ambaye ni Makamu Mwenyekiti na kwenu Waheshimiwa Wajumbe wote kwa maoni na ushauri mliiotupatia. Mawazo yenu yamesaidia kuiimarisha taarifa hii na kuwa ni yenye matumaini kwa

wananchi wote. Kwa kuzingatia ya kwamba maendeleo ya taifa yanaletwa na wananchi wenyewe, ni matarajio yetu kuwa ushauri mliotupatia utatupa mwelekeo makini wa mahitaji ya wananchi wa Zanzibar. Ni imani yangu kuwa wajumbe sote tutapokea imani hii ya wananchi na ya Mhe. Rais kwa kuchapa kazi kwa bidii, uadilifu na uaminifu mkubwa ili kuiletea nchi yetu maendeleo yenye tija na ya haraka zaidi.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa imani yake kubwa kwangu na miongozo anayonipatia nikiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Niahidi kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa kufuata miongozo iliyopo ili nitekeleze majukumu yangu kwa mujibu wa sheria na kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Spika, kawaida nchi yetu hupata neema ya mvua mara mbili kwa mwaka, mvua za masika ambazo zinaanza (Machi – Mei) na mvua za vuli zinazoanza (Oktoba –Novemba). Kwa bahati njema mwaka huu tumepata mvua kubwa ya Masika. Hata hivyo, pamoja na neema hiyo, mvua pia imeleta madhara ya kupoteza maisha ya watu, uharibifu wa miundombinu, mali za umma na za wananchi. Natoa rambi rambi kwa familia zilizopoteza jamaa zao na wananchi waliopata maafa ya mvua hizo. Kadhalika nawapa pole walioathirika na upepo mkali ulioleta athari kubwa zikiwemo kuezua mabati, kubomoa kuta za nyumba na kuathiri miundombinu ya umeme. Serikali iko pamoja na wale wote walioathirika na maafa hayo tunawaomba wawe na subira na tuendelee kushirikiana kwa hali na mali katika kipindi hiki.

Mhe. Spika, niruhusu pia kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Donge kwa ushirikiano wanaonipatia na kuwaomba tuzidi kushirikiana na kunishauri kwa maslahi ya wanajimbo wote lakini kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Vile vile naishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono na kunisaidia kufanikisha majukumu yangu.

Mhe. Spika, hotuba yangu ya leo imegawika katika sehemu kuu mbili. Kwanza ni Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2016/17 na pili ni Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/18.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2016

Hali ya Uchumi Duniani

Ukuaji wa Uchumi

Mhe. Spika, hali ya uchumi wa dunia huathiriwa na mwenendo tofauti katika ukuaji wake kwa nchi zilizoendelea, zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi. Kwa mwaka 2016, kwa ujumla uchumi wa dunia umekua kwa wastani wa asilimia 3.1 ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2015. Uchumi wa nchi zilizoendelea ulikua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 2.1 kwa mwaka 2015. Kwa upande wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi kasi ya ukuaji wa uchumi ilikua kwa wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2016, ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2015. Vile vile, kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imepungua na kufikia wastani wa

asilimia 1.6 kwa mwaka 2016 kutoka wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2015. Kadhalika, uchumi wa nchi za Afrika ya Mashariki, kasi ya ukuaji wa uchumi imeongezeka hadi wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2016 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2015.

Mwenendo wa Mfumko wa Bei Duniani

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei duniani kwa mwaka 2016 imepungua na kufikia asilimia 1.9 kutoka asilimia 3.3 mwaka 2015. Kwa nchi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi, kasi ya mfumko wa bei ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2016, kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2015. Mfumko wa bei katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa wa wastani wa asilimia 11.3 mwaka 2016, ikilinganishwa na wastani wa bei wa asilimia 7.0 mwaka 2015. Katika nchi za Afrika Mashariki mfumko wa bei uliendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka 2016.

Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

Ukuaji wa Pato la Taifa

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar bado unaendelea kuimarika ikilinganishwa na wastani wa viwango vya kasi ya ukuaji wa nchi za Kanda ya Afrika Mashariki na zile zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Ukuaji wa shughuli mbali mbali za kiuchumi Zanzibar katika mwaka 2016 umeimarika zaidi ikilinganishwa na mwaka 2015. Pato halisi la Taifa lilifikia TZS 1,628 bilioni mwaka 2016 ikilinganishwa na TZS 1,188 bilioni mwaka 2015, sawa na ukuaji wa asilimia 6.8.

Ukuaji na Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016 shughuli za sekta ya viwanda zimeendelea kukua kwa kasi kubwa zaidi ikilinganishwa na ukuaji wa sekta ya kilimo na sekta ya huduma. Sekta ya viwanda ilifikia ukuaji wa asilimia 9.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.0 kwa sekta ya huduma na asilimia 5.7 kwa sekta ya kilimo. Sekta ndogo zilizokua kwa viwango vikubwa kwa mwaka 2016, ni pamoja na sekta ndogo ya mazao ambayo ilikua kwa asilimia 7.3, uchimbaji mawe na mchanga asilimia 18.8, umeme na gesi asilimia 8.2, usafirishaji na uhifadhi asilimia 5.1, sekta ndogo ya elimu asilimia 7.4 na sekta ndogo ya afya ni asilimia 3.1.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine sekta ya huduma imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kufikia asilimia 45.1 ikilinganishwa na sekta ya kilimo asilimia 25.7 na sekta ya viwanda asilimia 18.6. Sekta ndogo zilizoonesha kuwa na mchango mkubwa kwa mwaka 2016, ni pamoja na sekta ndogo ya mazao asilimia 15.1, sekta ndogo ya biashara na ukarabati asilimia 7.2, sekta ndogo ya ujenzi asilimia 8.7, sekta ndogo ya malazi na chakula asilimia 9.7, sekta ndogo ya ukodishaji majengo asilimia 7.2 na sekta ndogo ya utawala wa umma asilimia 4.2.

Pato la Mwananchi

Mhe. Spika, kufikia mwaka 2016, Zanzibar inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 1,455,000. Pato la Taifa lilifikia TZS 2,628 bilioni kutoka TZS 2,310 bilioni mwaka 2015 kwa bei za mwaka husika. Hivyo ongezeko la Pato la Taifa limepelekea kuongezeka kwa Pato la mtu binafsi kufikia

TZS 1,806,000 sawa na US$ 830 ikilinganishwa na TZS 1,633,000 sawa na US$ 818 mwaka 2015, hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 11.

Mfumko wa Bei

Mhe. Spika, serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili kulinda ustawi wa mtumiaji wa mwisho. Kasi ya mfumko wa bei imeongezeka kufikia asilimia 6.7 mwaka 2016 kutoka asilimia 5.7 ya mwaka 2015. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa za chakula kufikia asilimia 8.4 mwaka 2016 kutoka asilimia 7.4 mwaka 2015 na bei za bidhaa zisizo za chakula ziliongezeka kufikia asilimia 4.8 mwaka 2016 kutoka asilimia 4.0 mwaka 2015.

Viashiria vya Umasikini

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya mwaka 2014/15 umasikini wa kipato umepungua kutoka asilimia 34.9 mwaka 2009/10 na kufikia asilimia 30.4 mwaka 2014/15 na umasikini wa chakula umepungua kutoka asilimia 11.7 mwaka 2009/10 na kufikia asilimia 10.8 mwaka 2014/15.

SEKTA YA NJE

Biashara na Nchi za Nje

Mhe. Spika, Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka na kufikia TZS 96.2 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 42.4 bilioni mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 127. Vile vile, thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umefikia TZS 167 bilioni mwaka 2016 ikilinganishwa na thamani ya TZS 157 bilioni mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Nakisi ya biashara imepungua na kufikia thamani ya TZS 70.8 bilioni mwaka 2016 kutoka thamani ya TZS 114.5 bilioni mwaka 2015 sawa na upungufu wa asilimia 38.1 kutoka upungufu wa nakisi wa asilimia 21.5.

Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Mhe. Spika, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 138.1 bilioni mwaka 2016 kutoka thamani ya TZS 94.7 bilioni mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 45.8. Wakati, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umepungua na kufikia thamani ya TZS 84 bilioni mwaka 2016 kutoka thamani ya TZS 401.3 bilioni mwaka 2015 sawa na upungufu wa asilimia 79.1.

Mwenendo wa uingiaji wa Watalii

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya utalii, katika mwaka 2016 idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 28 kufikia watalii 376,242 kutoka watalii 294,243 mwaka 2015. Katika kipindi cha mwaka 2016 kumejitokeza masoko mapya ambapo Zanzibar imepokea watalii zaidi kutoka katika nchi za Urusi, Poland, Ukraine, China, India na Israel baada ya kuanzishwa kwa safari za moja kwa moja za ndege kutokea nchi za Ukraine, Israel na Uturuki.

Uwekezaji Binafsi

Mhe. Spika, idadi ya miradi mipya iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*), imefikia 16 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 150.5 milioni mwaka 2016 kutoka miradi 36 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 346.8 milioni mwaka 2015 sawa na punguzo la asilimia 56.6. Idadi ya ajira zilizozalishwa kwa mwaka 2016 zimepungua kutoka ajira 1,597 mwaka 2015 hadi ajira 1,071. Hali hii inaweza kuathiri shughuli za kiuchumi ikiwemo kupungua kwa uhaulishaji wa fedha za kigeni nchini kwa maana ya *(capital transfer)* na kukosekana kwa ajira hasa kwa vijana waliotarajiwa kupata ajira katika sekta hizo.

SEKTA YA FEDHA

Huduma za Benki

Mhe. Spika, Huduma za kibenki ni moja wapo ya sekta za kiuchumi ambazo zimekuwa zikiimarika kwa kasi katika kipindi cha miaka ya karibuni. Hadi Machi 2016 Amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 33.8 na kufikia TZS 718.3 bilioni kutoka TZS 536.8 bilioni katika kipindi kama hiki mwaka 2015. Hali hii ilichangiwa na uhamasishaji wa benki kutokana na ushindani ukiambatana na kuimarika kwa huduma za kibenki kupitia simu za mikononi. Mikopo katika benki iliongezeka kwa asilimia 77.3 na kufikia TZS 358.6 bilioni hadi Machi mwaka 2016 ikilinganishwa na TZS 202.3 bilioni zilizotolewa kipindi kama hiki mwaka 2015. Uwiano wa mikopo na amana uliongezeka kutoka asilimia 37.7 hadi asilimia 49.9.

Mhe. Spika, Kati ya mikopo ya TZS 358.6 bilioni iliyotolewa, mikopo katika miradi binafsi ilifikia asilimia 45.2, utalii asilimia 23.4, biashara asilimia 15.9, ujenzi asilimia 4.3 na mawasiliano na usafirishaji asilimia 2.3. Sekta zilizobakia kwa ujumla zilipokea mikopo ya asilimia 8.4.

Thamani ya Sarafu ya Tanzania

Mhe. Spika, Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani iliendelea kupungua katika kipindi cha mwaka 2016. Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilipungua kwa wastani wa asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 20.8 mwaka 2015. Hii ni kutokana na kuimarika zaidi kwa uchumi wa Marekani hasa katika masoko ya kifedha kulikopelekea mataifa makubwa duniani ikiwemo nchi za Ulaya na China kuwekeza zaidi nchini Marekani, hali iliyopelekea kupungua kwa mzunguko wa sarafu ya dola kwa nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania.

Mapato na Matumizi ya Serikali

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17 Serikali ilikadiria kukusanya mapato ya ndani jumla ya TZS 482.4 bilioni sawa na asilimia 18.4 ya Pato la Taifa. Matumizi yalikadiriwa kuwa TZS 841.5 bilioni sawa na asilimia 39.4 ya Pato la Taifa. Utekelezaji halisi kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2015 hadi Machi 2017 jumla ya mapato ya ndani yalifikia TZS 389.6 bilioni sawa na asilimia 108 ya makadirio. Mapato ya kodi yalifikia TZS 366.0 bilioni sawa na asilimia 108.6 ya makadirio ya TZS 337.0 bilioni na mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia kiasi cha TZS 23.6 bilioni ikiwa ni

sawa na asilimia 94 ya lengo la kukusanya TZS 25.2 bilioni kwa kipindi hicho.

Maendeleo ya Kiuchumi

Mhe. Spika, licha ya kuwepo kwa baadhi ya changamoto za ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, maendeleo ya kiuchumi na kijamii yameendelea kuonekana. Miongoni mwa maendeleo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

i. Kuimarika na kuongezeka kwa Pato la Taifa kutoka TZS 1,188 bilioni hadi TZS 1,628 sawa na ongezeko la asilimia 6.8.

ii. Kuongezeka kwa idadi ya wateja wapya waliounganishwa na huduma ya umeme katika Gridi ya Taifa kutoka wateja 12,366 mwaka 2015 hadi kufikia wateja 12,768 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 3.3;

iii. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kutoka TZS 306.1 bilioni Julai–Machi 2015/16 hadi kufikia TZS 389.6 bilioni Julai – Machi 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hili limepelekea kupungua kwa utegemezi wa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

iv. Kuimarika kwa utoaji wa huduma katika sekta ya afya kwa kuongezeka kwa madaktari kutoka madaktari 110 mwaka 2015 hadi madaktari 151 mwaka 2016. Kufikia mwaka 2016 uwiano wa daktari kwa wagonjwa Zanzibar ni daktari mmoja anahudumia wagonjwa 9,272 ambayo ni zaidi ya lengo la Shirika la Afya Duniani (*WHO*) kwa nchi zinazoendelea ambapo daktari mmoja anapaswa kuhudumia wagonjwa 10,000. Aidha, madaktari 132 wanatarajiwa kumaliza masomo hivi karibuni, hii itapelekea kufikia lengo lililowekwa na Chama cha Afro Shirazi la kuwa na daktari mmoja kwa wagonjwa 6,000;

v. Kuongezeka kwa watoa huduma na wauguzi kutoka 1,089 mwaka 2015 hadi 1,111 mwaka 2016;

vi. Kupungua kwa idadi ya wagonjwa waliolazwa kutoka 63,991 mwaka 2015 hadi 60,107 mwaka 2016 na kupungua kwa idadi ya wagonjwa wanaofika hospitali bila kulazwa kutoka wagonjwa 374,982 mwaka 2015 hadi 334,615 mwaka 2016 katika hospitali za Serikali sawa na kupungua kwa wagonjwa kwa asilimia 11;

vii. Kuongezeka kwa safari za usafiri wa anga kutoka safari za ndani 54,900 mwaka 2015 kufikia safari 59,901 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 9 na kuongezeka safari za kimataifa kutoka 7,196 mwaka 2015 hadi safari 8,572 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 19;

Mhe. Spika, Maendeleo mengine ni:-

viii. Kuimarika kwa miundombinu ya barabara mpya kwa kiwango cha lami kufikia kilomita 21.8 mwaka 2016 kutoka kilomita 7.8 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 179.5;

ix. Kuongezeka kwa usajili wa vyombo vipya vya moto nchini kutoka vyombo 15,646 mwaka 2015 hadi 16,022 mwaka 2016 sawa ongezeko la asilimia 2.4 hali iliyopelekea kuongezeka kwa mapato yaliyotokana na usajili wa vyombo vipya vya moto kutoka TZS 942.3 milioni hadi TZS 1.0 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 7;

x. Kuongezeka kwa wanafunzi walioandikishwa katika skuli za Serikali kutoka wanafunzi 36,608 mwaka 2015 hadi wanafunzi 45, 394 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 24;

xi. Kuongezeka kwa matumizi ya mtandao *(internet)* kutoka idadi ya watu 477,562 mwaka 2015 kufikia watu 556,477 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 16.5;

xii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mboga za majani kutoka tani 15,515 mwaka 2015 hadi tani 27,256 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 76 na kupelekea kupungua kwa uagiziaji wa bidhaa hizo kutoka asilimia 80 mwaka 2015 hadi asilimia 45 mwaka 2016;

xiii. Kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa nyumba, Hoteli na Ofisi katika miradi mbali mbali inayoendelea nchini ikiwemo miradi ya nyumba za makaazi inayosimamiwa na *ZSSF*, *ZIPA* na jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali;

xiv. Kuendelea kwa hali ya amani na utulivu nchini.

MASUALA MTAMBUKA

i) Upelekaji wa madaraka kwa wananchi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivi sasa imo katika utaratibu wa kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa *(Decentralization by Devolution – D by D* au ugatuzi*)*. Utaratibu huu unatumika katika nchi nyingi na umeonekana kuleta manufaa makubwa katika kuharakisha maendeleo ya wananchi. Hii ni kutokana na kuwashirikisha wananchi katika kupanga, kutekeleza na kutathmini mipango ya maendeleo katika maeneo yao.

Mhe. Spika, Utaratibu wa upelekaji wa madaraka kwa wananchi unahusu hatua za kuhamisha baadhi ya majukumu yanayotekelezwa na Serikali Kuu na kuyapeleka katika Serikali za Mitaa. Majukumu haya ni yale yanayohusu huduma za jamii pamoja na mazingira wezeshi ya kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja, vikundi au jamii nzima katika eneo dogo la nchi.

Mhe. Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa husimamia huduma za kisekta kwa ujumla ambapo taratibu za kuandaa mipango ya maendeleo hufanywa kwa kuwashirikisha wananchi na wawakilishi wao waliochaguliwa (madiwani) katika ngazi za chini za utawala. Serikali imeanza kugatua sekta za Elimu ya Maandalizi na Msingi, Afya ya Msingi na huduma za ugani katika sekta ya Kilimo na Sekta nyingine zitafuata kadiri hali itakavyoruhusu. Mapitio ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 yalibainisha kasoro ya kutokuwepo kwa madaraka ndani ya maeneo madogo. Hivyo, kuanzishwa kwa ugatuzi ni kulipatia suluhu tatizo hilo.

Mhe. Spika, Serikali ina nia ya dhati ya kufanya mabadiliko ambapo Mkakati maalumu wa miaka

mitatu umeshaandaliwa unaojikita katika maeneo manne yakiwemo uelewa wa dhana ya ugatuzi; mapitio ya sheria ili ziendane na mfumo wa *D by D;* marekebisho ya mifumo na taratibu za fedha pamoja na muundo wa kitaasisi, hali ya utumishi na usimamizi wake. Kuanzia Julai 2017 ambapo ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji, mkakati unakusudia kuweka vyema masuala ya uratibu na utekelezaji wa mpango, mapitio ya mifumo na taratibu mbalimbali ili kuanzisha michakato ya marekebisho, mapitio ya miundo na majukumu ya wadau mbali mbali.

ii) Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar

Mhe. Spika, Tutakumbuka ya kuwa mwaka 2016, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitia saini Sheria nambari 6 ya mwaka 2016 inayohusiana na Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar na hivyo kuweka milango wazi kwa Zanzibar kuanza kulishughulikia suala hilo. Katika utekelezaji wa Sheria hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia *(Zanzibar Petroleum Regulatory Authority- ZPRA)* ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za mafuta na gesi asilia zikiwemo uandaaji wa kanuni na miongozo muhimu ambayo itaiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Taasisi hiyo itahitaji vifaa vya kisasa na utaalamu katika masuala ya wahandisi wa miamba, wahandisi wa mafuta, wachumi, wachambuzi wa masuala ya fedha na wanasheria.

Mhe. Spika, mchakato wa kuanzisha Kampuni ya Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar *(Zanzibar Petroleum Development Cooperation-ZPDC)* uko katika hatua za mwisho ambapo kampuni hiyo ndiyo itakayokuwa na leseni za vitalu, kulinda maslahi ya Serikali katika uwekezaji na kushirikiana na makampuni ya kigeni katika kuendeleza shughuli za mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar. Ili kuongeza uelewa kwa wananchi, utoaji wa elimu ya masuala ya mafuta na gesi unaendelea kufanywa kupitia vipindi vya redio, televisheni na mikutano mbali mbali ya wadau.

iii) Nishati inayorejesheka

Mhe. Spika, Serikali imechukua juhudi mbali mbali katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na umeme wa uhakika wakati wote. Kwa kutambua hilo, Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*) iliandaa mradi wa miaka mitatu wenye jumla ya *Euro* 3.0 milioni ukiwa na lengo la kuangalia uwezekano wa kuzalisha umeme hapa Zanzibar kwa kutumia nishati inayorejesheka ya jua na upepo.

Mhe. Spika, katika kufanikisha hilo, utafiti wa nishati ya jua na upepo ulifanyika na matokeo ya awali yanaonesha kuwa vipimo vya kuangalia mwenendo wa upepo na upatikanaji wa jua viko katika viwango vizuri. Wastani wa mwenendo wa upepo umeonekana kufikia kasi ya mita 6.35 kwa sekunde moja (6.35m/s) na kwa upande wa nguvu za jua matokeo yanaonesha kuwa kwa eneo la mita moja ya mraba lina uwezo wa kuzalisha kilowati 5.46 za umeme kwa siku moja (*5.46 kwh/m2/day*) viwango ambavyo vinatosheleza kwa mipango ya uwekezaji. Vipimo hivyo vinafanyiwa uchambuzi na Kampuni ya *GOPA-INTEC* kutoka Ujerumani na hatimae kuandaliwa ripoti ya Upembuzi yakinifu itakayojumuisha mipango ya usafirishaji wa vifaa *(logistic plan)*, uchambuzi wa kimazingira, taratibu za fedha zitakazokimu miradi ya nishati inayorejesheka na uwezo wa miundombinu ya umeme iliyopo ili kuelewa umadhubuti wake wa kuhimili na kusafirisha umeme utakaozalishwa kutokana na nishati inayorejesheka.

Mhe. Spika, mazingira ya kisheria na leseni ni muhimu katika utekelezaji wa miradi ya nishati inayotokana na jua na upepo. Kazi hii inafanywa na kampuni ya *MHW* kutoka Ubelgiji. Sambamba na hiyo kazi nyengine zinazoendelea ni uchambuzi wa kina wa gharama na faida ya miradi katika uwekezaji *(Cost/Benefit Analysis)*, Kujenga mazingira shirikishi kisekta upande wa Serikali na sekta binafsi katika utekelezaji wa Miradi ya nishati inayorejesheka pamoja na kujenga uelewa kwa Taasisi za Serikali, wawekezaji binafsi na wananchi kwa ujumla juu ya nishati inayorejesheka na matumizi bora ya nishati hiyo.

iv) Upungufu wa Mchanga na hatua za utatuzi wake

Mhe. Spika, Uchimbaji wa mchanga Zanzibar unafanyika kwa kufuata utaratibu wa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2015 ya usimamizi wa Mazingira. Kwa muda mrefu uchimbaji wa rasilimali hiyo ulikuwa ukifanywa na watu binafsi wenye kumiliki maeneo husika. Hali hiyo imepelekea uchimbaji mchanga usiofuata viwango na sheria za nchi na wenye kuathiri kwa kiasi kikubwa mazingira na maeneo ya kilimo.

Mhe. Spika, **k**ukosekana kwa Sera ya Ujenzi na kutofuatwa kwa sheria na Mpango wa Matumizi ya Ardhi pamoja na kuongezeka kwa kasi ya maendeleo ya ujenzi kumepelekea kuongezeka kwa kasi ya uchimbaji mchanga na kupungua kwa rasilimali hiyo kwa kiasi kikubwa. Kasi ya ujenzi nchini imeongezeka kutokana na mwamko wa wananchi wa kuwa na makaazi bora ya kuishi. Hali hii imepelekea kukua kwa mahitaji ya vifaa vya ujenzi kama vile mawe, mchanga na kokoto ambazo ni rasilimali muhimu kwa kazi za ujenzi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya utafiti ili kujua hali halisi ya upatikanaji na matumizi ya mchanga kwa Unguja na Pemba. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kwamba katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kuanzia 2005 – 2015, Unguja ilichimba tani 2,658,503 na Pemba ilichimba tani 200,959 za mchanga kutoka katika machimbo rasmi yaliyoidhinishwa na Serikali. Kiwango hiki ni sawa na wastani wa tani 241,682 kwa mwaka kwa Unguja na tani 18,269 kwa Pemba. Takwimu hizo ni sawa na uchimbaji wa wastani wa tani 20,140 kwa mwezi kwa Unguja na tani 1,522 kwa Kisiwa cha Pemba. Naomba nitoe indhari kuwa hizo ni takwimu za uchimbaji halali. Katika kipindi hicho cha miaka 10 jumla ya hekta 522 (Unguja) na hekta 150 (Pemba) zilichimbwa mchanga.

Mhe. Spika, Kiwango hicho cha matumizi ni kikubwa sana hasa kwa nchi ya visiwa kama Zanzibar. Hivyo, kutokana na matokeo ya utafiti huo, kuanzia tarehe 6 Machi 2017, serikali imeamua kuchukua hatua za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na rasilimali ya mchanga. Hatua hizo ni pamoja na kuweka suala la mchanga moja kwa moja katika udhibiti na usimamizi wa serikali, kuanza kufikiria matumizi ya teknolojia mpya, kuelimisha jamii kuhusu hali halisi ya upungufu na upatikanaji wa mchanga pamoja na kuangalia uzoefu wa nchi nyengine za visiwa *(Seychelles, Mauritius na Comoro)* juu ya matumizi endelevu ya Rasilimali ya Mchanga.

Mhe. Spika, usimamizi bora wa uchimbaji mchanga unaofanywa moja kwa moja na serikali umeanza kuleta mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kufuatwa kwa utaratibu wa sheria na viwango vya mazingira pamoja na kuongezeka kwa mapato, kutoka TZS 100 milioni kwa mwezi

hadi wastani wa TZS 584 milioni kwa mwezi. Uchimbaji wa mchanga unaofanywa na Serikali umezingatia mapato na ada ya serikali, Ada ya Halmashauri husika, Malipo ya Urejeshaji eneo na Malipo ya Fidia ya Mazao na Vipando. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kushirikiana na wananchi, makampuni ya watu binafsi na wadau wote ili kuhakikisha matumizi bora na endelevu ya maliasili zisizorejesheka yanafanyika kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vya baadae.

v) Utekelezaji wa Programu za kimkakati

Mhe. Spika, MKUZA III umeainisha programu za kimkakati ili kuwezesha Mkakati wa Awamu ya Tatu kutekelezeka na kuharakisha maendeleo. Programu za Kimkakati '*Flagship programs'* ni zile programu muhimu ambazo utekelezaji wake utaleta matokeo ya haraka na yenye tija katika ukuzaji wa uchumi na utekelezaji wa programu/miradi na shughuli nyengine. Programu hizo zinajumuisha mpya na zinazoendelea ambazo zitasaidia kurahisisha juhudi za kuimarisha utalii na maendeleo ya viwanda vidogo vidogo na vya kati nchini zikiwa ni sekta kuu katika awamu ya tatu ya *MKUZA*. Katika kuimarisha sekta hizo, programu zilizochaguliwa zimejikita katika maeneo sita nayo ni:-

xv. Kuimarisha maeneo ya uingiaji nchini ambayo hujumuisha programu na miradi ya kuimarisha bandari na viwanja vya ndege pamoja na ununuzi wa meli;

xvi. Kuimarisha Miundombinu: Eneo hili linajumuisha programu na miradi ya ujenzi wa barabara, uimarishaji wa njia za umeme pamoja na nishati inayorejesheka *(renewable energy)* ya umeme na maeneo huru ya kiuchumi (SEZs);

Mhe. Spika, Maeneo mengine ni:-

xvii. Kuimarisha Sekta za Uchumi: Eneo hili linahusisha programu na miradi ya uimarishaji wa uvuvi wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini; uwezeshaji wa umwagiliaji maji na ujenzi wa miundombinu, maendeleo ya viwanda, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi na uimarishaji sekta ya utalii;

xviii. Kukuza Uwezo wa Watu: Eneo hili linajumuisha programu na miradi ya kuimarisha ubora wa elimu, kujenga uwezo katika fani zenye upungufu wa wataalamu hasa katika sekta za afya, kilimo, viwanda, mafuta na gesi, mafunzo ya amali na uendelezaji wa ujasiriamali.;

xix. Uwekezaji katika Sekta za Jamii: Eneo hili linahusisha uimarishaji wa miundombinu ya afya, maji, ujenzi wa nyumba za bei nafuu na za kibiashara;

xx. Utawala Bora na Uimarishaji wa Taasisi: Eneo hili linajumuisha programu na miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uwekaji wa mji katika hali ya usalama pamoja na uanzishwaji na uimarishaji wa taasisi muhimu katika kuimarisha viwanda na utalii.

Mheshimiwa Spika, Jumla ya programu za kimkakati 17 zimeainishwa katika kipindi cha miaka minne itakayotekelezwa na Serikali, Washirika wa Maendeleo, sekta binafsi pamoja na ushirikiano wa sekta za umma na binafsi. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali imeanza maandalizi ya utayarishaji wa maandiko muhimu hasa upembuzi yakinifu ili kuweza kuelewa uhalisia, faida

na gaharama za programu na miradi hiyo. Mazungumzo na Washirika wa Maendeleo yameanza ili kupata msaada wa kiufundi na hatimae fedha za utekelezaji.

vi) Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, Masuala ya kuwalinda wanawake na watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ni miongoni mwa mambo yanayozingatiwa na kutiliwa mkazo. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeandaa Mpango Kazi wa miaka mitano (2017-2022) kwa ajili ya kupambana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ambao uko katika hatua za mwisho ya kuzinduliwa rasmi. Jitihada nyengine zilizofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa askari polisi 31 kutoka vituo vya polisi vya Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapatia taaluma na ujuzi ili waweze kushughulikia matukio yanayoripotiwa kwa uweledi zaidi.

Aidha, elimu ya udhalilishaji, namna ya kuripoti na kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji imetolewa kwa wanafunzi wa skuli 16 (sita kutoka Wilaya ya Magharibi 'A', saba kutoka Wilaya ya Magharibi 'B' na tatu kutoka Wilaya ya Mjini) pamoja na madrasa nane za Qur- an. Jumla ya kamati 41 (21 Unguja na 20 Pemba) za malezi za wazazi zimepatiwa mafunzo yaliyohusu majukumu ya kamati, dhana ya udhalilishaji, athari na namna ya kujikinga na vitendo vya udhalilishaji. Aidha, urushaji wa matangazo ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji umefanyika kupitia ZBC TV, ZBC Radio na Spice FM Radio. Jumla ya matangazo 1,674 yamesharushwa yenye lengo la kuelimisha jamii katika kuhakikisha jamii inakuwa huru dhidi ya vitendo vya udhalilishaji.

Mhe. Spika, jumla ya malalamiko 143 (Unguja 87 na Pemba 56) yalipokelewa na kupatiwa ushauri na maelekezo kama ifuatavyo: Madai ya mahari ni matano, kupigwa 22, kutoroshwa matatu, migogoro ya ndoa 22, madai ya mali baada ya kuachana 11, kutelekezwa na waume 50, madai ya shamba na nyumba matano, kubakwa moja, kupewa ujauzito tisa, migogoro ya familia minne, madai ya fedha ni moja, shambulio la matusi ni mawili, msaada wa makaazi mawili, msaada wa nauli mawili, kukatishwa masomo ni moja, migogoro ya ardhi miwili na kashifa katika mtandao ni moja.

Serikali itaendelea na juhudi zake za kuimarisha vyombo vya kisheria, kutoa elimu kwa jamii na kutekeleza Mpango kazi uliotayarishwa ili kuhakikisha kuwa udhalilishaji wa aina zote unatokomezwa hapa nchini. Tunatoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika vita hii kwa kuripoti mara tu tukio linapotokea, kuwa tayari kutoa ushahidi katika vyombo vya kisheria na kupunguza muhali kwa ndugu na jamaa wasiopenda maendeleo ya wanajamii wengine.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO 2016/17

Mhe. Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17 ni sehemu ya mwanzo ya utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Tatu (MKUZA III). Mkakati huo umegawika katika maeneo makuu matano ya matokeo kama ifuatavyo: (i) kuwezesha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu; (ii) kukuza uwezo wa watu; (iii) kutoa huduma bora kwa wote; (iv) kuweka mazingira endelevu na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi; na (v) kushikamana na misingi ya utawala bora. Nyaraka mbalimbali zimeandaliwa zitakazosimamia na kurahisisha utekelezaji wa MKUZA III.

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 25 na miradi 38 (programu moja na miradi saba ni mipya) ya maendeleo ambapo ulitegemewa kugharimu jumla ya TZS 395.9 bilioni kupitia maeneo makuu matano ya matokeo ya MKUZA III. Serikali ilipanga kutoa TZS 71.1 bilioni sawa na asilimia 18 ya bajeti yote ya maendeleo ambapo kati ya hizo, TZS 58.0 bilioni ni kwa miradi ya vipaumbele, yenye mikataba au dhima *(commitment)* na TZS 13.1 bilioni kwa miradi mengine. TZS 324.8 bilioni sawa na asilimia 82 zilipangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo TZS 89.2 bilioni ni ruzuku na TZS 235.6 bilioni ni mkopo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2016/17, programu na miradi mbali mbali iliyotarajiwa kupata fedha nyingi haikuanza au kuendelea na utekelezaji kutokana na sababu mbali mbali. Miradi hiyo ni pamoja na uendelezaji wa ujenzi wa jengo jipya la Abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume *(Terminal 2)* lililokadiriwa TZS 144.4 bilioni takriban asilimia 37 ya bajeti yote ya Maendeleo ya 2016/17; ujenzi wa barabara ya Wete-Chake TZS 6.4 bilioni, kujenga uwezo wa utendaji kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji TZS 4.0 bilioni; Programu ya *UNDAP* II yenye jumla ya TZS 3.53 bilioni inayojumuisha miradi ya kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa TZS 120.4 milioni; kuimarisha misaada Zanzibar – TZS 250.0 milioni; kujenga uwezo wa taasisi za Serikali - TZS 306.4 milioni; kuimarisha mazingira ya uendeshaji biashara – TZS 500.0 milioni; kuimarisha usimamizi wa mazingira, maliasili na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi - TZS 1.7 bilioni na kujenga uwezo wa Kitaifa wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi – TZS 654.2 milioni.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo kufikia Machi 2017, jumla ya TZS 124.4 bilioni zilipatikana sawa na asilimia 31.4 ya bajeti ya maendeleo ambapo TZS 37.9 bilioni zilitolewa na Serikali sawa na asilimia 53.4 na TZS 86.5 bilioni sawa na asilimia 26.6 zilitolewa na Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, upatikanaji wa kiwango hiki cha fedha kwa miezi tisa kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni ongezeko la asilimia 13.4 kwa fedha zote zilizopatikana kwa upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo ikilinganishwa na asilimia 18 ya fedha za bajeti ya maendeleo zilizopatikana kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16. Kati ya fedha hizo Serikali ilichangia jumla ya TZS 14.6 bilioni sawa na asilimia 28 ya bajeti ya Serikali na Washirika wa Maendeleo walichangia TZS 54.3 bilioni sawa na asilimia 16 ya bajeti ya Washirika wa Maendeleo.

UTEKELEZAJI WA MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2016/17

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendelea kuviimarisha vipaumbele vya mwaka wa 2016/17 kwa maeneo ambayo yalihitaji uwekezaji wa muda mrefu ili kufikia malengo ya maendeleo ya nchi. Maeneo hayo ni pamoja na kukuza uchumi kwa ujenzi wa miundombinu ya usafiri, kilimo, uvuvi, utalii, kuongeza ajira hususan kwa vijana; kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama; na kuimarisha mazingira. Kutokana na vipaumbele hivyo, Serikali iliweka mikakati mbali mbali ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unaendana na maendeleo ya wananchi na kuwa endelevu. Utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 ni kama ifuatavyo:

Kuendeleza Miundombinu ya Msingi ya Barabara, Bandari, Viwanja vya Ndege na Nishati

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi Unguja na Pemba shughuli kadhaa za kuendeleza miundombinu ya msingi zimefanyika zikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe –Fuoni yenye njia mbili yenye jumla ya kilomita nane na kuanza kufanya tathmini kwa nyumba na vipando katika eneo la barabara ya Wete – Chake. Ujenzi wa barabara ya Ole– Kengeja yenye urefu wa kilomita 35 unaendelea ambapo kilomita 11 kutoka Ole mpaka Mfikiwa zimeshawekwa tabaka la mwisho na kufikia hatua ya kuwekwa lami na ujenzi wa madaraja madogo 10 na madaraja makubwa mawili umefanyika. Barabara ya Jendele- Cheju-Kaebona eneo la kilomita 11.7 tayari zimeshawekwa lami hatua inayoendelea sasa ni ukamilishaji wa kilomita 1.3 pamoja na uwekaji wa alama za barabarani.

Mhe. Spika, kwa upande wa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri na viwanja vya ndege mambo yafuatayo yamefanyika:

i) Bandari ya Mpigaduri, kazi za uandaaji wa upembuzi yakinifu, tathmini ya kimazingira na mkataba wa ujenzi zimekamilika na hatua inayoendelea ni kukamilisha mikataba ya ubia kwa mradi na mkopo. Mkandarasi wa ujenzi ameanza kufanya uchunguzi wa udongo *(Geotechnical Investigation).*

ii) Jengo jipya la abiria katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA Terminal 2), Serikali imeshawasilisha tarifa zote zilizohitajiwa na sasa inasubiri idhini ya fedha za ziada kutoka benki ya *EXIM* ya China ili shughuli za ujenzi ziendelee.

iii) Zoezi la kumtafuta mshauri elekezi linakamilishwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa Uwanja wa Ndege Pemba.

Mhe. Spika, katika kuendeleza miundombinu ya nishati, Serikali inaendelea na hatua za kufikisha umeme katika kisiwa cha Fundo ambapo ujenzi wa laini kubwa na ndogo za umeme umefanyika sambamba na ufungaji wa transfoma nne katika maeneo ya Ndooni, Ngadu, Mabaoni, na Kimeleani. Kazi iliyobaki ni uwekaji wa nyaya za chini ya bahari *(submarine cable)* kutoka Ukunjwi hadi Fundo. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu wa Juni mwaka 2017. Kukamilika huko kutapelekea ndugu zetu wa Fundo nao kuwa na fursa ya kuungiwa umeme kutoka katika Gridi ya Taifa.

Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (Results for Prosperity- R4P)

Mhe. Spika, Utekelezaji wa Programu ya Matokeo kwa Ustawi (R4P) inayohusisha programu tatu unaendelea ambapo rasimu ya Sera ya Utalii tayari imeandaliwa na iko katika majadiliano kwa ngazi mbali mbali. Aidha, katika kukuza utalii, Serikali imewezesha ushiriki katika maonyesho ya kuutangaza utalii wa Zanzibar nchini Ujerumani na Dubai. Vile vile, maonyesho na matamasha mbali mbali ya kibiashara yamefanyika. Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi wa mashine 1,000 za kielekroniki za kutolea risiti (*Electronic Fiscal Devices - EFD*) zenye uwezo wa kutumia teknolojia ya mfumo wa '*Virtual Fiscal Device' (VFD*) ambayo inaonekana kuwa salama zaidi na rahisi kwa watumiaji. Kanuni zitakazotumika katika usimamizi wa mashine hizo

zimeshaandaliwa ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi za serikali. Kuchelewa kwa upatikanaji wa mashine hizi kumetokana na hatua ya kubadilisha mashine zilizopendekezwa awali na kutafutwa kwa mashine zinazoweza kuwa na mfumo wa kurikodi zaidi ya matumizi ya kutoa risiti pekee.

Kuimarisha Huduma za Kijamii

Mhe. Spika, elimu ni ngao muhimu katika kupata ujuzi na maarifa. Serikali iliendeleza ujenzi wa kituo cha mafunzo ya amali kiliopo Makunduchi Unguja ambapo ujenzi umefikia hatua ya kusimamisha nguzo za msingi wa majengo sita. Kwa upande wa kituo cha mafunzo ya amali cha Daya, Pemba ujenzi wake umesimama kwa kipindi cha miezi 7 (kutoka mwezi wa Septemba 2016 hadi Machi 2017) kutokana na kuchelewa kufika kwa Msimamizi Mshauri wa ujenzi kwa kutokamilika kwa taratibu za Mkataba. Hali hiyo imepelekea Mkandarasi kuanza ujenzi bila kuwepo Msimamizi Mshauri ili kulinda muda wa Mkataba wake. Rasimu ya ripoti ya mwisho kutoka kwa Msimamizi Mshauri wa ujenzi tayari imewasilishwa kwa maamuzi ya kuendelea na ujenzi.

Mhe. Spika, katika kuimarisha elimu ya sekondari, skuli ya Kwarara imekamilika na ujenzi wa skuli tisa uko katika hatua za tathmini kwa wakandarasi na zinatarajiwa kujengwa katika maeneo ya Mwembeshauri, Bububu, Kinuni, Fuoni na Chumbuni kwa Unguja na Chake Chake, Micheweni, Kizimbani na Mwambe kwa Pemba imeandaliwa. Aidha, Mpango wa utoaji chakula kwa skuli za msingi za Kidagoni, Kijini, Mfurumatonga na Mbuyutende kwa Unguja na Makangale, Mgogoni, Mkiang'ombe na Kinowe kwa Pemba unaendelea.

Mhe. Spika, Utoaji wa huduma za afya umeimarishwa Unguja na Pemba. Hospitali ya Abdalla Mzee imeimarishwa na kufikia hadhi ya kuwa hospitali ya Mkoa. Jengo la kitengo cha huduma za mama na mtoto limekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kwa Unguja. Aidha, matengenezo ya jengo la huduma za macho katika hospitali ya Mnazimmoja yanatarajiwa kuanza hivi karibuni na ujenzi wa jengo la maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umekamilika, shughuli za umaliziaji zinaendelea ikiwemo uwekaji wa milango, madirisha na umeme.

Tunawashukuru sana ndugu zetu wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi na Norway kwa misaada yao katika huduma za Afya.

Mhe. Spika, katika kuongeza huduma za upatikanaji wa maji safi na salama na uimarishaji wa miundombinu na usambazaji wa maji mijini na vijijini jumla ya visima 14 vipya vimechimbwa na matengenezo yamefanyika kwa visima vikongwe 20 ambavyo vinatoa huduma kwa jamii katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba mijini na vijijini. Aidha, kazi za ujenzi wa matangi matatu ya kuhifadhia maji (Saateni mawili na Mnara wa mbao moja) umekamilika na matangi matatu katika maeneo ya Chaani, Donge na Kisongoni (Kinyasini) unaendelea ambapo kazi ya ulazaji mabomba katika maeneo hayo pamoja na maeneo ya Nungwi, Buyu, Matemwe na Kiombamvua kwa Unguja na Tumbe na Finya kwa Pemba imekamilika.

Kuimarisha Kilimo

Mhe. Spika, Katika kuimarisha kilimo taaluma za ukulima na ufugaji bora kwa vikundi 1,500 vya skuli za wakulima na wafugaji ilitolewa. Utafiti mmoja juu ya utengenezaji wa chakula cha

kuku kwa kuongezea virutubisho vya mwani unaendelea kufanywa kwa wafugaji. Matangi ya maji 80 pamoja na seti 140 za vifaa maalum vya umwagiliaji vimenunuliwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa mboga za majani. Aidha, wakulima wapatao 510 (Unguja 270 na Pemba 240) wamepatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mbinu bora za uzalishaji wa mpunga ikiwemo teknolojia ya kilimo shadidi.

Mhe. Spika, Katika kuwawezesha wafugaji, jumla ya vikundi 12 vya wafugaji wa ng'ombe kwa pamoja *(community cow shed)* vimeanzishwa na kupatiwa ng'ombe mmoja kwa kila mwanakikundi na vikundi 10 vya wafugaji wa mbuzi kwa pamoja *(community goat shed)* vimeanzishwa na kupatiwa mbuzi 45 kwa kila kikundi. Vile vile, jumla ya wafugaji 60 wa kuku wamepatiwa kuku 25 wa aina ya *'kuroiler'* kwa kila mfugaji ili kuweza kufuga kwa kutumia gharama nafuu za ulishaji wa kuku na kuweza kujiongezea kipato.

Mhe. Spika, ujenzi wa soko la samaki la Malindi umeanza kwa kuweka miundombinu muhimu ya maji, ununuzi wa vifaa vya umeme na ufungaji wa *transformer*. Aidha, taratibu za kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa soko hilo zimeanza. Katika ujenzi wa Kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki, hatua za ujenzi wa uzio na ukarabati wa majengo makongwe katika eneo la mradi zimeanza na ujenzi huo unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Aidha, mapipa 26 ya *Fibre* kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki, kaa na majongoo ya pwani tayari yameshawasilishwa katika eneo la mradi, na ujenzi wa kisima kimoja cha maji chumvi tayari umekamilika. Pia kampuni ya uvuvi *Zanzibar Fisheries Company - ZAFICO* imeshasajiliwa.

Kuimarisha Maendeleo ya Sekta ya Viwanda

Mhe.Spika; Serikali inaendelea na azma ya kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vya kati *SMEs* ili kuongeza ajira na kuimarisha uchumi. Katika kufanikisha azma hiyo, mapitio ya Sera ya viwanda vidogo vidogo na vya kati *SMEs* ya 2006 yamefanyika, miradi 145 ya wajasiriamali imetembelewa ili kuweza kujua maendeleo, changamoto na kutoa mapendekezo yanayostahiki sambamba na kuanza matayarisho ya Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda kwa kukusanya na kuchambua taarifa za awali ili kutayarisha Sera ya Viwanda. Baada ya uundwaji wa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar *ZAFICO*, Serikali imeanza utaratibu wa mazungumzo na kampuni mbali mbali ikiwemo kampuni ya Hairu ya Sri Lanka kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya usarifu wa samaki. Hatua za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taasisi ya Viwango Zanzibar *ZBS* na maabara eneo la Maruhubi zimekamilika pamoja na msambazaji wa vifaa vya maabara ya kemikali.

Kuendeleza Programu za Kukuza Ajira kwa Vijana

Mhe. Spika,Katika kuwawezesha vijana kupata ajira na kuongeza kipato, mafunzo ya kusindika mazao kwa wajasiriamali yametolewa katika kituo cha kulelea wajasiriamali kilichopo Mbweni. Jumla ya vijana 177 wamefaidika na mafunzo hayo kati ya hao vijana 53 walipata mafunzo ya usarifu wa mazao ya matunda na mboga za aina mbali mbali na vijana 124 walipata mafunzo ya ujasiriamali kwa nadharia na vitendo. Aidha, kwa upande wa Pemba eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kulelea wajasiriamali limepatikana huko Mbuzini na ramani ya jengo hilo imeshaandaliwa.

Kuongeza Juhudib za Kulinda Mazingira dhidi ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kitaifa na Jamii kwa Ujumla

Mhe. Spika**,** hifadhi ya Mazingira ni muhimu katika maisha ya mwanadamu. Kupitia eneo hilo matayarisho ya upandaji miti kwa kutoa mafunzo yanayohusiana na upandaji wa mikoko kwa jamii iliyozunguka maeneo yaliyoathirika imefanyika na vifaa vya upandaji wa miti pamoja na fedha za utayarishaji wa mabango ya sehemu za upandaji wa miti vimetolewa. Aidha, kazi ya ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari katika eneo la Kisiwa Panza inaendelea.

Kufanya Tafiti katika Sekta mbalimbali

Mhe. Spika**,** katika kuimarisha maendeleo ya sekta, tafiti ni muhimu ili kusaidia kutoa maamuzi sahihi. Serikali imeanza hatua za awali za kutafuta Washauri elekezi watakaokidhi viwango vilivyoainishwa katika muongozo wa tafiti ambapo washauri hao watafanyakazi za utafiti kwa kushirikiana na sekta husika. Tafiti hizo ni:

(i) Uhusiano wa Matumizi ya Vyakula na Maradhi Yasiyoambukiza *NCD's.*

(ii) Athari ya Kasi ya Ongezeko la Watu kwa Maendeleo ya Uchumi wa Zanzibar

(iii) Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na Teknolojia ya Usindikaji wa Bidhaa katika Kuongeza Mnyororo wa Thamani na Masoko;

(iv) Utalii Endelevu kwa Maendeleo ya Zanzibar na;

(v) Tathmini ya Mahitaji ya Uwezo na Ujuzi Unaohitajika kwa Sekta ya Umma Zanzibar.

Jukumu la utekelezaji wa tafiti nyenginezo ndani ya mawizara bado litaendelea kubaki kwa taasisi husika kupitia Idara za Sera, Mipango na Utafiti. Aidha, utafiti mdogo wa uzalishaji wa chumvi umefanyika kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wazalishaji wa Chumvi *Association of Zanzibar Salt Production Organisations - AZASPO*, iliyopo Pemba kwa ajili ya kuongeza ubora na thamani ya chumvi inayozalishwa.

Mhe. Spika,utafiti wa kubadilisha kizio kipya cha mwaka 2015 kwa Pato la Taifa unaendelea na utafiti kwa ajili ya kubadilisha kizio kipya cha faharisi za bei umekamilika. Utafiti juu ya Kuanzishwa kwa Eneo la Kuhifadhia Aina mbalimbali za Mimea ya Asili inayoanza kutoweka na athari zake kwa Utalii ndani na nje ya nchi umeendelea kwa hatua za awali za kutambua kundi maalum la aina ya mimea *Species* ambayo ipo katika hatari ya kutoweka katika maeneo ya Masingini. Utafiti juu ya Mchango wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2017/18.

Kuimarisha Misingi ya Utawala Bora na Kisheria

Mhe. Spika,Utawala bora ni msingi muhimu katika kufikia malengo yaliyopangwa katika nyanja zote ikiwemo uwajibikaji, utii wa sheria pamoja na upatikanaji wa haki. Kazi ya kuandaa mfumo

wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi umefanyika kwa kununua vifaa na kazi ya kutayarisha mfumo inategemewa kuanza hivi karibuni. Kwa upande wa ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu eneo la Tunguu matayarisho ya upatikanaji wa eneo la ardhi yamekamilika hatua inayofuata ni kulisafisha eneo na kutangaza zabuni kwa ajili ya michoro ya jengo hilo.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2017

Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

Mhe. Spika**,** mwelekeo wa ukuaji wa uchumi duniani kwa mwaka 2017 unatarajiwa kukua kwa wastani wa matokeo tofauti kimaeneo. Kwa ujumla uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2016. Uchumi wa nchi zilizoendelea unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 1.9 kwa mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2016.

Mhe. Spika, uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2017 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2016. Aidha, uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kufikia wastani wa ukuaji wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2016.

Mfumko wa Bei wa Dunia

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kupanda kufikia wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2017 kutoka asilimia 1.9 mwaka 2016. Nchi zilizoendelea, kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 1.9 kutoka asilimia 0.8 mwaka 2016 na nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi zinatarajiwa kufikia asilimia 2.9 mwaka 2017 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2016.

Mhe. Spika, kwa ujumla nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kuendelea kuwa katika tarakimu mbili kutoka asilimia 11.3 mwaka 2016 na kufikia asilimia 10.8 mwaka 2017. Hata hivyo, baadhi ya nchi zinazotarajiwa kuwa na kasi ya mfumko wa bei wa wastani wa asilimia 5 ni kama vile Angola, Nigeria pamoja na Zambia.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2017

Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2017 uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.1 kutoka asilimia mwaka 2016. Ukuaji huo, unatarajiwa kuchangiwa na masuala yafuatayo:-

i. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu ya usafiri, umeme, maji na mawasiliano;

ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kuwa katika tarakimu moja.

iii. Kuendelea kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia asilimia 23.5 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka wastani wa asilimia 22.6 mwaka 2016/17 sambamba na

kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato pamoja na matumizi yasiyo ya lazima;

iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 22.8 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka asilimia 21 mwaka 2016/17;

v. Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka na kufikia asilimia 41.3 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka asilimia 39.4 mwaka 2016/17;

vi. Nakisi ya bajeti inakadiriwa kuwa asilimia 3 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka nakisi ya bajeti ya asilimia 4.4 mwaka 2016/17;

vii. Kuimarika kwa sekta ndogo ya ujenzi kutokana na kuwepo kwa miradi ya uwekezaji ikiwemo miradi ya hoteli, nyumba za kuishi na ofisi za Serikali;

viii. Kuongezeka kwa maslahi ya wafanyakazi wa Serikali kwa ongezeko la mishahara ya kima cha chini kwa asilimia 100 na;

ix. Kuendelea kuimarika kwa amani na utulivu.

Mfumko wa Bei wa Zanzibar

Mhe. Spika, Hali ya mfumko wa bei inatarajiwa kuwa tulivu na kuendelea kubakia katika tarakimu moja kutokana na sababu zifuatazo:-

i) Kushuka kwa bei za bidhaa duniani kama vile nishati ya mafuta, mchele, sukari na unga;

ii) Serikali kuendelea kutoa punguzo maalum la ushuru kwa bidhaa muhimu za chakula;

iii) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuendelea kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa bei za bidhaa kwa wafanya biashara ili kudhibiti upandaji wa bei usio wa lazima;

iv) Kuongeza uzalishaji viwandani na kuendelea utoaji wa pembejeo kwa bei nafuu na kwa wakati kwa wakulima;

MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18

Mhe. Spika, Mwaka 2017/18 ni muendelezo wa utekelezaji wa *MKUZA III* ambao ni muhimu katika kufikia malengo ya muda mrefu tuliyojipangia. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2014/15 unaonesha umasikini wa kipato bado ni mkubwa. Jitihada za pamoja zinahitajika katika kuimarisha utoaji wa huduma bora, uzalishaji mashambani na viwandani ili kuongeza ajira kwa wananchi walio wengi na waweze kujitegemea.

Mhe. Spika, Mkakati wa awamu ya Tatu unakusudia kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa kuimarisha uchumi endelevu, kwa kujenga miundombinu imara, kukuza uzalishaji kwenye

sekta ya kilimo, uvuvi, utalii na viwanda vidogo vidogo; kuimarisha rasilimali watu; ubora wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, mazingira endelevu na misingi ya utawala bora.

MAENEO YA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2017/18

Mhe. Spika, kwa mwaka 2017/18, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar yameibuliwa kutoka Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020; Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Mohamed Shein katika Uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Tatu *MKUZA III.* Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini, barabara na nishati

Mhe. Spika**, m**aeneo ya uingiaji nchini yanayojumuisha bandari na viwanja vya ndege yataimarishwa kwa kukamilisha jengo jipya la abiria la uwanja wa Kimataifa wa Zanzibar wa Abeid Amani Karume *Terminal 2,* kuanza ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri, ununuzi wa meli mbili ya mafuta na abiria/mizigo. Kwa upande wa barabara, mkazo unawekwa katika ujenzi wa barabara za Bububu-Mahonda – Mkokotoni, ukamilishaji wa barabara ya Chake –Wete na uendelezaji wa barabara ya Fuoni –Tunguu. Maeneo mengine ni usambazaji wa umeme katika kisiwa cha Kokota; kuandaa nyaraka za kisheria juu ya nishati inayorejesheka *Renewable Energy,* uendelezaji na kufanya utafiti katika mafuta na gesi asilia.

Kuendeleza Utalii

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa katika uchumi wetu. Serikali itaendelea kuimarisha maeneo na vivutio vya utalii yakiwemo kumbukumbu ya mambo ya kale kwa kufanya matengenezo maeneo ya Mwinyimkuu Dunga, Beit al Ajaib na Mkumbuu; na uimarishaji wa utafutaji Rasilimali Fedha kwa ununuzi wa mashine za elektroniki za kutolea risiti.

Kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio

Mhe. Spika, Serikali imedhamiria kuimarisha viwanda vya mwani, mboga za majani, dagaa na chumvi kwa kutoa taaluma mbali mbali za kiufundi na kimasoko. Aidha, inakusudia kukiimarisha Kiwanda cha Makonyo Pemba, ujenzi wa Kiwanda cha Samaki, kuandaa sheria na Mwongozo wa Mamlaka ya Uendelezaji Viwanda vidogo vidogo *SMEDA*, kukamilisha Mkakati na Mpango kazi wa Maendeleo ya viwanda na kuimarisha Taasisi ya Viwango kwa ajili ya kupima ubora wa bidhaa na huduma.

Kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo

Mhe. Spika,Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Kibokwa, Kinyasini, Chaani, Makwararani na Mlemele. Kwa upande wa uvuvi, jitihada zitaongezwa katika kuendeleza uvuvi wa bahari kuu kwa kuimarisha utendaji wa Kampuni ya Uvuvi iliyoanzishwa hivi karibuni na kuvutia wawekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa soko la Samaki la Malindi na

uimarishaji wa ufugaji wa mazao ya baharini kwa kujenga kituo cha kulea na kutotolea vifaranga vya samaki Beit el Ras na uendelezaji wa miundombinu ya mifugo na wafugaji wadogo wadogo wa ng'ombe wa maziwa, kuku na mbuzi.

Kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama

Mhe. Spika, Serikali itaendelea kutoa huduma za jamii kwa faida ya wananchi wote. Katika sekta ya elimu mazingatio zaidi yatakuwa katika ukamilishaji wa madarasa 143 yaliyoanzishwa na wananchi; ujenzi wa skuli tisa za ghorofa ngazi ya Sekondari Unguja na Pemba, ukamilishaji wa ujenzi wa skuli ya Kibuteni na ujenzi wa dakhalia za wanaume katika skuli za Kibuteni na Mkanyageni na ununuzi wa madawati kwa skuli za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika sekta ya afya, hospitali ya rufaa ya Mnazimmoja inaendelea kuimarishwa. Hospitali ya Wete na hospitali ya Chake Chake zitafanyiwa matengenezo na kuimarishwa, hospitali ya Makunduchi na Kivunge zitaendelezwa kufikia hadhi ya kuwa za Mikoa na hospitali ya Micheweni na hospitali ya Vitongoji zitaimarishwa kufikia hospitali za Wilaya. Serikali itaendelea na matayarisho ya ujenzi wa hospitali ya Binguni, ukamilishaji wa jengo la Mkemia Mkuu wa Serikali na maabara yake na ununuzi wa dawa za utibabu, uchunguzi wa maradhi pamoja na zana na nyenzo mbali mbali. Aidha, mfumo wa uhifadhi wa damu salama kwa mama na mtoto utaimarishwa kwa ununuzi wa vifaa muhimu na kuanza ujenzi na matengenezo ya vituo vya afya 15 Unguja na Pemba.

Mhe. Spika**,** maji ni rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu. Kwa kufahamu hilo, Serikali itaendelea kuimarisha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijiji kwa kuviendeleza visima 26 vilivyochimbwa na Ras Al Khaimah na kuimarisha miundombinu na mfumo wa usambazaji maji pamoja na uwekaji wa vifaa muhimu. Kwa upande wa sekta ya michezo, Serikali inakusudia kuanza matayarisho ya ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya na kuendelea na ujenzi wa kiwanja cha michezo cha *Mao Tze Dong*.

Kukuza uwezo wa watu

Mhe. Spika, jamii iliyoelimika ndio ngao katika maendeleo ya Taifa kwa kutoa huduma na kujiajiri. Serikali itaongeza juhudi za kusomesha wataalamu wa afya, kutoa mafunzo ya amali na ujasiriamali na kuendelea na ujenzi wa vituo vya amali Daya na Makunduchi.

Utawala bora, uimarishaji wa taasisi, kukabiliana na maafa na mabadiliko ya tabianchi na uwekaji mji katika hali ya usalama

Mhe. Spika, Eneo la Utawala Bora limepewa umuhimu unaostahiki. Serikali itatilia mkazo uimarishaji wa taasisi kwa ajili ya kupeleka madaraka kwa wananchi, ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu, ujenzi wa Ofisi za Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa upande wa Pemba na kuanza matayarisho ya ujenzi wa Wizara ya Fedha na Mipango Unguja, kuanza ujenzi wa nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba, uimarishaji wa nyumba za makaazi na mahanga kwa vikosi vya KMKM na

Mafunzo, uendelezaji wa jengo la kurekebisha tabia kwa watoto huko Hanyegwa Mchana, na uwekaji kamera na vifaa vya ulinzi katika maeneo ya Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, Awali nilieleza kuhusu maafa yaliyosababishwa na mvua na upepo katika mwezi wa Mei 2017 hapa Zanzibar. Ili kupunguza athari za maji yatokanayo na mvua, Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu kupitia miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwemo mradi wa Huduma za Jamii Mijini *ZUSP* ambao kwa kuanzia umeonesha mafanikio katika maeneo yaliyotekelezwa kwa awamu ya kwanza ya uwanja wa Mnazimoja, Jang'ombe, Kariakoo, Chumbuni, Daraja Bovu na Karakana. Aidha, katika awamu ya pili ya mradi unakusudia pia kushughulikia maeneo yanayotuwama maji katika bwawa la Mwanakwerekwe. Kwa sasa, mradi upo katika hatua za tathmini ya kumpata Mshauri Elekezi.

RASILIMALI NA MWELEKEO WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO 2017/18

Mhe. Spika, kwa mwaka 2017/18, Mpango wa Maendeleo unalenga kutekeleza jumla ya programu 27 (programu mbili ni mpya) na miradi 47 ya maendeleo miradi 11 ni mipya. Jumla ya TZS 496.6 bilioni zitatumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS 100.7 bilioni sawa na asilimia 25.4 ikilinganishwa na bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2016/17 ya TZS 395.9 bilioni. Serikali imepanga kutumia TZS 116.1 bilioni sawa na asilimia 23.3 ya bajeti ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS 45.3 bilioni sawa na asilimia 63.9 ya bajeti ya maendeleo ya mwaka 2016/17. Kati ya fedha za Serikali (TZS 116.1 bilioni) TZS 67.4 bilioni ni kwa programu na miradi ya kimkakati, yenye mikataba au dhima *Commitment* na TZS 48.7 bilioni kwa miradi mengine. Jumla ya TZS 380.5 bilioni sawa na asilimia 76.7 zimepangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 82.2 bilioni ni ruzuku na TZS 298.3 bilioni ni mikopo. Fedha hizo ni ongezeko la TZS 55.7 bilioni sawa na asilimia 17.1 ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/17 zenye jumla ya TZS 324.8 bilioni.

Mhe. Spika, MKUZA III unatekelezwa kupitia Maeneo Makuu Matano ya Matokeo, hivyo mgawanyo wa fedha kwa programu na miradi ya maendeleo umejikita katika maeneo hayo kama ifuatavyo:

Eneo la Kwanza: Kuwezesha Ukuaji wa Uchumi Jumuishi na Endelevu

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha mazingira bora yatakayosaidia ukuaji wa uchumi endelevu ili kupambana na umasikini uliokithiri na kupunguza umasikini wa kipato. Matarajio ya muda wa kati wa eneo hili ni kuwa na mazingira rafiki kwa ukuaji wa sekta binafsi na upatikanji wa ajira, kuwa na uwekezaji wa umma unaotosheleza ili kusaidia miundombinu ikiwemo ya mawasiliano na vichocheo vyengine vya uchumi, kuwa na sekta yenye ushindani ya utalii yenye manufaa endelevu na jumuishi kwa Wazanzibari, kuwepo na uzalishaji wa kisasa katika sekta za kilimo na viwanda kwa kuongeza thamani *(value addition)* na kuwepo sekta binafsi iliyoshamiri.

Mhe. Spika, eneo hili linatarajiwa kutekeleza jumla ya programu 12 na miradi 11 (miradi miwili ni mipya) ambapo limetengewa jumla ya TZS 259.09 bilioni sawa na asilimia 52.2 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga TZS 33.95 bilioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 225.14 bilioni.

Eneo la Pili: Kukuza Uwezo wa Watu

Mhe. Spika, mkakati mpya unakusudia kuimarisha uwezo wa watu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Eneo hili lina matarajio ya kuongeza ajira kwa watu wote kwa makundi mbali mbali (vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na kadhalika) mijini na vijijini kwa kuendeleza maarifa yao na kuongezeka uwezo wa wajasiriamali ili kuimarisha fursa za kuweza kujiajiri.

Mhe. Spika, eneo hili linatarajiwa kutekeleza jumla ya programu mbili na mradi mmoja ambapo limetengewa jumla ya TZS 11.3 bilioni sawa na asilimia 2.3 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga TZS 2.0 bilioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 9.3 bilioni.

Eneo la Tatu: Kutoa Huduma Bora Kwa Wote

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha upatikanaji wa huduma bora na za kisasa kwa jamii. Matarajio ya eneo hili ni kuwa na huduma bora za afya na usafi wa mazingira, maji safi na salama, na kupambana na maradhi yenye kuambikiza na yasiyoambukiza; kuwa na elimu bora kwa wote na jinsia zote; kuwa na makaazi bora, matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa nishati; kuwa na udhibiti wa unyanyasaji wa watoto na wanawake; kuwa na uwezo na utayari wa kupambana na majanga/dharura za aina zote; kuwa na usalama wa upatikanaji wa chakula kwa jamii yote.

Mhe. Spika, eneo hili linatarajiwa kutekeleza jumla ya programu nane na miradi 17 (miradi miwili ni mipya) ambapo limetengewa jumla ya TZS 152.7 bilioni sawa na asilimia 30.7 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga TZS 26.5 bilioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 126.2 bilioni.

Eneo la Nne: Kuwepo Mazingira Endelevu na Uhimili wa Mabadiliko ya Tabia nchi

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha uwezo wetu wa kukabiliana na mabadiliko ya mazingira na tabia nchi. Matarajio ya eneo hili ni kuwa na uwezo wa kutosha wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi; kuwa na uhifadhi wa viumbe vya baharini na nchi kavu na kupunguza upotevu wake; kuzuia uharibifu wa mazingira na kupunguza athari za kijamii zinazotokana na shughuli za kiuchumi.

Mhe. Spika, eneo hili linatarajiwa kutekeleza jumla ya miradi miwili ambapo limetengewa jumla ya TZS 854.7 milioni sawa na asilimia 0.2 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga TZS 50.0 milioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 804.7 milioni.

Eneo la Tano: Kushikamana na Misingi ya Utawala Bora

Mhe. Spika, eneo hili linakusudia kuimarisha misingi ya utawala bora, haki na sheria katika ngazi zote. Matarajio ya eneo hili ni kuwa na mifumo ya kiutawala na kitaasisi yenye kuwajibika, iliyo wazi na bila ya rushwa; kufikia usawa na uwiano wa kijinsia, jamii jumuishi, na uwezeshaji

wa wanawake, watoto wa kike, vijana, watu wenye ulemavu na watu walio katika mazingira hatarishi; kuwa na upatikanaji wa haki, kuheshimu utawala wa sheria, haki za msingi za binadamu na ushirikishwaji katika mchakato wa demokrasia; kuwa na uwajibikaji wa mashirika kwa jamii na kuwa na mazingatio zaidi ya watu katika mipango.

Mhe. Spika, eneo hili linatarajiwa kutekeleza jumla ya programu tano na miradi 16 (miradi saba ni mipya) ambapo limetengewa jumla ya TZS 72.6 bilioni sawa na asilimia 14.6 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga TZS 53.6 bilioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 19.0 bilioni.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Hotuba yangu hii haiwezi kukamilika bila ya shukurani za kipekee kwa watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji Ndugu Juma Hassan Reli, Kamishna wa Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini, Kamishna wa Ukuzaji Uchumi, Kamishna wa Mipango na Maendeleo ya Watendakazi, Kamishna wa Ufuatiliaji na Tathmini na Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kusimamia kwa umahiri kazi za kila siku za Tume ya Mipango na maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Naomba pia kumshukuru Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Aidha, natoa shukurani kwa Makatibu Wakuu wa Wizara yote za SMZ na Watendaji wao kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika mchakato mzima wa matayarisho ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo yaliyofanikisha matayarisho ya Hotuba hii. Ni matumaini yangu kwamba ushirikiano huu utaendelea zaidi katika utekelezaji wa majukumu yetu katika mwaka unaofuata. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa namna ya kipekee naomba kuyashukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Nchi Wahisani kwa misaada ya kifedha na kiutaalamu wanaoendelea kutupatia wakiwemo AfDB, AGRA, BADEA, CDC, CHAI, CHINA, COSTECH, EGH, EGYPT, EU, EXIM BANK, FAO, FINLAND, GAVI, GF, GERMANY, GLOBAL FUND, GRFC, GOOD NEIGHBORS, GN, GPE, INDIA, ICAP, IFAD, ILO, IMF, OPEC, JAPAN, JICA, KOREA, MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - NETHERLAND, OMAN, PBZ, PMI, RAS - AL - KHAIMAH, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, SPAIN, SWEDEN, TFT, UK, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, UNIDO, URT, USA, USAID, UN- HABITAT, UN WOMEN, Benki ya Dunia na WHO. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baada ya kusema hayo, naomba sasa Baraza lako tukufu, lipokee, lijadili na kupitisha Mapendekezo ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2017 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba Kutoa Hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji wako wa hotuba yako, Waheshimiwa Wajumbe sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili nae sasa aje awasilishe hapa lakini wakati huo huo nitatoa muda kwa Mhe. Waziri wa Fedha ambaye baadae atakuja kuwasilishia Hotuba ya Bajeti kuu ya Serikali ili nae baadae atakuja kuwasilisha tena

kwa hiyo kwa kuanzia ili Mhe. Waziri wa Fedha apate muda kidogo wa kupumua naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Mwenyekiti karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): (Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Bajeti): Mhe. Spika, kwanza kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu anipe subira wakati nikisoma Hotuba yangu hii vile vile anipe uwezo mkubwa sana wakati nikisoma hotuba yangu hii baadae nitayaeleza kwa nini ningezungumza kitu hicho, lakini nataka niseme tu asili ya mwanadamu yoyote anapokosewa huo anasamehe kile kilichokuwa mbele niwaombe Wajumbe kama kuna watu wote wamewakosea basi wasamehewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mtukufu kwa kunijaalia neema ya uhai na kutuwezesha kukutana leo hapa hii, tukiwa katika hali ya uzima na afya njema kwa kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti, ili niweze kutimiza sehemu ya majukumu ya Kamati yangu yanayotokana na maelekezo ya Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, kwa kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya majumuisho ya Kamati ya Bajeti kuhusu mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, Kamati yangu inamshukuru sana Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, kwa kukubali mwaliko wa Kamati kuhudhuria katika kikao chetu cha majumuisho. Aidha, Kamati yangu inathamini hekma, busara na mchango wake alioutoa wakati wa kikao hicho zilichosaidia kutatua changamoto iliyojitokeza wakati wa kikao hicho, ambacho kimsingi Kamati yangu ilifanya kazi kwa niaba yako na Baraza lako Tukufu lakini hata hivyo Kamati yangu haikuridhika na maelewano duni yaliyofanywa na Mhe. Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar walioathirika kutokana na mvua za masika ambapo waliathirika sana miundombinu ya barabara, pamoja na watu na mali zao. Aidha, napenda pia kuwapa pole watu wote waliopata athari kutokana na upepo mkali uliovuma kwa baadhi ya maeneo katika nchi yetu na kusababisha hasara kubwa kwa wananchi, kwa kuharibikiwa na nyumba zao, nawaomba wananchi wote walioathirika kwa namna au nyengine wawe na subra, na Mungu awape wepesi.

Mhe. Spika, tokea tarehe 10, Mei Baraza hili limekuwa katika kipindi muhimu cha mjadala wa bajeti, ambapo bajeti za Wizara zote kumi na tatu (13) zimewasilishwa na kujadiliwa na Wajumbe. Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali michango na hoja mbali mbali ambazo Wajumbe wamezitoa hazikuwa na dhamira ya kuikwamisha Serikali wala kuikandamiza, badala yake zilikuwa katika hali ya kutekeleza wajibu wa kikatiba kwa chombo hichi na kuisimamia na kuishauri Serikali, kwa dhamira chanya ya kujenga ili kuifanya bajeti yetu iwe bora zaidi, na iwanufaishe wananchi, ambao ndio tunaowatumikia katika sekta zote. Hivyo, kwa dhati kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwa namna walivyotekeleza wajibu wao, kwa kuzichambua bajeti za Wizara zote pamoja na kuishauri Serikali na namna bora ya utekelezaji wa uhakika kwa michango yao na

ushauri wao umekuwa na umuhimu mkubwa katika kuhakikisha bajeti ya Serikali inaleta tija kwa wananchi.

Mhe. Spika, **s**hukurani maalum ziwaendee Wajumbe wa Kamati yangu ya Bajeti, kwa ushirikiano wao walionionesha na kazi kubwa waliyoifanya ya kuchukua hoja mbali mbali za kibajeti zilizotokana na mijadala ya bajeti, ambazo Kamati yangu imezifanyia kazi. Kwa hakika kazi ambayo haikuwa rahisi hata kidogo hasa kwa kuzingatia kwamba michango iliyotolewa ni mingi na ilikuwa na umuhimu sana.

Mhe. Spika, naomba nizitilie mkazo shukurani zangu kwa kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mohammed Said Dimwa	Mwenyekiti
2.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	Mjumbe
4.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
5.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe
6.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	Mjumbe
7.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe

Aidha, Kamati yangu ilisaidiwa kwa karibu sana na Makatibu wawili

1. Ndg. Abdalla Ali Shauri na
2. Ndg. Kassim Tafana Kassim

Nao tunapongeza kwa namna ya pekee kwa kazi kubwa ambazo walizokuwa wakizifanya. (*Makofi)*

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016, pamoja na mambo mengine ilianzisha Kamati ya Bajeti. Aidha, Kanuni ya 100(2) ya Kanuni hizo, inaelekeza Serikali kwa kushirikiana Kamati ya Bajeti kufanya majumuisho kuhusiana na hoja mbali mbali zitakazojitokeza wakati wa mjadala wa Makadirio ya bajeti za Wizara zote.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati yangu imetekeleza jukumu hilo, kwa umakini mkubwa ambapo kwa muda wote wa majadiliano ya bajeti imekuwa ikifanya kazi ya kukusanya hoja mbali mbali zilizotokana na michango ya Wajumbe pamoja na maoni ya Kamati za kisekta, Mhe. Spika, maoni ya Kisekta yaliyoanzishwa na Baraza kupitia taarifa zao. Kwa msingi huo Kamati yangu ilipata fursa ya kukaa pamoja na Serikali kwa lengo la kushauriana kuhusu hoja zilizojitokeza wakati wa mijadala ili kuangalia maeneo ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza au kupunguza sehemu ya fedha zilizokadiriwa na kushauri mikakati ya utekelezaji wake. Hivyo, taarifa hii ni mrejesho kwa Baraza lako tukufu juu ya matokeo ya mashauriano katika Bajeti hii.

Mhe. Spika, katika kulikamilisha zoezi la majumuisho Kamati yangu ilikaa pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Khamis Mussa Omar, pamoja na baadhi ya Watendaji wakuu wa Wizara hiyo. Aidha, Kwa kuwa hoja zilizojadiliwa na Kamati yangu zilihusu Wizara tofauti, kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi katika kikao cha mashauriano, Kamati yangu iliwaita Mawaziri wa Wizara zilizohusika na hoja ambao nao pia waliambatana na watendaji wakuu wa Wizara hizo ili kuweza kusaidia kutoa ufafanuzi na tunawashukuru sana walifika kwa wakati na waliheshimu kikao chetu.

Mhe. Spika, kwa kuthamini umuhimu na michango wa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Kisekta, Kamati yangu pia iliona ni busara kuwaalika Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Kisekta za Baraza hili. Hivyo kwa dhati kabisa Kamati yangu inawashukuru Wenyeviti, mawaziri pamoja na watendaji wakuu wa Wizara kuambatana na mawaziri wao kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi wa hoja ambao uliisaidia Kamati kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, naomba ifahamike kwamba, Kamati yangu imepata changamoto nyingi wakati wa kutekeleza jukumu hilo, pamoja na ukweli kwamba Kamati imepatiwa mafunzo ya kuijengea uwezo, hata hivyo Kamati hiyo haikjiutosheleza kutokana na ukweli kwamba Kamati haikupata fursa kubwa ya kuona kwa kivitendo mafunzo hayo, namna Kamati ya bajeti inavyofanya kazi, badala yake imepata mafunzo ya kinadharia tu yaani "*theory*". Aidha, kutokuwepo kwa Sheria ya Bajeti ambayo kimsingi ingeweza kusaidia kuipa nguvu Kamati pamoja na kubainisha majukumu na mipaka ya vyombo mbali mbali katika mchakato wa bajeti, pia ni sehemu ya changamoto hizo. Kwa upande mwengine Kamati yangu ilikabiliwa na changamoto ya muingiliano wa ratiba ya kazi ambapo takribani kwa muda wa wiki nzima Kamati ililazimika kukosa kufuatilia mijadala ya bajeti za Wizara moja kwa moja kutokana na kupangiwa ratiba ya kupitia miswada mitatu yanayohusiana na masuala ya kodi.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwaarifu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Kisekta kwamba wanajukumu muhimu la kuipata Kamati ya Bajeti changamoto za kibajeti za Sekta wanazozisimamia ambazo wanahisi zinahitaji nguvu na ufuatiliaji wa Kamati ya Bajeti. Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inalazimika kusema hivyo kutokana na ukweli kuwa Kamati za Kisekta ndio wanaojua zaidi uhalisia wa changamoto zinazojitokeza katika Sekta wanazozisimamia, lakini pia wana nafasi kubwa ya kujua uzito wa changamoto hizo na kama zinahitajika kuzifikisha mbele ya Kamati ya Bajeti.

YATOKANAYO NA MIJADALA YA HOJA

Mhe. Spika, sasa kwa heshima sana naomba sasa nisome yatokanayo na mijadala na hoja mbali mbali ziliozotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, maeneo yaliyochangiwa kwa wingi na mengi na kwa ujumla ni michango yote iliyotolewa ilikuwa ni muhimu na mizuri.

Mhe. Spika, naomba ifahamike kwamba wakatiwa kuchukua hoja zinazotokana na mijadala na Bajeti na Kisekta za Kamati yangu imejielekeza zaidi katika masuala ya Kibajeti na ambazo moja kwa moja yanahusu vifungu vya kibajeti, aidha Kamati pia ilizingatia baadhi ya hoja

ambazo zilichangiwa na Wajumbe kwa hisia tofauti kwa lengo la kupata maelezo zaidi kutokana na Serikali, kutoka Serikali na kuweza kuishauri kuhusu utekelezaji na maeneo haya kwa kuwa baadhi ya maeneo hayo yamekosa ufanisi wa kiutendaji kutokana na changamoto za kibajeti.

Mhe. Spika, baadhi ya maeneo yaliyochangiwa na Wajumbe wengi na kwa hisia zaidi ni pamoja na haya yafutayo**.**

Waheshimiwa naomba mnisikilize vizuri ili kuona zile hoja zetu kama kweli. Kama kweli Bajeti ilikuwa makini na kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, naomba nizitaje kama ifuatavyo:

1) Udhalilishaji wa kijinsia na umuhimu wa kuiengeza bajeti ya fungu hilo.
2) Kutokuwepo Ufanisi katika utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Kitaifa *(Terminal II, na "E.Government").*
3) Utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa serikali.
4) Utaratibu mpya wa usimamizi wa uchimbaji mchanga na bei elekezi ya serikali.
5) Kuchelewa kukamilika miradi ya barabara.
6) Umuhimu wa kutumia mifumo ya kisasa katika kukusanya mapato.
7) Kutoridhishwa na huduma za Hospitali ya Mnazi Mmoja.
8) Nidhamu katika matumizi ya fedha za serikali.
9) Umuhimu wa kukuza ufanisi katika kukusanya mapato.
10) Kukamilishwa mabanda ya skuli ambayo wananchi wameyajenga kwa nguvu zao.
11) Mikakati ya kukabiliana na maafa pamoja na mambo mengine.

Mambo ya Msingi Yaliyobainika

Mhe. Spika, wakati wa mjadala wa bajeti za Kisekta Kamati yangu imebaini kwamba bado kuna changamoto nyingi za kibajeti katika taasisi nyingi za serikali kutokana na mahitaji makubwa waliyonayo, ambapo taasisi nyingi zimeshindwa kufikia malengo waliyojiwekea kutokana na ufinyu wa bajeti, mfano mzuri ni madeni ya vikosi vya Idara Maalum ambayo yanadaiwa na "*Supplier*" wao. Ili kukabiliana na changamoto hii Kamati yangu inaishauri serikali kuongeza vyanzo vya mapto ili kuongeza uwezo wa serikali katika kukusanya mapato.

Mhe. Spika**,** ushauri zaidi kuhusu vyazo vya mapato ambavyo serikali wanaweza kuvitumia ili kutanua wigo wa mapato unatolewa na Kamati yangu wakati wa kuwasilisha Houtuba ya maoni ya Kamati kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali.

Nidhamu Katika Matumizi ya Fedha za Umma

Mhe. Spika, Kamati yangu imegundua kuna mapungufu makubwa sana katika nidhamu ya usimamizi wa fedha katika serikali.

Mhe. Spika, nidhamu ya matumizi ni msingi muhimu katika kuyafikia malengo ya mipango inayojielekeza, iwapo suala la nidhamu ya matumizi halitozingatiwa, jitihada zetu katika kukuza

mapato hazitokuwa na tija yoyote kwani itakuwa ni sawa na kuchumia kwenye mkoba mbovu ama susu bovu tukalitia maji.

Mhe. Spika**,** Kamati yangu inalisema hilo kutoka na namna jambo hili linavyoathiri bajeti ya Serikali. Aidha, hamu ya Wajumbe wengi kutaka kuichangia taarifa ya Ukaguzi maalum wa Ripoti ya Mdhibiti iliyowasilishwa ambapo Mhe. Rais aliagiza kufanywa kuhusu mishahara hewa, inaonesha kwamba kiasi gani Wajumbe wa Baraza hili walikuwa hawaridhishwi sana na kitendo hicho.

Mhe. Spika, kwa kuwa Kanuni za Baraza la Wawakilishi zimeipa jukumu Kamati ya PAC kuifanyia kazi ripoti hiyo, tunaiomba Afisi yako iiwezeshe Kamati PAC kwa kuitengea muda wa kutosha ili iweze kufanikisha kazi ya ripoti hiyo na hatimae iwasilishe ripoti yake hapa Barazani kwa muda muafaka, ili Wajumbe wapate kuichangia ripoti hiyo. Kamati yangu imelazimika kulitilia mkazo suala hili, kwa kuwa ni ukweli kwamba, Kamati ya PAC inajukumu kubwa la kuifanyia kazi ripoti ya Mdhibiti ya kila mwaka kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali pamoja na Mashirika, bila ya kutengewa muda wa kutosha Kamati hii haitoweza kufanya kazi zake na kuwasilisha ripoti hii kikamilifu.

Utekelezaji wa Ahadi za Mhe. Rais

Mhe. Spika, Wajumbe wengi walilalamikia suala la utekelezaji wa Ahadi za viongozi wakuu (Mhe. Rais, pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais). Kamati yangu iliitaka serikali kuzingatia na kuzipa umuhimu ahadi hizo wakati wa upangaji wa Bajeti kwa kuwa nyingi kati ya ahadi hizo zina muda mrefu, hali ambayo hazileti taswira nzuri pia hali hiyo inaweza kupelekea wananchi kukosa imani na viongozi wao wakuu.

Ufanisi Mdogo Katika Kukusanya Mapato

Mhe. Spika, Kamati yangu imeona Mapato ni sehemu muhimu sana katika bajeti, hata hivyo pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali katika kuongeza mapato, imebainika kwamba bado kuna taasisi nyingi za Serikali hazifikii malengo katika kukusanya mapato, hali ambayo haileti taswira nzuri kwa taasisi hizo.

Ushauri wa Jumla

Kamati yangu inaishukuru Baraza la Wawakilishi kwa kuanzisha utaratibu huu wa serikali kufanya majumuisho ya mjadala wa bajeti ambao kimsingi unalipatia Baraza fursa pana ya kushauriana na serikali kuhusu mwelekeo wa Bajeti na mgawanyo wa fedha. Kutokana na upya wa Kamati hii, Kamati yangu wakati wa kutekeleza jukumu hili gumu ilipata changamoto ya kutoeleweka na baadhi ya Wajumbe pamoja na baadhi ya watendaji ambao walikuwa na hofu kwamba Kamati hii ina lengo la kuizuia bajeti ya serikali.

Mhe. Spika, Kamati yangu imefanya kazi kubwa ya kujaribu kuwaelewesha Wajumbe kuhusu jukumu la Kamati hii. Hata hivyo, tunaiomba Afisi ya Baraza ichukue juhudi za makusudi kuandaa utaratibu maalum wa mafunzo kwa wajumbe wote wa Baraza kuhusu Kamati ya Bajeti, aidha mafunzo kama hayo yatolewe kila mara wakati inapoanzishwa Kamati mpya baaala ya

kuwasomesha Wajumbe wa Kamati husika tu kuhusu majukumu ya Kamati yao, kwa kuwa msingi wa utekelezaji wa Kamati hizo unategemea kwa kiasi kikubwa mashirikiano na Wajumbe wote.

UFAFANUZI WA HOJA ZINAZOTOKANA NA MAJADILIANO YA MAJUMUISHO BAINA YA SERIKALI NA KAMATI YA BAJETI

Mhe. Spika, **k**wa msingi huo Kamati yangu ilipata jumla ya hoja 34 kutoka katika mafungu tofauti zikiwemo

1) Hoja zinazohusu ukusanyaji wa mapato,
2) Hoja za kuongeza mafungu ya bajeti,
3) Hoja za kupunguza baadhi ya mafungu ambayo yana fedha nyingi,
4) Hoja za kutoridhishwa na utekelezaji wa baadhi ya programu pamoja na
5) Hoja za jumla kuhusu utekelezaji wa bajeti ambazo zimechangiwa na wajumbe wengi.

Mhe. Spika, ili kutoa urahisi wa ufafanuzi wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati, Kamati yangu inaomba iwasilishe hoja hizo kwa njia ya Bango Kitita/Jadweli ambazo imezigawa katika sehemu tatu; sehemu ya kwanza inahusu Hoja za Kisekta, Sehemu ya Pili inahusu, majibu ya Serikali na sehemu ya Tatu ni Ushauri wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Spika, naomba niende kwenye hoja kama ifuatavyo:

Hoja Nam. 1

AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS: FUNGU C01-C05

Idara ya Watu Wenye Ulemavu kupitia programu ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu.

Kamati imearifiwa bajeti yake ni ndogo sana kwa mujibu wa mahitaji ya Idara hiyo, na uhalisia wa shughuli zake za kila siku ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imetengewa T.sh 498,832,240. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza la watu wenye ulemavu halikupata kukaa hata kikao kimoja kati ya vikao vinne (4) vilivyokusudiwa.

Majibu ya Wizara

Kamati iliarifiwa sababu ya kutofanyika kwa vikao hivyo ni kutopatikana kwa fedha kama ilivyotarajiwa. Pia vikao hivyo havikupewa kipaumbele kulinganisha na upatikanaji wa fedha hizo. Ambapo fedha zilizopatikana zilitumika kwa mafunzo, uhamasishaji na ununuzi wa vifaa visaidizi, na uendeshaji wa ofisi.

Iwapo vikao hivyo vitakuwa na kipaumbele Mkurugenzi anatakiwa awasilishe kwa Katibu Mkuu.

Maoni ya Kamati

Maoni ya kamati ni kuwa fedha zilizopangiwa ziingizwe kwa wakati ili Idara iweze kutekeleza majukuu yake ipasavyo ili fedha hizo ambazo zilipangiwa zinatakiwa zifikishwe katika sehemu hiyo kwa wakati iweze kutekeleza majukumu yake.

Miongoni mwa sababu zilizopelekea kufanyika kwa vikao hivyo ni pamoja na ufinyu na ucheleweshaji wa bajeti kati ya waliopata walikuwa wametenga milioni 462,121,000 Idara ilipata milioni 103,261,000 tu kwa asilimia 62.

Mhe. Spika, utaona jinsi gani hakuna ufanisi wowote kwenye idara hii asilimia 22 ni ndogo mno kwa hivyo tunomba serikali ielekeze bajeti ambayo inapitishwa na Baraza la Wawakilishi kufika kwa wakati ili basi makusudio mazima yaweze kutekelezeka.

Hoja Nam 2

Hoja ya pili ilikuwa ni Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya ambayo imepangiwa milioni 598,900,000/- lakini Tume ya UKIMWI imepangiwa milioni 846,800,000/-. Kutokana na umuhimu wa Mapambano dhidi ya Madawa ya kulevya. Imependekezwa kwamba, bajeti iliyopangiwa Tume ya Ukimwi ipangiwe Idara inayohusiana na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, na bajeti ya madawa ya kulevya ipangiwe Tume ya Ukimwi.

Kamati imearifiwa kwamba Tume ya Ukimwi ina mahitaji zaidi ya bajeti kutokana na kuwa na wafanyakazi wengi ukilinganisha na wafanyakazi wa Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya kwa maana hiyo mishahara mingi inakwenda pale. Lakini pia utafiti uliofanywa mara ya mwisho unaonesha bado kuna ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa jamii ya Kizanzibari. Aidha, kwa sasa Tume ya UKIMWI inakosa wadhamini wa miradi ya maendeleo ambao kabla walikua na msaada mkubwa katika maswala ya kibajeti. Lakini pia Tume ya Dawa zakulevya imeridhia kiwango kilichopangiwa.

Maoni ya Kamati

Maoni ya kamati ambayo baada kupitia hoja zote mbili hakuna pesa hapa zilizoongezwa kwa sababu fungu hili tumeliacha kama lilivyo kutokana na umuhimu wake.

Hoja ya Nam. 3

Hoja ya nne imependekezwa Bajeti ya Idara ya Sherehe na Maadhimisho pamoja na Kuwaenzi Viongozi ambapo ni Tsh 1,081,975,600 ipunguzwe, ili fedha hizo zitumike katika kukabiliana na maafa na hasara iliyotokezea kutokana na mvua na upepo pamoja na kusaidia kutengeneza miundo mbinu ya barabara zilizoharibika.

Jibu la Serikali

Kamati iliarifiwa kuwa kiuzoefu, bajeti iliyopangwa Idara hii, huwa haitoshelezi kwa uadhimishaji wa sherehe za kitaifa ikiwa ni pamoja na Sherehe za Mapinduzi, hivyo iwapo fedha zitapunguzwa, sherehe hizo hazitaweza kufanyika kama ilivyo ilivyokusudiwa.

Kamati imeridhika baada ya kuona vipengele mbali mbali na Mhe. Mohamed Aboud Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kueleza nia kubwa kwa hivyo, kamati yangu imeridhika na hoja ambayo ameitoa.

AFISI YA RAIS IKULU: FUNGU A01-A02

Idara ya GSO ina mazingira magumu ya kiutendaji kazi kutokana na ufinyu wa Bajeti inayopangiwa ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepangiwa TZS 75,000,000. Tatizo hili pia linatokana na Muundo wa Idara unaotokana na Sheria inayosimamia Idara hiyo. Aidha, utekelezaji wa Malengo kwa idara hiyo ni mdogo sana.

Jibu la Kamati

Wizara imekiri ni kweli idara hiyo ina matatizo yanayochangiwa pia na sheria inayosimia idara hiyo. Lakini yapo matatizo yaliyopatiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na suala la usafiri wa gari kwa Idara hiyo. Aidha, Kamati imehakikishiwa na Wizara kuwa bajeti iliyotengwa mwaka huu wa fedha inatosheleza mahitaji ya idara hiyo. Wizara hiyo imeanza kuchukua juhudi la hatua lakini cha kusitisha zaidi kuwa hata mtendaji wake Mhe. Waziri alipokuja mbele ya kamati hakuja naye, tungeomba tuu mara ya pili Mheshimiwa uje na mtendaji huyu ili ahakikishe yeye mweyewe.

Hoja nyengine kuhusu ahadi za za Mhe. Rais ambazo hazijatekelezwa licha ya kuwa ahadi hizo ni za muda mrefu. Wizara imeahidi kuendelea kuhimiza sekta husika ambazo zinahusika katika utekelezaji wa ahadi hizo ili zitekelezwe kwa wakati. Kamati ya kisekta imeagizwa kamati yangu Mhe. Spika, kwa niaba yako imeiagiza Kamati ya Kisekta kufuatilia hali hizo karibu pamoja na wizara hiyo ili jambo hilo kulipatia ufumbuzi zaidi.

Hoja ya nyengine kuhusu suala la mishahara hewa, suala hili msingi wake ni ripoti ya Ukaguzi maalum alioufanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokana na agizo la Mhe. Rais, Wajumbe walilizungumzia kwa hisia namna linavyoathiri bajeti ya Serikali na kuitaka Serikali kuwachukulia hatua waliobainika kuhusiana na kadhia hiyo.

Kamati imeelezwa kuwa suala hili bado linafuatiliwa, aidha kuna Kamati maalum iliyoundwa na Mhe. Rais, kufuatilia suala hilo na baada ya kukamilika taratibu, wanaohusika watachukuliwa hatua.

Mhe. Spika, tunaiomba sana Serikali kulifatilia kwa makini zaidi ili basi tuone basi haja ya pesa za wananchi zisitumike vibaya na hapa tunapotisha tuweze kupitisha kwa mafungu mazuri lakini kwa utumiaji halisi unaopatikana.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: FUNGU G01-G09

Mhe. Spika, hoja nyengine Wajumbe wameishauri serikali, kuhusu umuhimu wa Taasisi za serikali kutumia majengo yao wenyewe baada ya kukodi pamoja na kuyafanyia matengenezo (ukarabati) ili kulinda hadhi ya taasisi za serikali, lakini pia kuepuka upotevu wa fedha nyingi za serikali kwa kukodi majengo, mfano wa taasisi hizo za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Pemba ambao wanatumia jengo la serikali.

Mhe. Spika, kamati imeelezewa kuwa, kuhusu jengo la Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Wizara tayari wameshahamia katika jengo lake jipya. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa kuhamia jengo lake jipya.

Hoja ya pili baadhi ya Wajumbe walijenga hofu ya kutoridhika juu ya ufanisi wa Mradi wa *E-government*, ambao mwaka huu unatarajiwa kutekelezwa katika *phase* ya pili na ambao kiujumla unagharimu Serikali fedha nyingi kwa mfano kwa mwaka wa fedha za Kitanzania.

Mhe. Spika, wizara imeeleza baada ya ukamilifu wa awamu ya kwanza ya kuweka miundo mbinu, awamu ya pili ya mradi imekusudia kutekelezwa katika maeneo ya *"e-tax" na "e-health*", ambayo ni mapya kwa mujibu wa *"scope*" tuliyoiona.

Mhe. Spika, naomba nikiri kamati yako ilifatilia na kielelezo nitakukabidhi kama ipo haya ya kuwapa wajumbe na ninaomba wajumbe hili tusiwe na wasiwasi nalo, kwa sababu tulililfatia kwa ukaribu zaidi.

Mhe. Spika, kwa sababu Idara hii ilipangiwa bilioni 10,000,000,000 ambazo ndizo za Serikali lakini bilioni 46,000,000,000 ilikua ndiyo fedha za wahisani kwa ujumla wake ilikuwa inatisha kuona fungu hili bado Serikali inakuja kwenye Baraza hili inaweza kuomba bilioni 56,000,000,000 kwa sababu wa utekeleza huo.

Lakini niombe baada ya kujiridhisha kamati yenu ya bajeti kwa niaba yenu nasema twende mbele tuone mwakani *e-government* inavyotekelezwa.

AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ: FUNGU D01-D09

Baadhi ya Wajumbe walichangia kuhusu Kiwanda cha Ushoni cha Kikosi cha Valantia, ambapo walikitaka kiwezeshwe ili kiweze kuzalisha viatu kwa kiwango kikubwa na kizuri. Aidha Wajumbe walipendekeza kikosi hicho kiongezewe Bajeti kwa kuwa bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017, kwa kipindi cha miezi tisa kati ya Tsh 827,200,000 walipata Tsh 27,430,000 sawa na asilimia 3.3

Mhe. Spika, utaona jinsi gani hapa Bajeti ya Serikali isivyotekelezeka na inatisha zaidi. Bejeti iliyopangwa kwa kazi za Maendeleo. Hivyo, Wajumbe wamesisitiza kwa mwaka wa fedha 2017/2018 bajeti iliyopangwa ya Tsh 4,000,000,000 ipatiwe kama ilivyojipangia.

Mhe. Spika, makusanyo ya Chuo cha Mafunzo kwa mwaka 2016/2017 hayaridhishi hususani Viwanda vya mafunzo ambapo hadi machi 2017 jumla ya Makusanyo yalikuwa TSh 2,419,000 sawa na asilimia 22 ya makadirio ya Tsh 11,000,000

Mhe. Spika, inasikitisha sana lakini baada ya kukaa na kushauriana na Wizara pamoja na Idara Maalum walitupa stakabadhi maalum inayoonesha lakini pia tulishauri juu ya jambo zima na imekubali kufanya hivyo kwa hivyo waheshimiwa wajumbe jambo hilo tumelifuatilia kwa karibu zaidi.

Ongezeko la ufanisi katika suala zima la mapato, Wajumbe wamependekeza Ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri itumie Mashine pamoja na njia za Kibenki. Lakini Wizara imekuja imesema Wizara imeeleza kuwa imejipanga kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki, katika ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kama ni moja wapo ya mikakati yao iliyojipangia.

Ushauri wa Kamati

Kamati yangu inashauri Kamati ya Kisekta kulifuatilia suala hili na kuhakikisha linatekelezwa ndani ya mwaka wa fedha wa 2017/2018. Watakapokuja tena hapa waweze kutwambia lugha nyengine.

Mhe. Spika, kuhusu ununuzi wa gari mbili za *"Fire Airport"* Ununuzi huu takriban ulikuwa umekusudiwa dola 3,400,000. Wajumbe wengi wameonesha kutoridhishwa na gharama za ununuzi wa gari hizo, kwa kuwa gharama zilizotumika ni kubwa sana**.** Aidha, Wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum hawakupatiwa nyaraka za ununuzi wa gari hiyo, Wizara imeelekeza kuwa *specification* za gari hizo zipo na kama ingeweza kuhitajika wangepewa.

Kwa kuwa nilifatilia na mlinipa jukumu hilo nimefatilia Mhe. Spika, ikiwa ipo haja ya kutoa *specification* hiyo zipo lakini na vile vile bei hali ambayo iliyonunuliwa tumekubaliana nayo na Wizara.

Mhe. Spika, kwa fedha za OC walizingiziwa wajumbe wa Halmashauri na madeni hayo yanofanyiwa.

WIZARA YA HABARI UTALII UTAMADUNI NA MICHEZO: FUNGU JO1-J02

Mhe. Spika, Wajumbe wameitaka Serikali kufanyika jitihada zaidi ili kuhakikisha mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii yanaongezeka. Aidha mfumo unaotumika sasa hivi wa kukusanya takwimu za watalii Bandarini na katika viwanja vya ndege, ambao hutegemea taarifa za takwimu kutoka Idara ya Uhamiaji zibadilishwe.

Wizara imeeleza takwimu za Watalii zinapatikana kutoka kitengo cha takwimu cha Idara ya Uhamiaji, ambapo takwimu hizo zipo za aina mbili,(watalii wanaotoka moja kwa moja kutoka Tanzania bara na wanaotoka moja kwa moja kutoka nje ya nchi). Kwa sasa takwimu zote hizo zinakusanywa. Aidha, Idara inajiandaa kuanza kutumia mfumo wa *"Digitali".*

Hivi karibuni Wizara imekaa na kampuni ya *"Azam Marine"* kwa lengo la kujadiliana juu ya namna ya kuboresha ukusanyaji na takwimu hizo.

Mhe. Spika, Lengo la Wizara imesema Wizara inaelekeza takwimu za watalii kupatikana kutoka Kitengo cha Idara ya Uhamiaji lakini Kamati. Kamati imeshauri utaratibu utumike aina moja wa kukusanya kwa takwimu hizo kwa *Airport* na Bandarini, lakini pia ukusanyaji wa takwimu hizo ujumuishe hata watalii wa ndani wanaokuja Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Aidha, ukusanyaji wa takwimu hizo unajiandaa kuanza kutumia uandaliwe katika mazingira ambayo hayatawasumbua watalii, na pia itashauriwa kuwa kuandaliwe fomu za kujaza wageni za kutambua wanakotoka, kabla ya kushuka katika chombo cha usafiri ndege au chombo cha usafiri cha baharini.

Hoja ya pili ilikuwa kutokana na umuhimu wa Sekta ya Utalii, Wajumbe pia wameshauri bajeti ya kuutangaza utalii iongezwe ili utalii wa Zanzibar uweze kutangazwa zaidi na kuongeza Idadi ya Watalii wanaokuja Zanzibar. Ambapo bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni bilioni 425,293,000 tu.

Mhe. Spika, Wizara inaeleza kuwa, tatizo si kutangaza utalii pekee, lakini pia kuwafanya watalii kubaki Zanzibar na kushawishika kurudi tena. Aidha kuna jumla ya Tsh. Bilioni moja zilizotengwa kwa ajili ya uboreshaji wa maeneo ya kihistoria.

Pia Kamati imearifiwa kuwa, fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, zinatosha kulingana na malengo yenyewe.

Kamati inashauri kuwa, isitosheke na dhana kuwa Zanzibar ni *"Brand"* inayojiuza yenyewe na inahitajika kuweza kufanya *publicity* ya uhakika soko la utalii, kwani hata nchi zilizopiga hatua kubwa kwenye utalii, ambazo zinaendelea kutangaza nchi zao kwa gharama kubwa, ili kuenda sambamba na ushindani wa kimataifa. Tungeiomba Serikali lazima ishindane kwenye masoko haya na kwa sababu hiyo iweze kutangazwa pesa ambazo tuliziona sisi kama kamati basi hazikuweza kuweza kuutangaza utalii kwa kina zaidi.

Hoja ya tatu wajumbe wengi hawakuridhishwa na ukusanyaji wa mapato wa Wizara ya Habari katika Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utalii na Maeneo ya kihistoria ambapo kwa mujibu wa ripoti ya Kamati, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya milioni 170,110,202 zilikusanywa kwa asilimia 43 tu ya lengo la makusanyo ya milioni 392,268,000.

Mhe. Spika, hii utaaona jinsi gani ilivyopungua hapa lakini Wizara imeanza kusema Wizara imeeleza kuwa, kuharibika kwa jengo la *Beit el Ajaib*, pamoja na uharibifu uliojitokeza katika jengo la "*People's Palace"* ni miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua idadi ya watalii wanaotembelea humo.

Mhe. Spika, Kamati imeshauri jitihada zaidi ziongezwe katika kusimamia na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria pamoja na kubuni vianzio vipya vya mapato vilivyomo katika taasisi zinazohusika na programu hiyo

WIZARA YA UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO: FUNGU Q01

Mhe. Spika, nimelazimika sana nitizame mbele ili wajumbe wako sasa waisikilize vizuri kwa sababu hoja hii ilikuwa na mashiko ya kipekee.

Mhe. Spika, wajumbe wengi waliochangia Wizara hii kwa kugusa kifungu cha Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Watoto ambacho kilitengewa Tsh 55,100,000 milioni tu. Wajumbe walitaka kifungu hichi kiongezewe fedha ili kiende sambamba na hali halisi ya tatizo la udhalilishaji katika nchi yetu ikiwa ni njia moja wapo ya kusaidia harakati za kupambana na vitendo hivyo.

Mhe. Spika, wizara inajibu, Wizara imeeleza kuwa Wizara imefanikiwa kukaa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Habari, na kuifanyia kazi hoja hiyo na kukubaliana na mabadiliko yafuatayo:

Kifungu SQ 010202 programu ndogo ya Mapambano dhidi ya udhalilishaji wa Wanawake na watoto chenye shilingi 55,100,000/ kiongezwe fedha hadi kufikia shilingi 175,100,000 ambapo ni sawa na ongezeko la shilingi 120,000,000 ambapo ni sawa na asilimia 69% ya makadirio.

Aidha, mapendekezo hayo ya fedha yalifikiwa katika vifungu vifuatavyo:

a. Fungu SQ010201 Programu ndogo ya Kuratibu wa Masuala ya Kijinsia na Uendelezaji Wanawake shilingi 80,000,000/=

b. Fungu SQ010301 Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi ya Jamii shilingi 42,000,000/=

Waheshimiwa wajumbe kamati imeliona hili na kufurahishwa na faraja kubwa ya Mhe. Waziri kwa kukubali na kuziona hoja za wajumbe ambao imeonekana inafaa. Mhe. Waziri nichukuwe fursa hii kukupongeza sana kwa umakini wako na ushirikiano mkubwa sana wa kamati juu ya mambo hayo.

Mhe. Spika, niombe kwa aina ya kipekee hivi ndivyo tunavyotaka kukaa kama Kamati ya Bajeti na kamati nyengine yoyote hakuna uadui kati yetu na Serikali kuna utendaji kazi.

Mhe. Spika, hoja ya pili kwa wizara hiyo wajumbe wengi walichangia kuhusu utaratibu wa pencheni za Wazee waliofikia miaka 70 kwamba hauko vizuri, ambapo baadhi yao hawajafikia miaka 70 wanalipwa kwa sababu walijiandikisha na baadhi yao wamefikia miaka 70 lakini hawalipwi kwasababu hawajajiandikisha. Aidha, utaratibu wa kuwafuta wazee waliofariki na kuwaingiza wazee wapya hauko wazi. Kutokana na hali hiyo, Wajumbe wamejenga hofu ya kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya zoezi hilo hazitumiki ipasavyo.

Wizara imekiri kuwepo kwa tatizo hilo, na imeiarifu kamati kwamba wamepanga mikakati kufuatilia, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfumo *“database”* ili kugundua wanaofanya udanganyifu.

Aidha wizara ilimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi juu ya suala hili na ripoti yake tayari itawasilishwa kwa Mhe. Rais.

Vile vile wizara inakusudia kuomba msaada kwa ajili ya zoezi hili kupitia shirika la kazi "ILO" katika kupata mfumo ambao utawasaidia kutatua changamoto hizo.

Kamati imeomba watendaji waliohusika kufanya udanganyifu wachukuliwe hatua. Aidha Kamati imeiomba Kamati ya kisekata, ilifuatilie zaidi suala hili, kwa kushirikiana na Wizara husika kwa kufanya uhakiki kwa kila wilaya.

Mhe. Spika, hoja ya tatu katika wizara hiyo wajumbe wengi walichangia kuhusu Bajeti ya Mabaraza ya Vijana kuwa ni ndogo sana ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mabaraza ya Vijana yote ambayo takriban yapo 52 ngazi ya Shehia, 11 ngazi ya Wilaya na 1 ngazi ya Taifa yametengewa Tsh 100,000,000 tu ambazo kimsingi haziyawezeshi Mabaraza hayo kutekeleza shughuli zake ipasavyo.

Mhe. Spika, wizara ilieleza kuwa, fedha hizo hazikutengwa kwa ngazi za wilaya, na shehia, isipokuwa zilitengwa kwa ngazi ya kitaifa, kwa ajili ya shughuli za uratibu kupitia Katibu Mtendaji kwa ajili ya shughuli za uratibu ngazi ya Taifa na kusukuma maendeleo ya mabaraza ya vijana.

Aidha, Wizara imeeleza kuwa, zipo program nyengine za Wizara, ambazo zinasaidia masuala ya vijana kwa ujumla.

Kwa kuwa utaratibu wa Baraza la Vijana bado ni mpya, Wizara inaeomba waachiwe fedha hizi kama alivyopanga ili kuangalia basi ufanisi wake zaidi.

Mhe. Spika, kwa hili kamati haikuona umuhimu wa kuchukua fungu hili na imeliacha kama lilivyo.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KIFUNGU KO1

Mhe. Spika, kwa kuwa suala la elimu ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali na kwa kuwa kuna mahitaji mengi ya wanafunzi wanaohitaji mikopo ya elimu ya juu, ambapo wengi wao wanakosa mikopo hivyo, Wajumbe wamependekeza fungu la Mikopo ya Elimu ya juu liongezwe ili kuweza kuongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na huduma hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Idara hiyo imepangiwa Tsh 10,203,700,000.

Wizara imeelekeza kuwa, kwa mwaka huu wa fedha, kasma hiyo imeongezeka, kulingana na bajeti ya mwaka jana 2016/2017. Aidha Wizara imeeleza kuwa, fedha hizo kwa mwaka huu wa fedha hazitawanufaisha wafanya kazi wa Serikali.

Sambamba na ongezeko hilo, kwa mwaka huu wa fedha, mbali mbali zitagharimia za masomo (ada), Wizara pia itawapatia wanafunzi fedha za kujikimu (posho) ambapo jumla ya wanafunzi 1600 wapya watanufaika na mkopo huo.

Naomba Mhe. Spika, nifafanue kidogo hapa wizara hii ilikuwa haiwalipi wanafunzi wa Zanzibar *living expenses* sasa kwa kuona upo umuhimu na kukaa na kamati kushauriana imeona sasa ipo haja ya kuweza kuwalipa na wao wanafunzi wa Zanzibar, tunaishukuru sana na tumpongeze sana Mhe. Waziri kwa suala hili la wanafunzi.

Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, kuhakikisha kuwa, fedha zinaingizwa kwa wakati ili wanafunzi wasipate usumbufu hasa wale wenzetu wanaoishi nje ya nchi hii au nje ya Zanzibar kwa sababu usumbufu ni mwingi sana unaojitokeza hasa kwa watoto wa kike.

Hoja ya pili wajumbe wengi walizungumzia suala la kumalizia majengo ya Skuli ambayo wananchi wamejitolea kuyajenga.

Wizara imekiri kuwepo kwa tatizo hilo, na kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tayari fedha zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha jumla ya madarasa 285.

Aidha kuna wafadhili mbali mbali wameahidi kusaidia suala hili ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya *"Milele Foundation"*

Mhe. Spika, ushauri wa Kamati, Kamati imeridhika na majibu ya Wizara, pia lakini imeelekeza Kamati ya kisekta kufuatilia kwa karibu zaidi kuona madarasa hayo yamejengwa kwa wakati.

Mhe. Spika, hoja ya tatu wajumbe wamependekeza kuwa fedha zilizochangishwa kwa ajili ya ununuzi wa madawati isiwekwe benki, bali ianze kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, ili kuepuka kuongezeka kwa gharama za utengenezaji.

Wizara imeelekeza kuwa, kutokana na kuwepo kwa changamoto ya uchache wa madarasa, imeona ni vyema kuanza kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo kabla ya ununuzi wa madawati, ambayo yakinunuliwa kabla ya kuwepo kwa madarasa ya kutosha itapelekea changamoto nyengine kwa kukosa sehemu ya kuyaweka.

Kamati imeridhika na maelezo haya ya Serikali na kuwaachia fungu hilo liendelee kama lilivyopita.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA MALIASILI: FUNGU L01

Kuhusu Soko la Kinyasini amabalo lilitengewa bilioni 2,500,000,000 na lilitarajiwa liwe tayari kwa miezi 6. Aidha, soko hilo lilitakiwa liwe la ghorofa mbili , liwe la kisasa, na liwe na *lift* tofauti na ilivyo kwa sasa ambapo linaonekana kuwa ni la kawaida

Mhe. Spika, maelezo ya Wizara, Wizara imeelekeza kuwa, kwa mujibu wa makubaliano ya wafadhili na Halmashauri husika, jengo hilo liliafikiwa kuwa liwe la kawaida (la chini) lakini msingi *(foundation)* yake uwe na uwezo wa kujengewa ghorofa tatu.

Aidha kwa sababu halina ghorofa kutokana na makubaliano hayo, fedha za *"lift"* zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa uzio pamoja na kuongezea idadi ya vyoo.

Aidha jengo limechelewa kumalizika kutokana na kuwepo chagamoto ya upatikanaji wa vifaa.

Mhe. Spika, Kamati kwa kuwa fedha zilizotumika kwa mradi huo ni nyingi, Kamati imeishauri Kamati ya kisekta kufuatilia kwa karibu ujenzi huo kwa karibu zaidi.

Mhe. Spika, hoja ya pili ni wajumbe wengi wamechangia kuhusu suala la mchanga kutokana na uamuzi wa Serikali kuyachukua Mashamba ya Mchanga yaliyokuwa yanamilikiwa na watu binafsi bila ya kulipwa fidia. Aidha, Wajumbe wamesikitishwa na bei kubwa wanayouziwa wananchi kinyume na bei elekezi iliyotolewa na Serikali.

Wizara imeelekeza kuwa, ipo tayari kulipa fidia, iwapo mdai atakuja na nyaraka halali zitakazo halalisha madai yake.

Aidha, kimsingi Serikali haijaelekeza bei ya mchanga, lakini ongezeko hilo linasababishwa na wafanyabishara kutokana na kutokukubaliana na utaratibu uliowekwa na Serikali.

Kamati imeshauri Serikali iondoe zamu za kwenda kuchukua mchanga mashimoni ikiwa ni moja ya sababu zinopelekea wafanya biashara kupandisha bei ya mchanga.

Aidha, Serikali imeshauriwa na kamati kutoa elimu kwa wananchi, kuhusiana na rasilimali hiyo na umuhimu wa kudhibiti matumizi yake.

WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO: FUNGU R01

Mhe. Spika, imependekezwa kuwa, wajumbe walichangia kwa hisia sana kupendekeza kuwa kianzio cha Mapato cha Mali Maiti ambacho kwa sasa kipo chini ya Wizara ya Biashara Kihamishiwe Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambayo ipo chini ya Wizara ya Katiba, Sheria , utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Wizara imeeleza kuwa, tayari imeanza kulichukulia hatua suala hilo, kwa kuwaandikia Wizara ya Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuhusu kukirejesha kitengo hicho.

Kamati imeshauri kwa kuwa chanzo hicho hakihusiani moja kwa kwa moja na Dini ya Kiisalm, Kamati imeshauri kuwa, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba, na Katibu Mkuu Wizara ya Biashara, wakae pamoja na kushauriana juu ya kitengo hicho ili kupata hatua muafaka ya kuweza kukiweka.

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI: FUNGU P01

Mhe. Spika, wajumbe wengi, hawakuridhishwa na Maendeleo ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege *Termina II* wa *Karume International Airport* ambao umechukua zaidi ya miaka mitano. Aidha, Wajumbe wengi wakati wakichangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, wameonesha kutoridhishwa na mradi huo, ambao umekuwa wa muda mrefu umegharimu Serikali fedha nyingi. Pia Wajumbe wameitaka Serikali kuwachukulia hatua waliohusikana na uzembe katika kadhia hiyo.

Majibu ya Serikali

Kimsingi, Serikali imeeleza kuwa kwa sasa mkwamo wa mradi huo umeshapata utatuzi, ambapo wafadhili *(Exim Bank)* amekubali kuingiza fedha ili kuendeleza mradi huo, ambapo mradi huo unatarajiwa kuendelea ndani ya mwaka huu wa fedha.

Kamati imeshauri katika ujenzi wa *Terminal* hiyo kuzingatiwe kujengwa kwa mfumo wa kutiririsha maji, ili kuepuka kutuama kwa maji katika eneo hilo.

Aidha, kwa mradi huo kuwa siku nyingi na kuigharimu Serikali fedha nyingi. Kamati ya Kibajeti imekukusudia kufata moja kwa moja yenyewe. Haikuagiza Kamati ya Kisekta hapa kwa sababu Kamati ya Kisekta imeshafanya nao kazi kwa kipindi kirefu sana.

Suala la Pili Fungu la Idara ya Utunzaji wa Barabara UUB liongezwe ili Idara hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi, kwa kuzitengeneza barabara zilizoharibiwa na mvua ya masika. Aidha kutokana na ubovu wa barabara nyingi, Wajumbe wengi wameonesha hofu juu ya Wakandarasi wanaopewa tenda za ujenzi wa barabara ambazo mara nyingi huwa zinakosa viwango. Hivyo, wajumbe wameitaka serikali kuangalia uwezekano wa kuitumia Idara ya UUB ili iweze kutengeneza barabara hiyo badala ya kutegenezaa wakandarasi wa nje ambao hawana viwango.

Majibu ya Serikali

Mhe. Spika, wizara imeeleza ina mpango wa kuanzisha viwango "*standard*" yake maalum ya ujenzi wa barabara ambavyo vitafuatwa na wakandarasi wote wa barabara wakati wa ujenzi wa barabara. Aidha, serikali ina mpango wa kuwa na mamlaka ya barabara ambayo itafanya kazi sawa na zinazofanywa na "*TanRod*" kwa Tanzania Bara. Vie vile wizara imeelekeza kuwa fedha hiyo ni zaidi ya bajeti iliyopangwa kwa mwaka 2016/2017 kwa ujumla fedha hizo. Mhe. Spika, hapa inaonesha wizara imepata ufumbuzi mkubwa sana na kuanza kuanzisha taasisi yenyewe, lakini wameleta ufafanuzi mzuri sana wa kuwa fedha ambazo zilitengwa hapa zinatosheleza, na hivyo kamati yangu imeshauri Mwenyekiti wa Kamati kisekta kuwafatilia kwa ukaribu zaidi na alete jibu katika *rotation* ya mwanzo ya kamati hizi.

Mhe. Spika, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano imependekeza bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iongezwe ili waweze kukabiliana na changamoto nyingi zinazowakabili zikiwemo zile za ubovu na uchakavu wa majengo ya nyumba za taasisi zake, uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa usafiri kwa ajili ya idara mbali mbali.

Wizara imeeleza kwamba kimsingi hawana chanagamoto ya vitendea kazi, badala yake walikuwa na tatizo la "*maintenance*". Hata hivyo, kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa mwaka huu inataraji changamoto hizo zitaondoka. Kamati imeridhika na majibu haya ya wizara na haikuweza kuchukua hatua yoyote imeachia fungu kama lilivyo.

WIZARA YA AFYA

Mhe. Spika, katika fungu la huduma za ufuatiliaji wa maradhi yasiyoambukizwa yaliyopo yaliliopo Wizara ya Afya kwenye kitabu kikubwa cha bajeti imetengewa milioni 30,000,000

makisio yake, lakini kwenye fedha ya maendeleo hakuna kitu zero na kwenye kitabu kidogo kinaonesha zimetengwa milioni 96,000,000, lakini na maendeleo ni 2,865,967,000. Mhe. Spika, wizara imeeleza kwamba usahihi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo.

Inaonesha kuwa kwenye kitabu kikubwa "*estimate book*" yake haikufuatana na buku lakini imeeleza wazi kamati kuwa iko sawa na kamati imeridhika kwa hivyo changamoto hiyo imeondoka. Lakini ulielekeza Mhe. Spika, ulipokuwa umekaa kama Mwenyekiti kufuatilia huduma sahihi za Mnazi Mmoja, kamati imekaa na wizara na kupatia ufumbuzi mkubwa sana. Na tunamshukuru Mhe. Waziri wa Afya kwa kutupa mashirikiano makubwa na hatimae basi Wizara ya Afya tukamaliza kwa jambo zuri zaidi.

WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI MAJI NA NISHATI

Mhe. Spika, hoja iliyojitokeza kuiokoa *ZECO* na kubeba mzigo mkubwa wa madeni imependekezwa Wizara ya Fedha kulipa moja kwa moja *ZECO* huduma ya umeme kwa zile taasisi ambazo hazijaungiwa mita za TUKUZA ili kupata nguvu Shirika kuweza kutoa huduma bora kwa wakati na pia kuweza kulipa madeni ya *TANESCO*

Mhe. Spika, wizara katika kukabiliana na chanagamoto hiyo ya *ZECO* imeanzisha utaratibu maalum wa kuzifungia mita za TUKUZA Taasisi za Serikali. Aidha, wizara imeeleza kuwa**, s**erikali ina mkakati maalum wa kuhakikisha inamaliza madeni ya taasisi zake yanayodaiwa na *ZECO*, pamoja na deni la zamani inalodaiwa na TANESCO ambalo kwa sasa serikali kupitia *ZECO* inalipia jumla ya Tsh 4.5 bilioni kila mwezi ili kuhakikisha hailimbikizi deni jipya kwa *TANESCO*.

Mhe. Spika, kamati imeridhika na maelezo yaliyotolewa na wizara kuhusu mikakati ya serikali kumaliza deni lake la moja kwa moja ambalo la mrefu kwa *TANESCO*, na madeni ya taasisi zake kwa *ZECO*. Kuhusiana na madeni ya viongozi wakuu kamati imeagiza kupatiwa vilelezo kutoka wizara husika vinayothibitisha kuwa madeni yote wanayodaiwa Viongozi Wakuu wa Serikali yameshalipwa.

Mhe. Spika, hii ilitokana na kuwa viongozi wetu wakuu ambao waliambiwa wanalipiwa pesa nyingi za ziada ambazo wizara imetwambia tayari imeshazilipa.

Hitimisho

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha majumuisho ya mjadala wa makadirio ya bajeti. Aidha, napenda pia kuwashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha majumuisho ya Kamati ya Bajeti.

Mhe. Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi ndugu Raya Issa Msellem pamoja na wasiadizi wake kwa kuiwezesha kamati hii kwa kutekeleza majukumu yake vizuri. Mhe. Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu mkubwa nipende sana kuishukuru familia yangu kwa kunivumilia wakati nikitekeleza majukumu yangu kikatiba nje na ndani ya Zanzibar.

Lakini mwisho kwa umuhimu mkubwa nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika kwa hekima zako, busara zako pamoja na Naibu Spika Mwenyezi Mungu awalinde na hasada zote. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

Waheshimiwa Wajumbe, wengi wenu mmekuwa mnanileta vibarua kwa ajili ya kuomba kuchangia, ambayo ni sahihi kwa sababu hoja zote zimeshawekwa mezani. Lakini wengi walikuwa wanaashiria ndani ya vibarua vyao wangependa kuchangia kuanzia siku ya Alhamis. Kwa hivyo, nimeona bora ninyanyuke nikuambieni kwamba maombi yanaweza yakaendelea kuja lakini tutakuwa tuna siku mbili za mapumziko, yaani kesho na keshokutwa. Kwa hivyo, hapa tutaanza kuchangia tena kuanzia tarehe 15/06/2017 tutakuwa na siku tatu za kuchangia hizi bajeti zilizosomwa. Tarehe 15, tarehe 16 na tarehe 19/06/2017 kwa sababu tarehe 17 na tarehe 18 ni siku ya Jumamosi na Jumapili. Kwa hivyo, maombi mnaweza mkaendelea kuyaleta lakini kuchangia tutaanza kuchangia kuanzia tarehe 15/06/2017 mtakuwa na siku mbili za kujiandaa kwenda kujitayarisha kwa ajili ya kuja kuchangia hizi bajeti. Baada ya maelezo hayo machache Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali
Makadirio ya M apato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako hili tukufu mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha wa 2017/18. Kwa kutekeleza azma hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako sasa likae kama Kamati Maalum ya kupokea na kujadili mapendekezo hayo.

Mhe. Spika, imani inatutaka waumini kuanza kwa jina la Mwenyezi Mungu, Muumba wetu. Naomba nami nianze kwa kumtukuza na kumshukuru sana Mola wetu, Subhanahu Wataala, kwa neema zake alizotujaalia ambazo miongoni mwake ndizo zinazotuwezesha sisi kuwepo hapa mchana huu kutimiza wajibu wetu kwa jamii iliyotupatia ridhaa ya kuiongoza na kusimamia maendeleo yake. Mhe. Spika, kwangu mimi pia, bila ya neema hizo za uhai, afya na utulivu wa kila aina alionijaalia Muumba wetu, nami nisingeweza kutekeleza wajibu huu. Namshukuru na kumdhukuru sana mola wetu.

Mhe. Spika, kifungu cha 105 cha Katiba yetu ya mwaka 1984, kama ilivyorekebishwa, kinamtaka Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Baraza lako hili makadirio ya matumizi ya serikali kwa mwaka unaofuatia. Kwa kuwa mwaka wa fedha mpya wa 2017/18 unakaribia kuanza, nakushukuru Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kutimiza wajibu wangu wa kikatiba kwa dhamana yangu ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, kifungu cha 26 cha Katiba yetu kinaweka dhima ya uongozi wa nchi yetu. Kifungu ndicho kinaweka uwepo wa Rais wetu, kinampa dhamana ya kuwa ndiye Mkuu wa nchi yetu ya

Zanzibar, kuwa Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na pia kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kiongozi huyu anapatikana kwa njia ya uchaguzi unaofanywa na wananchi wenye sifa za kuchagua. Kutokana na Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 20 Machi mwaka jana (2016), kwa sasa Rais wetu, Mkuu wa nchi ya Zanzibar, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza letu la Mapinduzi ni Dkt. Ali Mohamed Shein. Ndiye aliyechaguliwa na wananchi walio wengi kuwaongoza kwa miaka mitano hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sisi sote ni mashahidi wa uongozi thabiti, wenye subra, hekima na uadilifu mkubwa wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Tumeshuhudia mwaka mwengine wa mafanikio ya pekee chini ya uongozi wake. Naomba tu uniruhusu, kwa sasa nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi mahiri na kumaliza vyema mwaka mmoja wa kipindi chake cha uongozi wake. Kwangu mimi sina budi pia kumshukuru sana kwa imani yake inayoendelea kwangu inayodhihirika katika uamuzi wake wa kuendelea kunipa dhamana kubwa ya kuiongoza wizara hii ambayo ndio roho ya serikali, Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa dhati ya nafsi yangu namuombea Mhe. Rais kuendelea kuwa mfano wa uongozi wa uadilifu, uongozi uliojaa hekima na uongozi wa kuwapenda bila ya ukomo watu wote anaowaongoza**.**

Mhe. Spika, mafanikio tunayoyaona kwa Mhe. Rais yanachangiwa pia na ushauri na usaidizi mzuri kutoka kwa msaidizi wake wa karibu, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais na Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Barazani. Mhe. Balozi Seif nae amejipambanua kwa uongozi imara, usioyumba na usaidizi wa dhati kwa Rais wetu. Nasi tunampongeza sana na kumshukuru kwa miongozo yake anayotupatia katika kuhakikisha uwepo wa utendaji ulio bora. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niruhusu pia nitumie fursa hii kuwakaribisha na kuwapongeza sana wenzetu, Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil ambao wameteuliwa na Mhe. Rais, kuwa Wajumbe wa Baraza hili muhimu. Pili kwa Mhe. Dkt. Sira kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na hivyo Waziri Asiye na Wizara Maalum. Namkaribisha tena Dkt. Sira nikijua kuwa sio mgeni katika Baraza hili na nikitambua mchango wake mkubwa katika Baraza lililopita. Tunawaombea kwa Allah Mtukufu utumishi shupavu na imara kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza letu hili limeonesha utendaji imara wa kuisimamia serikali. Mwaka mmoja wa uhai wa Baraza hili la tisa umeweka viwango vipya vya utendaji wa chombo hiki muhimu kwa uhai na maendeleo ya Zanzibar. Nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mhe. Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi, nampongeza sana Naibu wako Mhe. Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa Baraza, Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Wajumbe wote wa Baraza hili. Utendaji wa mwaka huu mmoja umedhihirisha kuwa tukishirikiana vyema, kwa umoja wetu tuna nafasi kubwa ya kuwatumikia vyema wananchi wote wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, umoja wetu huo unadhihirika tena katika kikao hiki cha Bajeti kwa Waheshimiwa Wajumbe kuisimamia vyema serikali, kuihoji na kuwakilisha maslahi ya wananchi wa majimbo

wanaowawakilisha bila ya kusahau maslahi makubwa zaidi ya Taifa letu. Hongereni sana Waheshimiwa Wajumbe wote.

Mhe. Spika, katiba yetu, chini ya Kifungu cha 9, imeweka bayana kuwa mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe. Kwamba nguvu na uwezo wa serikali kufuatana na Katiba unatoka kwa wananchi wenyewe. Ni dhahiri kuwa, pamoja na kutoa ridhaa yao kwa chama na viongozi wa kuwaongoza, wananchi ndio wenye mamlaka ya kuongoza nchi na hivyo wana nafasi muhimu sana katika utawala na maendeleo yao.

Mhe. Spika, kwa mukhtadha huu, pongezi zangu haziwezi kukamilika bila ya kutambua, kushukuru na kupongeza mchango adhimu wa wananchi wote wa kila kona ya Zanzibar, ukiwemo wa kuendelea kuipa ridhaa serikali kuwaongoza na kusimamia maendeleo yao. Katika ridhaa hiyo, wananchi pia wameendeleza utulivu ambao unaipa serikali murua wa kutekeleza wajibu wake na wamedumisha amani inayowezesha nao kila mmoja kufanya shughuli zake za kijamii na kujiimarisha kiuchumi. Nawashukuru sana wananchi wote kwa imani yao, utulivu na mchango wao mkubwa katika kuiendeleza mbele nchi yetu.

Mhe. Spika, tumo katika Baraza hili tukiwa Wajumbe ama wa kuchaguliwa na wananchi katika Majimbo yetu ya uchaguzi, kupitia viti maalum au kwa uteuzi wa Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa upande wangu, mimi ni muwakilishi niliyechaguliwa na Wananchi wa Jimbo la Donge. Kwa fursa hii, na kwa mara nyengine tena, naomba kuwashukuru sana viongozi na wananchi wote wa Jimbo la Donge kwa mashirikiano makubwa wanayoendelea kunipa. Wananchi wa Donge waendelee kunivumilia na kunipa ari na nguvu kubwa za kutekeleza majukumu yangu kwao na kwa Taifa langu. Nasema sitoacha kuwashukuru siku zote kwa imani yao isiyoyumba kwangu mimi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, pongezi na shukurani, niruhusu sasa niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2016/17.

HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO

Mhe. Spika, maelezo ya kina juu ya mwenendo wa uchumi wa dunia, kanda na Zanzibar nimeshayatoa leo asubuhi ya leo wakati nikiwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17. Hivyo, si azma yangu kuyarudia tena maelezo yale bali niruhusu tu kutaja tena mambo muhimu yaliyojitokeza katika uchumi wetu.

Kwanza, ni ukweli kwamba uchumi wetu umeendelea kukua, kwa ukuaji halisi wa Pato la Taifa wa asilimia 6.8 mwaka 2016 kutoka asilimia 6.5 mwaka 2015 na hii inadhihirisha kuwa tumeendelea kupata mafanikio makubwa zaidi ya kiuchumi mwaka 2016, kushinda mwaka 2015. Kwa ujumla sasa Pato letu la Taifa limefikia TZS trillioni 2,628 kwa bei za mwaka 2016.

Mhe. Spika, inatia moyo zaidi kuona kuwa mafanikio haya ya ukuaji wa uchumi yametokea wakati mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Kanda ya Kusini mwa Jangwa la Sahara umeonesha kudorora. Aidha, mafanikio yamepelekea wastani wa pato la mtu kupanda kutoka

TZS 1,633,000 (Dola za Kimarekani 818) hadi TZS 1,806,000 (Dola 830). Kilimo cha mazao, hoteli na mikahawa, na ujenzi ndio sekta ndogo zilizoongoza kwa mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/17

Mapato

Mhe. Spika, Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilihusisha jumla ya TZS 841.5 bilioni iliyotokana na mapato ya ndani ya TZS 482.4 bilioni na mapato kutoka nje ya TZS 324.8 bilioni. Kiasi kilichobakia cha TZS 34.3 bilioni kilitarajiwa kitokane na mikopo ya ndani ya TZS 33.0 bilioni na fedha za msamaha wa madeni (*MDRI*) TZS 1.3 bilioni.

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, itakumbukwa kuwa Baraza lako liliidhinisha makadirio ya mapato ya ndani ya TZS 482.4 bilioni kwa mgawanyo wa ukusanyaji ufuatao:

a) Bodi ya Mapato (*ZRB*) TZS 237.4 bilioni;
b) Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*) TZS 188.8 bilioni;
c) Mapato ya Mawizara TZS 26.4 bilioni;
d) Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT TZS 21.0 bilioni;
e) Gawio la faida kutoka Benki Kuu (*BoT*) TZS 4.0 bilioni; na
f) Gawio la faida kutoka Mashirika ya SMZ TZS 4.8 bilioni.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato ya nje, serikali ilikadiria kupata jumla ya TZS 324.8 bilioni, ikiwemo ruzuku ya TZS 93.3 bilioni na mikopo ya TZS 231.5 bilioni.

MATUMIZI

Mhe. Spika, kutokana na mapato hayo ya TZS 841.5 bilioni, Baraza lako liliidhinishia serikali kutumia jumla ya TZS 445.9 bilioni kwa kazi za kawaida na TZS 395.6 bilioni kwa kazi za maendeleo. Matumizi hayo yamegawanyika kwa utaratibu ufuatao:

a) Mishahara ya wafanyakazi TZS 223.7 bilioni
b) Matumizi mengineyo TZS 80.6 bilioni
c) Matumizi ya kazi za maendeleo TZS 395.6 bilioni ambapo mchango wa SMZ ni TZS 71.1 bilioni na Washirika wa maendeleo ni TZS 324.8 bilioni.
d) Matumizi ya Mfuko Mkuu ni TZS 82.3 bilioni.

UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA
(JULAI 2016 - MACHI 2017):

MAPATO

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa cha utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/17, jumla ya TZS 448.2 bilioni zimekusanywa, sawa na asilimia 110 ya matarajio ya kukusanya TZS 406.9 bilioni. Makusanyo haya yanajumuisha makusanyo ya ndani ya TZS 389.6 bilioni na mapato kutoka nje ya TZS 58.6 bilioni. Kwa ujumla, mapato yamekuwa kwa asilimia 12.3 ikilinganishwa na TZS 391.0 bilioni zilizokusanywa hadi Machi 2016.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mapitio, mafanikio mazuri zaidi yamejitokeza katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kufikia TZS 389.6 bilioni, sawa na asilimia 108 ya lengo la kipindi hicho. Ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2015/16 ambapo mapato ya ndani yalifikia TZS 306.1 bilioni, mapato yameongezeka kwa asilimia 27.3.

Mhe. Spika, mapato ya kodi ndio yamefanya vizuri zaidi ambapo jumla ya TZS 366.0 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 108.6 ya makisio ya jumla ya TZS 337.0 bilioni. Ukusanyaji huo unamaanisha ukuaji wa makusanyo ya kodi kwa asilimia 27 kutoka TZS 288.5 bilioni zilizokusanywa hadi Machi 2016. Aidha, mapato yasiyo ya kodi nayo yamekua kwa asilimia 34 kutoka TZS 17.6 bilioni za mwaka jana hadi TZS 23.6 bilioni, sawa na asilimia 94 ya makisio ya jumla ya TZS 25.2 bilioni kwa miezi tisa ya mwaka huu.

Mhe. Spika, taswira ya jumla ya utendaji inaashiria kuimarika kwa mapato kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani uliochangiwa na mambo yafuatayo:

i. Kuimarika kwa usimamizi kwa *ZRB* na *TRA*;
ii. Kuimarika kwa uchumi kutokana na ukuaji wa asilimia 6.8;
iii. Kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar ambapo mwaka 2016 tulipokea watalii 82,000 zaidi na kufikia watalii 376,242 kutoka watalii 294,243 wa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 28.
iv. Kuimarika kwa shughuli za biashara kutokana na, miongoni mwa mambo mengine, amani na utulivu uliopo nchini.
Utendaji wa Mapato yasiyo ya kodi umeathiriwa na kuchelewa kulipwa kwa gawio la SMZ kutokana na faida ya Benki Kuu ambalo hatimae limelipwa katika robo ya nne badala ya robo ya tatu ya mwaka.

Mhe. Spika, kutokana na mwenendo huo mzuri wa ukusanyaji wa mapato yetu, serikali haikuhitaji kutumia sana fursa ya kukopa ndani iliyoidhinishwa na Baraza lako. Utakumbuka kuwa mwaka jana, serikali iliomba na Baraza lako liliidhinisha kukopa ndani jumla ya TZS 33.0 bilioni ili kuziba nakisi ya Bajeti ya kiasi hicho. Hadi Machi 2017, fedha zilizokopwa ndani ni TZS 8.1 bilioni tu, sawa na asilimia 24.5 ya Bajeti ya mwaka.

Mhe. Spika, wazee wetu waliotangulia wametutaka kuwatunza wachezao kwao. Mwenendo wa utendaji wa taasisi zetu za ukusanyaji wa mapato kwa mwaka huu unaoendelea umeonesha utendaji mzuri na ulioimarika sana. Naomba nitumie fursa hii kuwatunza kwa kuwapongeza sana

viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*) hapa Zanzibar pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*). Utendaji wao pamoja na jitihada za serikali za kudhibiti matumizi ya fedha za umma zimesaidia sana katika kuimarisha huduma za serikali. Naamini kuwa jitihada hizi zitaendelezwa katika mwaka ujao kwa kuziba mianya iliyobakia na kuimarisha zaidi mapato yetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato ya nje, kukwama utekelezaji wa baadhi ya miradi mikubwa, ikiwemo ujenzi wa jengo jipya la abiria, kumepelekea taswira ya utekelezaji tofauti na iliyoonekana katika mapato ya ndani. Kwa sababu hii, uingiaji wa mikopo na ruzuku kutoka nje ni chini ya matarajio. Hadi kufikia Machi 2017, ni TZS 58.6 bilioni tu zimekusanywa kutokana na mikopo na ruzuku kutoka nje, sawa na asilimia 18 ya matarajio ya mwaka. Kiasi hicho kinatokana na TZS 30.8 bilioni za ruzuku na TZS 27.8 bilioni za mikopo. Ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana ambapo jumla ya TZS 82.8 bilioni zilipatikana, kunajitokeza pia kushuka kwa mapato ya nje kwa asilimia 29.3.

Mhe. Spika, kuhusu uendelezaji wa ujenzi wa Jengo jipya la Uwanja wa Ndege, bado Serikali inaupa mradi huu umuhimu wa kipekee kutokana na mchango unaotarajiwa kiuchumi na kijamii. Kwa mnasaba huu, jitihada maalum zimechukuliwa kuhakikisha kuwa mradi unakwamuka na ujenzi wa jengo hilo unaendelea. Mazungumzo zaidi yamefanyika baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China pamoja na Benki ya *Exim* ambayo inagharamia ujenzi huo kwa mkopo.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali yetu katika kupiga hatua zaidi za maendeleo. Baada ya mazungumzo ya pande mbili hizi inatarajiwa kuwa sasa ujenzi utaendelea tena mapema mwaka ujao wa fedha na hatimae kukamilika mwishoni mwakani.

MATUMIZI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mapitio, matumizi halisi yalifikia jumla ya TZS 424.8 bilioni, yakijumuisha matumizi ya vyanzo vya ndani ya jumla ya TZS 378.3 bilioni na TZS 46.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/17, kunajitokeza ongezeko la matumizi la asilimia 20.4 kutoka TZS 352.9 bilioni zilizotumika kwa miezi tisa hadi Machi 2016.Kati ya matumizi hayo, TZS 338.8 bilioni zimetumika kwa Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 100 ya lengo lililowekwa.

Mhe. Spika, Mgawanyo wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo:

i. Mishahara TZS 149.5 bilioni sawa na asilimia 99 ya lengo;
ii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ya TZS 80.6 bilioni sawa na asilimia 112 ya lengo;
iii. Ruzuku kwa Taasisi TZS 42.2 bilioni sawa na asilimia 97; na
iv. Matumizi mengineyo ya kuendeshea ofisi (*other charges*) TZS 66.5 bilioni sawa na asilimia 102 ya lengo.

Mhe. Spika, tokea mwezi wa Aprili mwaka jana serikali ilianzisha Pencheni ya Wazee ambapo wazee wote waliofikisha umri wa miaka 70 hulipwa Shilingi elfu ishirini kila mwezi. Katika kipindi cha mapitio, serikali imetekeleza vyema utaratibu huo ambapo malipo yamekuwa yakifanyika tarehe 15 ya kila mwezi nchini kote, Unguja na Pemba. Malipo haya yamesaidia sana wazee wetu sio tu kwa mahitaji yao madogo madogo bali pia kuongeza imani kwa serikali yao inayowajali.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho serikali pia imetumia jumla ya TZS 39.5 bilioni ikiwa ni mchango wake katika utekelezaji wa kazi za maendeleo, sawa na asilimia 93 ya lengo la TZS 42.7 bilioni. Kazi hizo zinajumuisha matengenezo makubwa katika sekta ya habari kwa lengo la kuwa na studio za kisasa za utangazaji ili kuimarisha huduma zinazotolewa na Shirika la habari Zanzibar. Matengenezo hayo ni pamoja na Uimarishaji wa Shirika la Utangazaji Redio na Televisheni ikiwemo kampuni ya usambazaji maudhui (*ZMUX*), kuimarisha vifaa vya kurushia matangazo kwa kutumia *"Microwave link"* na Mkonga wa Taifa kwa vituo vyote vya Unguja na Pemba, kulifanyia matengenezo makubwa jengo la *ZBC* Televisheni kwa kuweka mfumo mpya wa umeme na hewa baridi, kununua vifaa vya kisasa vya kurikodia na kurushia matangazo pamoja na kutengeneza studio zote za redio na televisheni.

MFUKO WA MIUNDOMBINU (*INFRASTRUCTURE FUND*)

Mhe. Spika, serikali ilianzisha Mfuko wa Miundombinu ili kufanikisha uimarishaji wa Miundombinu ya Msingi kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato. Lengo ni kuharakisha maendeleo ya miundombinu muhimu kwa kutumia rasilimali zetu wenyewe. Kwa mwaka unaoendelea wa fedha, jumla ya TZS 26.6 bilioni zimetarajiwa kupatikana na kuingizwa katika Mfuko huo. Hadi Machi 2017, jumla TZS 21.0 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 105 ya lengo la miezi tisa. Makusanyo hayo yanajumuisha TZS 13.3 bilioni kutoka *ZRB* na TZS 7.7 bilioni kutoka *TRA.*

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, fedha kutoka Mfuko wa Miundombinu zilitarajiwa kugharamia utekelezaji wa Miradi kumi na moja (11) kama nilivyoiainisha katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana. Hadi mwishoni mwa Machi 2017, jumla ya TZS 17.1 bilioni zimetumika kutoka Mfuko wa Miundombinu kwa kugharamia Miradi ya uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi, kulipa fidia barabara ya Ole – Kengeja, na ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu.

Mhe. Spika, serikali pia ilitoa ahadi ya kuwapelekea nishati ya umeme wananchi wenzetu wanaoishi katika visiwa vyote vidogo vidogo, awamu kwa awamu. Kwa mwaka unaoendelea wa fedha (2016/17), Baraza lako liliidhinisha matumizi ya TZS 2.0 bilioni kwa ajili ya kupeleka umeme katika Kisiwa cha Fundo ili kuanza utekelezaji wa azma hiyo. Nina furaha kulijuulisha Baraza hili kuwa hadi Machi 2017 tayari serikali imeipatia *ZECO* jumla ya TZS 1.8 bilioni kutoka Mfuko wa Miundombinu kwa madhumuni hayo.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, tayari *ZECO* imeshatekeleza matayarisho yote kwa kufanikisha upelekaji wa umeme katika kisiwa hicho. Hatua iliyobakia ni uwekaji wa waya wa chini ya bahari ambao utakamilika kutengenezwa mwishoni mwa mwezi huu wa sita. Mradi unatarajiwa kukamilika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/18. Kukamilika kwa mradi huo ni hatua muhimu sana ya

kuharakisha maendeleo ya wananchi wenzetu, wakaazi wa kisiwa cha Fundo.

DENI LA TAIFA:

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Deni la Taifa limefikia TZS 377.1 bilioni, kutoka deni la TZS 398.6 bilioni lililokuwepo mwezi Machi 2016. Deni hili limejumuisha deni la nje TZS 270.2 bilioni ambalo limeongezeka. Naomba Mhe. Spika, hapo kuwe na masahihisho, ambalo limeongezeka kwa asilimia 1.3 kutoka TZS 266.8 bilioni. Aidha, deni la ndani ni TZS 106.8 bilioni ambalo limepungua kutoka TZS 130.2 bilioni, ambapo upungufu huo ni sawa na asilimia 21.9. Mafanikio yanatokana na mkazo uliowekwa na serikali katika ulipaji wa madeni ikiwemo deni la kiinua mgongo cha wastaafu serikalini. Katika kipindi hicho, jumla ya TZS 19.1 bilioni zimetumika kulipa kiinua mgongo cha Wastaafu 1,455. Serikali pia imelipa deni la Hati Fungani iliyoiva pamoja na kulipa riba kwa mikopo mingine ya ndani.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia Pato letu la Taifa kama nilivyoeleza awali, deni hilo ghafi ni sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Kutokana na ukuaji wa uchumi na mwenendo mzuri wa mapato ya ndani na hadhari kubwa inayochukuliwa ya kudhibiti kuongezeka sana Deni la Taifa, uwiano huo wa Deni na Pato la Taifa unaonesha kuwa: (i) Serikali inahimili deni hilo; (ii) nchi inakopesheka; na (iii) tuna uwezo wa kulipa madeni.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17, serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato ya ndani. Matokeo ya utekelezaji wa baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo:

i. Ada ya Ukaguzi wa Bidhaa katika kituo *(Destination Inspection Fee)* na Uthibitishaji wa Bidhaa *(Customs Declaration-TANSAD)*

Mhe. Spika, hatua hii imehusisha utozwaji wa Ada ya Ukaguzi wa bidhaa *(Destination Inspection Fee)* kwa asilimia 0.6 ya thamani ya bidhaa iliyoingizwa na Ada ya Uthibitishaji wa Bidhaa *(Customs Declaration-TANSAD)* ambayo ni 10 USD kwa kila kadhia ya Forodha kwa ajili ya kuimarisha *TRA* na *ZRB*. Jumla ya TZS 1.4 bilioni zimekusanywa hadi kufikia Machi 2017 sawa na asilimia 21 ya lengo la mwaka la kukusanya TZS 6.68 bilioni.

ii. Vibali vya Kodi kwa Wazabuni *(Tax Clearance Certificate)*

Mhe. Spika, Jumla ya TZS 32.4 bilioni zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii ambapo TZS 31.8 bilioni zimetokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na TZS 0.6 bilioni ni kutokana na Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*).

iii. **Uhaulishaji wa magari kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara**

Mhe. Spika, hatua imehusisha kukusanya tofauti ya kodi wakati magari hayo yanapotaka kuhaulishwa kwenda Tanzania Bara. Hatua hii imeiningizia Serikali jumla ya TZS 6.8 bilioni hadi Machi 2017.

iv. Usajili wa Vyombo vya Moto

Mhe. Spika, serikali ilidhinishiwa kusajili kwa namba za Zanzibar vyombo vyenye usajili wa Tanzania Bara vilivyopo Zanzibar ili kuleta usawa katika utekelezaji wa sheria na usajili. Hatua hii ilichelewa kutekelezwa hivyo hadi Machi 2017 ni TZS 90 milioni tu zimeweza kukusanywa.

MATARAJIO HADI JUNI 2017

MAPATO

Matarajio ya Mapato Julai – Juni 2016/2017

Mhe. Spika, inatarajiwa kwamba hadi kufikia Juni 2017, mapato kwa ujumla, yatafikia TZS 668.3 bilioni sawa na asilimia 86 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 841.5 bilioni. Kati ya fedha hizo, na kutokana kuimarika kwa utendaji wa *TRA* na *ZRB* na mwenendo mzuri wa uchumi wetu, mapato ya ndani yanatarajiwa kuvuka lengo na kufikia TZS 530.2 bilioni, sawa na asilimia 110 ya makisio ya mwaka ya TZS 482.4 bilioni.

Mhe. Spika, matarajio ya ukusanyaji wa mapato hayo Kitaasisi ni kama ifuatavyo:

i. TRA inatarajiwa kukusanya TZS 211.3 bilioni na hivyo kuvuka lengo kwa TZS 22.5 bilioni, sawa na utendaji wa asilimia 112 ya lengo;

ii. ZRB inatarajiwa kuvuka lengo kwa utendaji wa asilimia 113 sawa na nyongeza ya TZS 35.3 bilioni kwa mapato kufikia TZS 307.9 bilioni. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi ni TZS 265.3 bilioni, sawa na asilimia 117 ya lengo la kukusanya TZS 237.4 bilioni na mapato yasiyokuwa ya kodi ni TZS 42.6 bilioni sawa na asilimia 131 ya lengo la TZS 32.5 bilioni;

iii. PAYE kutoka SMT inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo; na

iv. Mikopo ya ndani inatarajiwa kufikia TZS 8.1 bilioni sawa na asilimia 24.5 ya Bajeti ya kukopa TZS 33.0 bilioni.

Mhe. Spika, kutokana na sababu nilizozieleza awali, mikopo na ruzuku kutoka nje inatarajiwa kufikia jumla ya TZS 150.0 bilioni sawa na asilimia 46.2 ya makadirio ya mwaka.

MATUMIZI

Mhe. Spika, inatarajiwa kwamba hadi kufikia Juni 2017, kwa ujumla matumizi yatafikia TZS 687.2 bilioni sawa na asilimia 81.7 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 841.5 bilioni. Matumizi hayo yamejumuisha ongezeko la mshahara kwa kipindi cha April hadi Juni 2017.

Mhe. Spika, mchanganuo wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo:

Matumizi ya kawaida yatafikia TZS 470.2 bilioni kama ifuatavyo**:**

i. Mishahara (Wizara) TZS 223.8 bilioni

ii. Mishahara (Ruzuku) TZS 26.7 bilioni
iii. Matumizi Mengineyo (Wizara) TZS 90.0 bilioni
iv. Matumizi mengineyo (Ruzuku) TZS 31.1 bilioni
v. Mfuko Mkuu wa Serikali (*CFS*) TZS 98.6 bilioni
vi. Matumizi Mengineyo (Wizara) TZS 90.0 bilioni
vii. Matumizi mengineyo (Ruzuku) TZS 31.1 bilioni
viii. Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS) TZS 98.6 bilioni

Matumizi ya maendeleo yatafikia TZS 217.0 bilioni kwa mgawanyo ufuatao:

i. Mchango wa Serikali TZS 67.0 bilioni
ii. Mikopo na Ruzuku TZS 150.0 bilioni

MAREKEBISHO YA MISHAHARA, 2016/2017

Mhe. Spika, katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi kupandisha kima cha chini cha mshahara ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wake katika awamu hii ya pili. Nyongeza hiyo ni kutoka TZS 150,000/= hadi kufikia TZS 300,000/= kwa wafanyakazi wa kawaida Serikalini na kutoka TZS 203,000 za sasa hadi TZS 406,000/- kwa mwezi kwa Wafanyakazi wa Idara maalum za SMZ ili walingane na wenzao wa vikosi vya SMT. Kwa makundi yote mawili, ongezeko hili ni sawa na nyongeza ya asilimia 100 ya kima cha chini cha mishahara.

Mhe. Spika, huu ni muendelezo wa jitihada za Mhe. Rais za kuimarisha maslahi na hivyo kuleta ufanisi kazini ambazo amekuwa akizichukua tokea kuingia madarakani. Katika Hotuba yangu ya Bajeti ya Serikali ya mwaka jana nilieleza kuwa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais itatetekelezwa kwa kufanya marekebisho hayo ya mshahara kuanzia mwezi wa Aprili, 2017. Sambamba na nyongeza hiyo, niliahidi pia kupunguza Kodi ya Mapato (*PAYE*) kwa kundi la kipato cha chini kutoka asilimia 13 hadi asilimia tisa, ili kuimarisha zaidi maslahi ya wafanyakazi wa kima cha chini cha mshahara kwa kuzingatia gharama za maisha.

Mhe. Spika, tuna wasia wa wazee wetu. Wazee walitusisitiza kuwa "ahadi ni deni". Wakatuambia pia kuwa "uungwana ni vitendo, tutende watu wataona". Nina furaha kulijuilisha Baraza lako hili kuwa serikali imetekeleza ahadi zake.

Kwanza, kama alivyoahidi Mhe. Rais, Serikali imepandisha mshahara wa kima cha chini kwa makundi yote mawili kwa asilimia 100.

Pili, aliahidi nyongeza hiyo itaanza April 2017 na imeanza Aprili 2017.

Na tatu, kiwango cha kodi kwa kundi la mwanzo linaloanza kutozwa kodi kimepunguzwa kutoka asilimia 13 ya kabla hadi asilimia 9. (*Makofi*)

Mhe. Spika, huo ndio uungwana, na hivyo ndio vitendo vya Serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein. Ameahidi na ametenda; Kwa hivyo yeye ni Muungwana. Sasa ni jukumu letu watumishi wa umma kuuenzi uungwana huu kwa kuongeza jitihada zenye ufanisi katika kuwahudumia vyema zaidi wananchi wote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa sasa marekebisho hayo yatawahusu, kwa viwango tofauti, wafanyakazi wote wa serikali na taasisi zake zipatazo ruzuku ya Mishahara kutoka Serikalini isipokuwa wale ambao mishahara yao kwa mwezi inafikia TZS 1,500,000.00 au zaidi. Hata hivyo, marekebisho hayo yanaambatana pia na marekebisho ya kiasi cha kipato ambacho kitasamehewa Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi Binafsi. Ili kuleta uwiano baina ya sekta hizo mbili na kwa azma ya kupunguza athari kwenye mapato ya Serikali, kiasi cha kipato kutokana na ajira ambacho kitasamehewa kodi ni hadi TZS 180,000/= kwa mwezi sawa na TZS 2,160,000 kwa mwaka.

Mhe. Spika, mwaka jana nilieleza kuwa Serikali inafanya marekebisho haya ikielewa athari yake kwenye Bajeti. Kwa sasa, zoezi hili la marekebisho ya mishahara litahitaji ziada ya TZS bilioni 6,126.9 kwa mwezi ambapo ni ziada ya TZS bilioni 2,317.6 kwa mwezi ni kwa ajili ya Idara Maalum wakati kwa wafanyakazi wengine wa Serikali, ziada ni TZS bilioni 3,809.3 kwa mwezi. Kwa kipindi cha miezi mitatu (Aprili – Juni, 2017), jumla ya TZS bilioni 18,381 za ziada zitahitajika kwa ajili ya kukidhi nyongeza ya mshahara ambapo kwa ujumla, mishahara sasa itagharimu TZS 22.7 bilioni kwa mwezi kutoka wastani wa TZS 16.6 bilioni kwa mwezi.

Mahitaji hayo ya ziada yalizingatiwa katika Bajeti inayoendelea na hivyo yataweza kulipwa na hayataathiri utendaji wa maeneo mengine ya Bajeti.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu, visiwa vyetu vinapata nishati ya umeme kutoka Tanzania Bara. Shirika letu la ZECO linanunua umeme huo kutoka Shirika la Umeme la Tanzania Bara, *TANESCO*. Kutokana na sababu mbalimbali, kumejitokeza deni ambapo *ZECO* inadaiwa na *TANESCO* ambapo ankara za miezi kadhaa ama hazikulipwa kwa ukamlifu au hazikulipwa kabisa. Pia kuna sehemu ya deni ambayo inatokana na kutokubaliana baina ya Mashirika hayo, na wakati mwengine na Msimamizi wa bei za huduma hizo kwa Tanzania Bara, *EWURA*.

Mhe. Spika, Kwa upande mwengine, deni linachangiwa pia na madeni ya ndani yanayodaiwa kwa wateja mbalimbali wa *ZECO* ikiwemo Serikali. Kwa mujibu wa kumbukumbu za *ZECO*, deni linalokubalika na ambalo halina utata ni TZS 65.6 bilioni. Deni hili la kibiashara linapaswa kulipwa.

Mhe. Spika, Naomba kulitaarifu Baraza lako kuwa tayari *ZECO* limeanza kulipa deni lake kwa *TANESCO*. Kwa upande wake, Serikali pia inaiwezesha ZECO kwa kulipa deni linalodaiwa na Shirika hilo. Kwa hatua za awali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa jumla ya TZS 10.0 bilioni kwa ajili ya kulipwa *TANESCO* kwa mujibu wa makubaliano ambayo yamefikiwa na Serikali mbili katika kushughulikia deni hilo.

Mhe. Spika, kwa robo hii ya mwisho ya mwaka 2016/17, Serikali inatarajia pia kulipa jumla ya TZS 3.0 bilioni sawa na wastani wa TZS 1.0 bilioni kila mwezi. Aidha, SMZ imeikumbusha SMT kuilipa *TANESCO* jumla ya TZS 18.0 bilioni ambazo zilipaswa kulipwa SMZ mwaka 2011/12 kutokana na marejesho ya kodi ya *PAYE*. Awali SMZ iliomba kuwa fedha hizo zilipwe *TANESCO* ili kupunguza deni la *ZECO* lakini hadi sasa bado hazijalipwa. Kwa upande wake, *ZECO* pia italipa jumla ya TZS 5.6 bilioni hadi Juni 2017. Aidha, Serikali inatarajia kuwa SMT nayo italipa deni ambalo *ZECO* inadai Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar linalofikia TZS 2.2 bilioni ambazo nazo zitapunguza deni la *TANESCO*. Kwa utaratibu huu, hadi kufikia mwisho

wa mwezi Juni 2017, inatarajiwa kuwa *ZECO* itakuwa imeshailipa *TANESCO* jumla ya TZS 40.4 bilioni.

MWELEKEO WA BAJETI YA 2017/18

Mhe. Spika, Serikali imo katika kipindi cha miaka mitano ya mwisho cha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020. Kwa dhamira ya utekelezaji huo, tayari Serikali imeidhinisha Mkakati mpya wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (*MKUZA III*) ambao unahitaji Wizara na Taasisi zote kujielekeza katika kutimiza wajibu wake ili malengo yake yaweze kufikiwa na nchi ipate maendeleo zaidi.

Mhe. Spika, asubuhi ya leo nimetoa maelezo ya kina juu ya maeneo matano makuu ya matokeo pamoja na maeneo 23 ya Kimkakati katika *MKUZA III*. Mkazo utaendelea kuwekwa katika kugharamia uendeshaji wa serikali pamoja na mipango ya Maendeleo kwa kutumia rasilimali za ndani pamoja na kuwa bado Washirika wa Maendeleo watakuwa na nafasi ya kusaidia jitihada za serikali. Wakati jitihada zikiongezwa katika taasisi za ukusanyaji za *TRA* na *ZRB*, kila Wizara itapaswa pia kusimamia vyema vianzio vya mapato vilivyo katika Wizara na Taasisi zao.

VIPAUMBELE VYA KITAIFA:

Mhe. Spika, Serikali inaelewa haja ya kuwa na maeneo machache ya vipaumbele kwa utekelezaji ili kuweza kuwa na matokeo makubwa zaidi. Hata hivyo, kwa kuzingatia hali yetu ya maendeleo, bado tunahitaji kuzingatia maeneo mengi zaidi ili kujikwamua katika hali ya sasa. Kwa mnasaba huo, kwa mwaka 2017/18, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ni haya yafuatayo:

a) Kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, makaazi na upatikanaji wa maji safi na salama;
b) Kuimarisha miundombinu ya uingiaji nchini inayojumuisha bandari na viwanja vya ndege;
c) Kuimarisha miundombinu ya msingi ikiwemo barabara na nishati;
d) Kuendelea kuimarisha Utalii hususan katika maeneo yaliyotajwa awali katika Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (*R4P*);
e) Kushajiisha zaidi uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio;

Mhe. Spika, maeneo mengine ya Kipaumbele ni:

f) Kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uimarishaji wa uvuvi wa bahari kuu na uendelezaji wa mifugo;
g) Kukuza uwezo wa watalamu katika fani zenye upungufu mkubwa wa wataalamu (afya, kilimo, viwanda, mafuta na gesi asilia), mafunzo ya amali na uendelezaji wa ujasiriamali;
h) Kufanya tafiti mbali mbali katika sekta zote zitakazosaidia utoaji sahihi wa maamuzi na upangaji wa mipango ya maendeleo;

Utawala bora na uimarishaji wa taasisi kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; uwekaji mji katika hali ya usafi na usalama.

MWELEKEO WA MAPATO:

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, tunakumbuka kuwa pamoja na hatua kubwa zinazoendelea kuchukuliwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, bado kuna fursa ya kuongeza mapato hayo bila ya kuathiri uwekezaji nchini. Lengo la Serikali ni kutimiza kwa vitendo shabaha ya Chama Cha Mapinduzi kama ilivyoelezwa katika Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ya kukusanya angalau TZS 800.0 bilioni kutoka mpato ya ndani ifikapo mwaka 2019/20. Tayari Zanzibar inaonesha kiwango cha juu cha ukusanyaji wa mapato kulingana na uchumi wake ambapo uwiano wa mapato ya ndani na Pato la Taifa ni asilimia 22.6 kwa mwaka 2016/17.

Mhe. Spika, Uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa ni asilimia 21. Jitihada zaidi zinakusudiwa kuwekwa mwaka 2017 kwa uwiano wa mapato ya ndani kufikia asilimia 23.5 ya Pato la Taifa wakati mapato yatokanayo na kodi yakifikia asilimia 22.8 ya Pato la Taifa.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia shabaha hizo za Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake ya Mapinduzi ya Zanzibar, jumla ya TZS 675.8 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kwa mwaka 2017/18 kutoka katika vyanzo vya ndani kwa mchanganuo ufuatao:

i. *ZRB* imepangiwa kukusanya TZS 347.3 bilioni kutokana na mapato ya Kodi;
ii. *TRA* imekadiriwa kukusanya TZS 258.7 bilioni;
iii. Mapato ya Mawizara na Gawio la Mashirika ya SMZ TZS 48.8 bilioni; na
iv. Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT ni TZS 21.0 bilioni.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18, Serikali inatarajia kupokea jumla ya TZS 380.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Ruzuku ni TZS 82.2 bilioni na Mikopo ya TZS 298.3 bilioni. Bado Serikali itaendelea kuweka katika Bajeti Misaada ya Kibajeti kwa njia ya “100T” ili kuruhusu kupokelewa kwake pindi ikipatikana. Kwa sasa mwenendo wake umeendelea kuwa wa kutotabirika.

MWELEKEO WA MATUMIZI

Mhe. Spika, Serikali inakadiria kutumia jumla ya TZS1,087.4 bilioni katika mwaka wa fedha 2017/18 ikiwemo Matumizi ya Kazi za Kawaida ya TZS 590.8 bilioni na Matumizi ya Kazi za Maendeleo ya TZS 496.6 bilioni. Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya Mishahara TZS 324.7 bilioni;
ii. Ruzuku za matumizi ya kawaida TZS 64.3 bilioni;
iii. Matumizi Mengineyo (O/C) TZS 101.7 bilioni;
iv. Matumizi mengineyo ya Mfuko Mkuu TZS 100.0 bilioni;

v. Mchango wa Serikali katika Matumizi ya Maendeleo TZS 116.1 bilioni; na
vi. Mikopo na Ruzuku kutoka nje kwa Matumizi ya Maendeleo TZS 380.5 bilioni.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18, marekebisho ya mishahara yaliyoanza kutekelezwa rasmi mwezi Aprili 2017 yataambatana na ongezeko la mchango wa Mfuko wa Jamii *ZSSF* kwa muajiri kutoka asilimia 10 hadi 13. Nyongeza hii itapelekea kuongezeka kwa bajeti ya mishahara hadi kufikia TZS 25.6 bilioni kwa mwezi kutoka TZS 22.7 bilioni ya sasa.

Mhe. Spika, kwa ujumla, malipo ya mishahara yatahitaji kutengewa TZS 325.9 bilioni kwa mwaka 2017/18, sawa na asilimia 48.2 ya makadirio ya mapato ya ndani. Kiwango hicho cha malipo ya mshahara kinajumuisha pia mahitaji ya fedha kwa marekebisho mbali mbali ya mishahara kutokana na upandaji wa vyeo, ajira mpya na marekebisho yatakayohitajika kurekebisha kasoro zitakazojitokeza katika utekelezaji wa nyongeza hiyo.

Mhe. Spika, sambamba na ongezeko hilo la mishahara, Serikali pia imezingatia hali ngumu inayowakabili wafanyakazi wake wa zamani ambao kwa sasa wameshastaafu na wanaishi kwa kutegemea kipato cha pencheni. Miongoni mwao wamo watu walioshika madaraka makubwa katika nyadhifa mbalimbali ambao nao wanaishi kwa pencheni ndogo sana kutokana na msingi wa pencheni hiyo kuwa ni mishahara waliomalizia, ambayo mingine ilikuwa midogo kulinganisha na sasa hivi. Mara ya mwisho kufanyika marekebisho makubwa ya pencheni ilikuwa ni mwaka 2011 ambapo kima cha chini cha pencheni kiliongezwa kutoka Shilingi 20,000 kwa mwezi hadi Shilingi 40,000.

Mhe. Spika**,** Kwa dhamira ya kuinua kipato cha Wastaafu hao, Serikali imefanya pia mapitio ya kima cha chini cha Pencheni kwa kuzingatia kuwa kima cha sasa kimepitwa na wakati kutokana na kupanda kwa gharama za maisha. Mapitio hayo yamezingatia pia wastaafu waliokuwa na nyadhifa Serikalini ambao kwa sasa wanapokea kiwango kidogo cha Pencheni kutokana na mishahara midogo waliomalizia utumishi wao. Jumla ya TZS 10.0 bilioni zimetengwa kwa ajili ya malipo ya ziada ya pencheni kwa mwaka 2017/18 kutokana na viwango vipya ambavyo vimepangwa kuanza kutumika mara tu mwaka mpya wa fedha utakapoanza, Julai 2017. Hivi sasa Mhe. Spika, tuko kwenye mchakato na kima cha chini kitatangazwa hapo baadaye. (*Makofi*)

Mhe. Spika**,** kwa upande wa matumizi ya kugharamia Mpango wa Maendeleo ya TZS 496.6 bilioni, takriban robo yake (asilimia 23.3) yatatokana na makusanyo ya ndani. Haya ni mafanikio muhimu kwa serikali kuendelea, hatua kwa hatua, kubeba dhamana kubwa zaidi ya kugharamia maendeleo ya Zanzibar. Sambamba na hatua hiyo, sehemu kubwa ya fedha za nje pia inatokana na mikopo ya TZS 298.3 bilioni ambapo Ruzuku inatarajiwa kupungua na kufikia TZS 82.2 bilioni tu.

UGATUZI WA MADARAKA

Mhe. Spika**,** kwa muda mrefu Serikali imekuwa na dhana ya kusogeza huduma muhimu karibu zaidi na wananchi na kuimarisha uwajibikaji wake kwao. Azma hii inahitaji kuhamishwa kwa awamu majukumu ya utoaji wa baadhi ya huduma kutoka Serikali Kuu na kuhamia Serikali za Mitaa (Ugatuzi). Kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imepanga kuanza rasmi utekelezaji wa upelekaji wa madaraka hayo kwa wananchi. Kwa kuanzia, majukumu yatakayohamishiwa

Serikali za Mitaa ni pamoja na huduma za Elimu ya Maandalizi na Msingi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Afya ya Msingi kwa Wizara ya Afya na huduma za Ugani kutoka Wizara inayosimamia Kilimo.

Mhe. Spika**,** Hata hivyo, bado Miradi ya Maendeleo na shughuli zinazohusiana na Sera na Miongozo katika maeneo hayo zitasimamiwa na sekta husika sambamba na maeneo yanayohitaji ununuzi wa jumla kama vile chaki, mabuku na dawa. Jumla ya TZS 6.3 bilioni zimetengwa kwa ajili ya huduma hizo za ugatuzi zikiwemo TZS 1.0 bilioni kutoka Mfuko wa Wafadhili *(Basket Fund*) unaodhaminiwa na Danida na Unicef na TZS 1.4 bilioni kutoka SMZ.

Mhe. Spika, Chini ya utaratibu mpya, Serikali za Mitaa zitaendelea kukusanya mapato yake, kupanga na kutekeleza bajeti zake ikiwemo katika maeneo yaliyogatuliwa. Kwa kuzingatia mahitaji kutokana na majukumu ya ziada ya matumizi yatakayohamia Serikali za Mitaa, Serikali kuu itahaulisha fedha kwa njia ya ruzuku ili kugharamia majukumu ya ziada kwa maeneo "yaliyogatuliwa" kulingana na vigezo vilivyowekwa.

Mhe. Spika, Bajeti za Serikali za Mitaa zitaendelea kupitishwa na Mabaraza ya Madiwani husika ambapo Baraza la Wawakilishi litaidhinisha ruzuku kwa Serikali za mitaa kwa maeneo yaliyogatuliwa. Kwa kuanzia, ruzuku itakuwa kwa shughuli maalum (*special grant*) na haitoruhusiwa kuhaulishwa kwa ajili ya kugharamia matumizi mengine tofauti na yaliyokusudiwa.

MAZINGATIO MAALUM YA SERIKALI

Mhe. Spika**,** awali nilizungumzia juu ya deni la umeme inalodaiwa Shirika letu la *ZECO* na Shirika la umeme la Tanzania Bara, *TANESCO*. Nilisema pia kuwa kimsingi, Serikali imeamua kuchukua hatua maalum za kulisaidia *ZECO* kulipa deni lake lisilo na utata la TZS 65.6 bilioni. Baada ya malipo yaliyokwishafanyika na yale yatakayofanyika, *ZECO* itakuwa imeshalipa jumla ya TZS 40.4 bilioni hadi Juni mwaka huu. Bakaa ya deni ya TZS 25.2 bilioni itaendelea kulipwa mwaka ujao wa fedha. Serikali imepanga kuilipa *ZECO* TZS 1.0 bilioni kila mwezi ili nayo iweze kuongezea wastani wa TZS 2.0 bilioni na kufanya malipo kila mwezi kuwa wastani wa TZS 3.0 bilioni sawa na TZS 25.2 bilioni hadi Juni 2018 ambapo deni lote litakuwa limemalizika.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia dhamira yake ya kuendelea kuimarisha zaidi huduma mbali mbali na kuwaondolea shida wananchi, serikali imefanya mazingatio maalum kwa baadhi ya maeneo yanayoendana na maeneo ya kipaumbele na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Ili kutekelezwa mazingatio hayo, jumla ya TZS 57.2 bilioni zimetengwa katika Bajeti ya 2017/18 kama ifuatavyo:

i. Ununuzi wa Meli mpya ya mafuta TZS 18.0 bilioni
ii. Ulipaji wa Deni la Umeme (*TANESCO*) TZS 12.0 bilioni
iii. Uimarishaji wa Makaazi ya Askari wa Idara Maalum TZS 1.62 bilioni;
iv. Uanzishaji wa Bima ya Afya TZS 2.0 bilioni;
v. Kuongezwa Bajeti ya Ununuzi wa Dawa, chanjo na Vifaa tiba kufikia TZS 8.0 bilioni;
vi. Kupeleka umeme katika Kisiwa cha Kokota TZS 1.58 bilioni

vii. Kutoa fedha za mtaji kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali 1.5 bilioni;

Mhe. Spika, maeneo mengine maalum yaliyozingatiwa ni:

i. Kuimarisha Usafiri katika Visiwa vidogo (*landing crafts*) TZS 0.8 bilioni
ii. Kumalizia Visima vilivyojengwa kwa msaada wa Ras Al Khaimah TZS 1.5 bilioni;
iii. Umaliziaji wa Madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi TZS 2.0 bilioni;
iv. Ununuzi wa mtambo wa lami na vifaa vya barabara TZS 2.5 bilioni;
v. Kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu TZS 0.9 bilioni;
vi. Kumalizia ujenzi wa Skuli ya Sekondari JKU TZS 1.3 bilioni;
vii. Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya TZS 0.5 bilioni; na
viii. Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu TZS 2.5 bilioni.

Mhe. Spika, kama inavyojitokeza katika mchanganuo huo, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha huduma kwa wananchi wenzetu wanaoishi katika visiwa vidogo. Kwa mwaka ujao inakusudia kuanza ununuzi wa boti maalum (*landing crafts*) kwa ajili ya kutoa usafiri wa uhakika wa kuunganisha visiwa hivyo. Aidha, baada ya mafanikio yaliyopatikana mwaka 2016/17 ya kupeleka umeme katika Kisiwa cha Fundo huko Pemba, kwa mwaka ujao wa fedha serikali itapeleka umeme katika kisiwa cha Kokota, kilichooko Pemba. Pemba.

Mhe. Spika, ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa madarasa, jitihada maalum pia zinawekwa katika kumaliza madarasa yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, kutokana na umuhimu wa nishati ya mafuta ya bidhaa za petroli, serikali inakusudia kutekeleza nia yake ya kununua meli mpya ya mafuta ili kuchukua nafasi ya M.V Ukombozi ambayo sio tu imechoka sana baada ya kutumika kwa muda wake, bali pia haikidhi tena masharti ya kimataifa ya usafiri wa baharini. Aidha, bado serikali inafanyia kazi dhamira yetu ya kununua meli nyengine ya abiria pindi mazungumzo na wajenzi yatakapokamilika na hali ya fedha kuruhusu.

Mhe. Spika, Kati ya mchango wa SMZ katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya TZS 34.9 bilioni zinatarajiwa kutumika kutoka Mfuko wa Miundombinu kugharamia Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo:

i. Uimarishaji wa Taasisi ya Viwango (*ZBS*) - TZS 2.0 bilioni;
ii. Uimarishaji wa Elimu Mbadala - TZS 1.6 ilioni;
iii. Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu - TZS 1.8 bilioni;
iv. Usambazaji wa Umeme Vijijini (Kokota) - TZS 1.6 bilioni;
v. Malipo ya ujenzi wa barabara ya Mzambarauni - Madenjani - TZS 2.0 bilioni;
vi. Fidia kwa ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake Chake - TZS 1.5 bilioni;
vii. Ununuzi wa boti za usafiri visiwani (*Landing crafts*) - TZS 0.8 bilioni;
viii. Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi - TZS 20 bilioni;
ix. Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi - TZS 2.1 bilioni;
x. Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba - TZS 0.5 milioni; na
xi. Programu ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha TZS 1.0 bilioni.

Mhe. Spika, kwa kiasi kikubwa, mafanikio yanayopatikana yanatokana na kuimarika kwa uwekezaji nchini na mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi. Hotuba yangu hii

isingekamilika bila ya kuwapongeza Wawekezaji wote, wa ndani na nje, kwa mchango wao mkubwa katika ukuaji na maendeleo ya uchumi wetu. Aidha, mchango wao huo umekuwa chachu muhimu katika kuimarisha ajira, kukuza kipato na kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Mhe. Spika, napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia wawekezaji na wafanyabiashara wote, waliopo na wenye nia ya kuwekeza na kufanya biashara, kuwa serikali itaendelea kuchukua hatua zaidi za kuimarisha mazingira ya biashara nchini na ufanisi katika kushughulikia uwekezaji. Kwetu sisi, kama ilivyokuwa siku zote, "Unguja ni njema, na atakae aje". Tutaendelea kuwakaribisha na kushirikiana na Wawekezaji wote ili kufanikisha uwekezaji wao na kuhakikisha kuwa una tija iliyokusudiwa kwao, kwa Serikali na kwa Wananchi. Serikali pia inafanya mapitio ya utaratibu wa mchakato wa ushughulikiaji wa miradi kwa nia ya kuondosha urasimu na pia kuwa na kituo kimoja cha kweli cha ushughulikiaji wa miradi ya uwekezaji (*one –stop centre*).

MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ukusanyaji wa mapato ya ndani bado kuna fursa ya kuongeza zaidi mapato kutokana na viwango vilivyopo. Kwa sababu hiyo, na kwa dhamira ya kuendeleza utulivu wa sera zetu za kodi na hivyo kushajiisha zaidi uwekezaji binafsi nchini, kimsingi bado serikali haipendekezi kupandisha kodi. Badala yake, inapendekezwa kuendeleza na jitihada zinazoonesha mafanikio za kuimarisha mapato ya ndani kutokana na vyanzo vilivyopo kwa kuimarisha utendaji na kuziba mianya ya uvujaji. Kwa muelekeo huo, hatua za ziada zifuatazo zinapendekezwa:

i. Kutungwa kwa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa

Mhe. Spika, kimsingi tayari Serikali inatoza na kukusanya Ushuru wa Bidhaa kwa kutumia Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kinachopendekezwa ni kutungwa Sheria makhsusi kwa Zanzibar ili kutoza Ushuru huo kwenye mambo ambayo sio ya Muungano ambayo mamlaka ya utozaji wake yapo kwa SMZ. Lengo la hatua hii ni kuondoa utata wa kisheria kuhusu uhalali wa kutoza Ushuru huo hapa Zanzibar. Hatua hii inatarajiwa kuingizia serikali ziada ya TZS 10 bilioni.

ii. Kufutwa kwa Sheria ya Ushuru wa Stempu nam. 6 ya 1996 na kutungwa Sheria ya Ushuru wa Stempu

Mhe. Spika, kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa Ushuru wa Stempu katika Hati mbalimbali (*instruments*), katika mauzo kupitia Stakabadhi na kuweka utaratibu nafuu kwa Wafanyabiashara wadogo, inapendekezwa kufutwa kwa Sheria ya Ushuru wa Stempu namba 6 ya 1996 na kutungwa Sheria mpya badala yake. Hatua hii haikusudii kuongeza viwango vya ushuru huo na inatarajiwa kuiingizia serikali jumla ya TZS 400 milioni.

iii. Kutoza *VAT* kwenye Huduma za Fedha

Mhe. Spika, mwaka jana, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilianzisha utaratibu wa kutoza *VAT* kwenye ada zinazotozwa na Benki katika huduma mbalimbali za Fedha katika Benki za

Biashara. Sisi Zanzibar hatukuanzisha utaratibu huu. Hata hivyo, pamoja na kuzitaka Benki kutotoza Kodi hiyo kwa huduma zinazotolewa Zanzibar, wameendelea kuionesha kodi hiyo bila ya kuilipa Serikalini kwa madai kuwa mifumo yao hairuhusu kutenganisha huduma baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Hivyo inapendekezwa kutoza Kodi hiyo kwenye ada au kamisheni inayotozwa na Benki katika huduma zake na hivyo kuwezesha kuwasilishwa kodi hiyo Serikalini.

iv. Sheria ya Mafunzo ya Amali (*Vocational Training Act*) Namba 8 ya 2006

Mhe. Spika, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 27(4) cha Sheria hiyo ili kuweka bayana namna ya ukadiriaji wa Tozo hiyo na kuleta ufanisi katika ukusanyaji wake.

v. Sheria ya Ajira (*Employment Act*) Nam.11 ya 2005

Mhe. Spika, Imebainika kuwa malipo ya mishahara kwa njia ya fedha taslimu (c*ash basis*) hupelekea ukwepaji wa kodi itokanayo na mishahara (*PAYE*). Utaratibu huo pia umejitokeza kuvutia wahalifu kwa kulenga Wawekezaji wanaolipa mishahara kwa fedha taslimu. Ili kuziba mwanya huo, inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 100(2) cha Sheria hiyo ili iwe ni lazima kwa malipo yote ya mishahara kwa wafanyakazi wa kudumu yafanywe kupitia hesabu zao za benki. Hatua hii inatarajiwa pia kuimarisha usalama kwa kuondoa kishawishi cha uvamizi na wizi katika sehemu za kazi. Jumla ya TZS 600 milioni zinatarajiwa kupatikana kutokana na utekelezaji wa hatua hiyo.

vi. Ada ya Biashara (*Trade Levy*)

Mhe. Spika, pamoja na jitihada mbalimbali za Serikali, bado uwekezaji wetu umeegemea zaidi katika Sekta ya Utalii, hususan katika ujenzi wa hoteli. Bila ya shaka Serikali bado inakaribisha uwekezaji zaidi katika Sekta hiyo. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya 2020, azma ya Serikali ni kujenga uchumi imara, unaohusisha Sekta za Huduma, Viwanda na Kilimo cha Kisasa. Hata hivyo, hadi sasa bado uwekezaji katika viwanda haujapata muitikio wa kutosha.

Mhe. Spika, kumejitokeza malalamiko kwa Wawekezaji wachache wa sekta hiyo dhidi ya kutozwa Ada ya Biashara katika uingizaji wa malighafi na pembejeo za viwanda kunakopunguza uwezo wao wa ushindani na pia kurejesha nyuma uwekezaji katika viwanda. Kwa dhamira ya kurekebisha kasoro hiyo na kuvutia zaidi uwekezaji viwandani, inapendekezwa kusamehe Ada ya Biashara (*Trade Levy*) katika uingizaji wa malighafi na pembejeo za viwandani (*raw materials and industrial inputs*). Haitarajiwi kuwa hatua hii itakuwa na athari ya kupunguza mapato bali itasaidia kuonesha nia ya Serikali ya kuendeleza viwanda nchini.

vii.* Usajili wa Namba Binafsi za Magari (*Private Number Registration)

Mhe. Spika, tokea Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua jitihada za kujenga jamii moja, iliyo sawa na isiyo na matabaka ya kipato wala rangi. Hatua hizi zimesaidia sana kuimarisha umoja wa jamii yetu. Hata hivyo, kwa upande mwengine, serikali pia imeruhusu usajili wa namba binafsi katika gari kwa kutumia herufi na

nambari tofauti na nambari za kawaida. Kwa kiasi fulani utaratibu huu umeonekana kuleta matabaka na hivyo mambo haya mawili hayaendi katika mustakabali mmoja.

Mhe. Spika, Ili kudhibiti matumizi ya nambari binafsi tofauti na zile za kawaida, na ili kuendelea kujenga jamii moja yenye usawa na isiyo na matabaka, inapendekezwa kubadilisha utaratibu na kiwango cha malipo kwa namba binafsi. Kuanzia mwaka wa fedha 2017/18, inapendekezwa kuwa kiwango cha usajili wa namba hizo, kwa gari zilizopo na kwa usajili mpya, kiwe TZS 15.0 milioni kwa mwaka badala ya kiwango cha sasa cha TZS 3.0 milioni kwa miaka mitatu. Kama nilivyoeleza, nia ya hatua hii sio kuongeza mapato bali ni kuendelea kujenga jamii iliyo sawa.

SURA YA BAJETI

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hali ya mapato na matumizi yaliyooneshwa hapo juu, au niliyoyaeleza hapo awali Bajeti ya mwaka 2017/18 inatarajiwa kuhusisha mapato ya jumla ya TZS 1.0874 trilioni. Kati ya fedha hizo, mapato ya ndani ni TZS 675.9 bilioni yanayohusisha pia TZS 11.0 bilioni kutokana na hatua mpya za kuimarisha mapato. Ruzuku na Mikopo kutoka nje ni TZS 380.5 bilioni.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, jumla ya TZS 1.0874 trilioni zinatarajiwa kutumika na hivyo kuacha nakisi ya TZS 30.0 bilioni baina ya mapato na matumizi. Serikali imepanga kukopa katika soko la ndani kiasi hicho cha TZS 30.0 bilioni ili kuziba nakisi hiyo na hivyo kuleta uwiano wa makadirio ya mapato na matumizi. Kati ya jumla ya matumizi hayo, TZS 590.8 bilioni zimepangwa kutumika kwa kazi za kawaida na TZS 496.6 bilioni kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba katika Hotuba yangu ya Bajeti mwaka jana, nilizungumzia pia mwenendo wetu mzuri juu ya Bajeti yetu kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka nje. Nilieleza matarajio ya kupungua kwa utegemezi wa Ruzuku kutoka nje kutoka asilimia 12.2 ya Bejeti ya mwaka 2015/16 hadi asilimia 11.1 mwaka 2016/17. Kutokana na mchango wa Ruzuku ya TZS 82.2 bilioni unaotarajiwa katika Bajeti ya TZS 1.0874 trilioni ya mwaka 2017/18, utegemezi wa Bajeti unatarajiwa kushuka zaidi na kufikia asilimia 7.3 tu.

Sura ya Bajeti

MFUMO WA BAJETI 2017/18					
Maelezo	**Makisio 2016/17**	**Matarajio 2016/17**	**Makisio 2017/18**	**% ya Bajeti**	**% ya Matarajio**
MAPATO					
A Mapato ya ndani	461.4	*509.2*	654.9	*41.9*	*28.6*
B 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	0.0	-	-	-	-
C PAYE kwa W/Kazi wa SMT	21.0	*21.0*	21.0	*0.0*	*0.0*
C Dhamana za Hazina na Hati Fungani	33.0	*8.1*	30.0	*10.0*	
F Msamaha wa Madeni (MDRI)	1.3	*1.3*	0.0	*0.0*	*-100.0*
G Mikopo na Ruzuku	324.8	*150.0*	380.5	*-6.4*	*153.7*
H Mfuko wa Wafadhili (BF)	0.0	-	1.0	-	
Jumla ya Mapato	**841.5**	***689.6***	**1087.4**	***1.3***	***57.7***
MATUMIZI					
Matumizi ya Kawaida	**445.9**	***470.2***	**590.8**	***16.8***	***25.6***
i) Mishahara (Wizara)	223.8	*223.8*	295.6	*8.7*	*32.1*
ii) Mishahara (Ruzuku)	26.7	*26.7*	30.3	*-6.6*	*13.6*
iii) Matumizi Mengineyo (Wizara)	82.9	*90.0*	100.6	*-1.7*	*11.7*
iv) Matumizi Mengineyo (Ruzuku)	31.1	*31.1*	64.3	*9.1*	*106.6*
v) Mfuko mkuu wa Serikali (CFS)	81.4	*98.6*	100.0	*-3.3*	*1.4*
Matumizi ya Maendeleo	**395.6**	***217.0***	**496.6**	**-0.8**	***128.9***
i) Mchango wa Serikali	70.8	*67.0*	116.1	*36.5*	*73.3*
ii) Mikopo na Ruzuku	324.8	*150.0*	380.5	*-6.4*	*153.7*
Jumla ya matumizi	**841.5**	***687.2***	**1087.4**	**1.3**	***58.2***

Mhe. Spika, kipindi cha kwanza cha awamu ya saba kilianza mwaka wa fedha 2010/11. kibajeti, kumetokea mabadiliko makubwa baina ya mwaka huo na sasa. Mtakumbuka kuwa mwaka huo, Bajeti ya Serikali ilikua jumla ya TZS 444.6 bilioni tu hivyo Bajeti imepanda kwa asilimia 144.6 hadi sasa. Aidha, mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa TZS 171.7 bilioni ambapo mapato yatokanayo na kodi yalikadiriwa kufika TZS 161.0 bilioni. Ikilinganishwa na makadirio ya mapato ya ndani ya TZS 675.8 bilioni kwa mwaka 2017/18, hii inaashiria kuwa mapato yetu yamekuwa kwa zaidi ya mara tatu (asilimia 319.8).

Mhe. Spika, kwa upande wa utegemezi wa Bajeti, kwa mwaka 2010/11 jumla ya Ruzuku na Misaada ya Kibajeti ilikadiriwa kuwa TZS 134.2 bilioni sawa na utegemezi wa Bajeti wa karibu thuluthi moja (asilimia 30.2). Aidha, kwa kuzingatia makadirio ya matumizi ya kawaida ya mwaka huo ya TZS 193.4 bilioni, taswira ni kwamba mapato ya ndani hayakuweza kukidhi hata matumizi yetu ya kawaida ya kulipa mishahara, kuendesha Serikali na kugharamia Mfuko Mkuu wa Serikali. Hivyo, kama ilivyo kwa nakisi ya matumizi ya kawaida dhidi ya mapato ya ndani ya TZS 21.7 bilioni, mchango wa Serikali katika Kazi za Maendeleo wa TZS 39.5 bilioni ulitokana na Misaada ya Kibajeti kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, tusighafilike, mwaka 2010 kima cha chini cha mshahara Serikalini kilikuwa Shilingi laki moja. Leo hii ni Shilingi laki tatu, mara tatu ya kiwango kilichokuwepo wakati Mhe. Dkt. Shein anachukua dhima ya kutuongoza.

Mhe. Spika, nayasema haya sio kwa nia ya kukebehi utendaji wetu wa miaka iliyopita. Nayakumbusha ili sisi sote tuweze kutambua, kuthamini na kushukuru maendeleo makubwa tuliyoyapiga katika miaka sita hii ya awamu ya saba ya kujitawala, chini ya uongozi wa Dkt. Ali

Mohamed Shein. Mapendekezo ninayowasilisha leo yanaonesha kuwa sasa tumeweza kujitegemea kutokana na fedha zetu za ndani katika malipo ya mishahara na stahili nyengine zilizoimarishwa za wafanyakazi wetu, fedha za kuendeshea serikali na pia kumudu kutoa mchango mkubwa, takribani robo, katika Bajeti ya Kazi za Maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, haya ni mafanikio makubwa sana tuliyopiga katika kipindi kifupi. Sote hatuna budi kuyapongeza. Hii ni ishara bayana kuwa tukidhamiria, na chini ya uongozi imara, tunaweza. Tuungane kuendeleza jitihada hizi za kuimarisha uwezo wetu wa ndani sambamba na ukuzaji wa uchumi wetu katika kipindi kilichobakia cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, moja ya vipaumbele vya bajeti ya mwaka huu itaendelea kuwa ni uimarishaji wa elimu. Bado sehemu kubwa ya jamii yetu inaundwa na watoto wanaostahiki kupata elimu ili waweze kumudu vyema mahitaji ya baadae ya kilimwengu ya kiuchumi na kijamii. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha elimu, ikiwemo kuwekeza katika miundombinu muhimu kama vile majengo ya skuli za kisasa, maabara na vitabu. Serikali pia imebeba jukumu kubwa zaidi kwa kuondoa michango kwa wazazi katika elimu ya msingi na jukumu la kugharamia mitihani ya elimu ya msingi na sekondari. Kutokana na mahitaji makubwa ya kifedha kwa kuhudumia elimu, Serikali itaanzisha Mfuko wa Elimu kuanzia mwaka ujao wa fedha. Mbali ya fedha zitakazokuwa zikitengwa na Serikali kwa madhumuni hayo, wananchi, Kampuni binafsi, mashirika ya kimataifa na wafadhili wengine wanakaribishwa kuchangia katika mfuko huo muhimu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka huu inaashiria mageuzi makubwa. Tumezungumzia mageuzi katika mfuko wa Bajeti yetu ambayo kwa kiasi kikubwa tunaelekea kwenye kutumia wenyewe sehemu kubwa ya mapato yetu; tumezungumzia mageuzi yanayopelekea huduma muhimu kutolewa karibu zaidi kwa wananchi na kwa uwajibikaji mkubwa kwao na kuendelea kuimarika kwa huduma za jamii, ikiwemo kuanzishwa kwa mfuko maalum wa elimu pamoja na usogezaji karibu zaidi wa huduma kwa wananchi kupitia katika mfumo mpya wa Madaraka Mikoani (Ugatuzi). Kwa kuzingatia mageuzi yote haya, Bajeti ya mwaka huu inastahiki kuitwa 'Bajeti ya Mageuzi na Huduma Bora za Jamii'. *(Makofi)*

Hapa Mhe. Spika, naomba uniruhusu kurejea kwa kuzingatia mageuzi yote haya, Bajeti ya mwaka huu inastahiki kuitwa Bajeti ya Mageuzi na Huduma Bora za Jamii.

SHUKRANI

Mhe. Spika, kama ilivyo desturi, matayarisho ya mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/18 yameshirikisha viongozi na watendaji mbalimbali, Serikalini na kwa kiasi pia sekta binafsi. Siwezi kumaliza hotuba hii bila ya kutambua mchango wa wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kufanikisha mapendekezo haya ambayo leo hii nayawasilisha kwenu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tunashukuru sana sana kwa mashirikiano yote tuliyopatiwa yaliyochangia sana maandalizi haya.

Mhe. Spika, kufuatia marekebisho ya Kanuni za Uendelezaji wa Baraza letu, kwa mara ya kwanza katika historia ya Baraza letu Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali yamewasilishwa

kwenye Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, chini ya uongozi weledi wa Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed *(*Dimwa*).* Kamati imeyajadili kwa kina mapendekezo haya na tunathamini sana upeo mkubwa wa mawazo ya Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti na Wajumbe mahiri wa Kamati hivyo. Michango yao imesaidia sana kuibua fikra mpya na kuisaidia Serikali katika mazingatio ya mambo mengine muhimu.

Mhe. Spika, Kamati pia imepokea na kuzingatia Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 ambao imeujadili kwa kina. Pia tunaishukuru sana na naomba hapa nifanye masahihisho tunaishukuru sana Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipitia, kuijadili na kuipitisha Miswada ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Sheria ya Ushuru wa Stempu, na kutoa maelekezo na maoni yao ambayo yamesaidia sana kuimarisha Miswada hiyo kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza lako. Tunaishukuru sana Kamati hii kwa mashirikiano mazuri inayotupatia.

Mhe. Spika, matayarisho ya Bajeti hii yamehusisha mashirikiano makubwa ya Watendaji mbalimbali Serikalini. Naushukuru sana uongozi wa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dr. Abdulhamid Yahya Mzee, na Makatibu Wakuu wote kwa mchango wao katika matayarisho ya mapendekezo haya. Ni maoni yao ndio yalisaidia kukamilishwa Mapendekezo haya ya Bajeti na kuiruhusu Wizara ya Fedha na Mipango kuyawasilisha Baraza la Mapinduzi na hatimae, leo hii, hapa katika Barazani la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee, nashukuru sana mashirikiano na utendaji bora wa Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na Tume ya Mipango. Kwa ujumla wao, naomba kuwashukuru kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bwana Khamis Mussa Omar, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango - Bwana Juma Hassan Reli, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango - Bwana Ali Khamis Juma, Mhasibu Mkuu wa Serikali - Bi Mwanahija Almas Ali, Kamishna wa Bajeti – Bwana Mwita Mgeni Mwita, Afsa Mdhamini Pemba Ibrahim na watendaji wote wa Wizara na Tume ya Mipango. Kazi yao kubwa sote tunaithamini sana.

Mhe. Spika, Zanzibar ni Kisiwa lakini kiulimwengu, tunaishi na kushirikiana na mataifa na mashirika mbalimbali. Kuna wakati tunakubaliana kwa mambo mengi na kuna wakati tunatofautiana kwa baadhi yake, lakini bado tunaendelea kushirikiana. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi, nachukua fursa hii kushukuru sana uhusiano wetu na msaada wa nchi za Canada, China, Cuba, Denmark, Falme za Kiarabu, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mashirika ya Kimataifa, naomba nitambue na kushukuru misaada ya mashirika yafuatayo*: ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO na WSPA. (Makofi)*

Mhe. Spika, kabla ya kutoa hitimisho naomba nieleze kwamba naelewa kuwa ili kuimarisha usimamizi wa Baraza la Wawakilishi kwa Serikali Baraza letu la Wawakilishi limebadilisha kanuni zake, ambapo miongoni mwa mambo mengine imeanzisha kamati mpya ya bajeti. Nimebahatika kukutana na kamati hii mara tatu awali nilipowasilisha mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018, baadae nilipowasilisha Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 pamoja na Miswada ya Ushuru wa Bidhaa na ule ushuru wa Stemp, mara ya tatu ni juzi na jana wakati tulipokutana kushauriana juu ya hoja zilizojitokeza wakati wa majadiliano ya bajeti ya Wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, nayasema haya kwa sababu ya kuweka *Hansard* sawa kwa bahati mbaya sana nimemsikia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti akisema kuwa mimi Waziri wa Fedha na Mipango sikutoa mashirikiano mazuri kwa kamati hiyo, nasema hii ni bahati mbaya kwa sababu tukio pekee ninalolikumbuka ni mjadala namna ya kuendesha mashauriano hayo kwa kuzingatia kuwa Bajeti hizo zote za Mawizara zilikwisha pitishwa na Baraza lako tukufu. Tulichokitaka kupatiwa ufafanuzi kabla ya kuanza mjadala ni kwamba je tunao uwezo wa kubadilisha vifungu ambavyo tayari Baraza lako tukufu lilikwisha, kamati ya Matumizi ya Baraza lako tukufu ilikwishapitisha.

HITIMISHO:

Na baada ya mashauriano na kukubalika kuwa kikao cha Kamati kiendelee sote tulishirikiana kwa ukamilifu na Kamati, mimi binafsi nilishiriki vikao vyote siku zote mbili tokea vilivyoanza mpaka kumalizika. Sasa namshauri sana ndugu yangu Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) mashauriano tuliyoyafanya pale yalikuwa kwa nia safi ya kuweza kukubaliana na utaratibu kwa kuelewa kwamba Baraza hili ni chombo muhimu sana, na sisi wengine tulikuwa na hofu Mhe. Spika, ya kwamba vifungu vile visibadilishwe wakati tayari vilikwishapitishwa na Kamati ya Matumizi ya Baraza la Wawakilishi.

Lakini nitaomba Mhe. Spika, kwamba hii itatusaidia pia kufikiria namna bora zaidi ya kuimarisha kanuni zetu za uendeshaji wa Baraza Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na baada ya maelezo yangu niliyoyatoa awali kwa heshima kubwa sana sasa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ambapo Serikali imekadiria kukusanya jumla ya Shs. 1,087,400,000,000/= kati ya mapato hayo Shs. Bilioni 675.9 za Mapato ya ndani na Shs. bilioni 380.5 zinazotokana na ruzuku na mikopo kutoka nje na Shs. Bilioni 30 za mikopo ya ndani.

Mhe. Spika**,**vile vile, kwa heshima kubwa, kwa mwaka huo wa 2017/18, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Themanini na Saba na Milioni Mia Nne (TZS 1.0874 Trilioni). Kati ya fedha hizo, Baraza linaombwa kuidhinisha Matumizi ya kazi za kawaida ya TZS 590.8 bilioni na yale ya kugharamia Mpango wa Maendeleo ya TZS 496.6 bilioni.

Mhe. Spika, Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kunipa nafasi nikaeleza utaratibu natumia Kanuni 52 lakini hoja yagu iko katika Kanuni ya 58.6 katika suala zima la muda wa kuchangia. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameeleza amesoma hutuba, amesoma Mpango pamoja na Hutuba mimi nipo Barazani hapa kipindi kirefu sana lakini kwa mara ya mwanzo sana kwa kweli katika hotuba ya Bajeti ya Mwaka huu ni bajeti ya aina yake inahitaji mchango mkubwa na inahitaji mawazo mengi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri, katika ukurasa wa 51 kifugu cha 103 alielezea kwamba hii ni bajeti ya Mageuzi na Huduma bora za Jamii lakini mimi nimekwenda mbali zaidi kwa sababu hutuba hii mimi naita hotuba ya bajeti ya matumaini, kwa hivyo Mhe. Spika, tunaomba sana tunajua leo hatuchangii bajeti lakini ile siku tutakazoanza kuchangia bajeti tunaomba sana Mhe. Spika, utupe muda wa kutosha kwa sababu tuna vitabu hivi karibu 13 vyote vimo katika bajeti hii kuu ya Serikali. Kwa hivyo tunahitaji tuseme vizuri sana na tuipongeze Serikali yetu kwa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia mia moja na ziada.

Sasa Mhe. Spika, hoja yangu niliyosimama ni hiyo ili utupe nafasi nzuri Wajumbe pamoja na kwamba umetupa zaidi ya siku tatu, lakini ule muda uliokuwemo kwenye kanuni uutumie vizuri au utumike vizuri tuweze kujenga hoja kuishauri Serikali yetu vizuri. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma hilo litazingatiwa na hasa kwa vile mtakuwa nma siku nyingi siku tatu kwa ajili ya kuchangia kwa hivyo muda utazingatiwa na utaheshimiwa. Mhe. Waziri wa Fedha ahsante nitoe Shukurani zangu kwa namna ulivyowasilisha kabla hatujaendelea naomba nitoe tangazo. Kwanza naomba kuwatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti wanatangaziwa na Mwenyekiti wa Kamati yao mara baada ya kuakhirisha hapa basi wanaombwa wakutane ukumbi namba mbili kuna kikao kifupi kinafanyika.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nichukue nafasi kuwatangazia wageni wetu ambao wamefika leo kwenye *Gallary* kundi la mwanzo la viongozi mbali mbali Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mhe. Ayoub Mohammed Mahamoud, karibu sana kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa ya Zanzibar, Mgeni wetu wa pili ni Mhe. Spika, mstaafu Mhe. Pandu Ameir Kificho karibu sana mzee wetu karibu tunaendeleza shughuli ambazo umetupasia. Anayefuata ni Balozi mdogo wa India Mister T.C Barupal kwa niaba ya Mabalozi wenzake na Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa ziliopo hapa Zanzibar.

Viongozi wanaoufuata sasa ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Abdulhamid Yahya Mzee, Pia nitawaomba Makatibu Wakuu pamoja na Manaibu Makatibu Wakuu wote kwa pamoja msimame mliopo, karibuni sana.

Kundi jengine la Viongozi ni Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama Kamanda Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ahsante mmesimama kwa pamoja, kuna Kamanda wa Jeshi *JWTZ* Nyuki Brig, Kamanda wa Polisi Zanzibar, Kamanda wa *KMKM*, Mkuu wa *JKU*, Kamanda wa Chuo cha Mafunzo, Kamana wa Vikosi vya Valantia, Kamanda wa Zimamoto na Uokozi, Naibu Mkurugenzi Idara ya Uhamiaji.

Kundi jengine ni baadhi ya Wakurugenzi na viongozi wengineo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar (*CAG*) karibu, Naibu Mwanasheria Mkuu karibu sana, Mkurugenzi wa Uchaguzi, wengine watakuwa wamekwenda kusali Mkurugenzi wa Mashitaka *DPP* nae pengine atakuwa miongoni wa waliokwenda Msikitini, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Mugheri karibu, Mkurugenzi *Chember of Commerce*, Mkurugenzi Mtendaji *PBZ*, Mkurugenzi ZSSF, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamishna wa Bajeti karibu, Kamishna wa *ZRB*, Mufti Mkuu wa Zanzibar, itakuwa kenda msikitini, Kadhi Mkuu wa Zanzibar yupo, Katibu wa Mufti, Mkurugenzi Habari Maelezo.

Pia wapo baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa, Naibu Katibu Mkuu wa *CCM* karibu, Mwenyekiti wa *CCM* Mkoa wa Magharibi hayupo yuko msikitini, Mwenyekiti wa *CCM* Mkoa wa Mjini, Naibu Katibu Mkuu *TADEA* karibu sana, Katibu Mkuu ADC, Naibu Katibu Mkuu *ACT* Wazalendo.

Wageni wengine ni Wakuu wa Vyuo VC Zanzibar State University, VC - Alsumait University - Chukwani karibu, VC Zanzibar University.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya Tangazo hilo la wageni Katibu shughuli inafuata.

Katibu: Kwa vile orodha yetu ya shughuli zetu za Baraza za leo zimemalizika naomba sasa uliahirishe Baraza.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile hakuna shughuli inayofuata baada ya hapo naomba sasa naomba niahirishe Kikao cha Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Alhamis tarehe 15/06/2017 saa 3.00 za asubuhi.

(Saa 6.53 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 15/6/2017 saa 3.00 asubuhi)